# ATHARI ZA KIMAENDELEO KATIKA MUKTADHA WA NYIMBO ZA NGOMA YA MBASSA YA JAMII YA WACHAGGA


Na

Kolman Aloyce Mboya


Tasnifu kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma


Chuo Kikuu cha Dodoma

Septemba, 2012

## ITHIBATI

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma na anapendekeza tasnifu hii inayoitwa: ***"Athari za Kimaendeleo katika Muktadha wa Nyimbo za Ngoma ya Mbassa ya Jamii ya Wachagga"*** ikubaliwe kwa minajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma

……………………….

Dkt. Frowin Paul Nyoni

(MSIMAMIZI)

Tarehe: …………………

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi **Kolman Aloyce Mboya**, ninatamka na kuthibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halali, ambayo haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada inayofanana na hii au nyingine yoyote.

Sahihi: …………………………….

Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili wala kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa maana yoyote ile bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu cha Dodoma.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa ninatanguliza shukrani zangu kwa Mweneyezi Mungu ambaye ndiye muumba wa vyote, amenijalia uhai, afya, nguvu na uwezo wa kufanya kazi hii.

Kazi hii ni matokeo ya miongozo na michango ya watu mbalimbali, hivyo katika shukrani zangu za pili ninaomba ziende kwa msimamizi wangu wa kazi hii ambaye ni Dkt. Frowin Paul Nyoni kwa kunishikilia usukani wa tasnifu hii toka mwanzo hadi kuhakikisha nimeikamilisha.

Tatu, ninawashukuru walimu walioniwezesha kufikia lengo la kupata Shahada hii ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili, nikianza na Prof. Joshua Madumulla, Prof. Lakshnmanan, Dkt. Elias M. Songoyi na Dkt. Rafiki Sebonde wote hawa ni walimu walionifundisha darasani na kunisimamia kwa kuhakikisha kwamba nimefaulu.

Nne, ninawashukuru Dkt. P.D Maimu, Dkt Adam O. Korogoto na Bi Asha R. Changai (Katibu muhtasi wa Idara ya Kiingerza) wote wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa kunipa maoni mawazo, makala, vitabu na tasnifu mbalimbali vyote hivyo vilisaidia katika kufanikisha kazi hii ya utafiti.

Tano ninawashukuru viongozi mbalimbali wa serikali na taasisi zake, baadhi yao ni Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mheshimiwa L. Gama, kwa kuniruhusu kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali ya mkoa wake na Mheshimiwa Josephy Mngere Mushi Diwani Kata ya Kindi. Pia ninamshukuru Mkurugenzi mtendendaji wa Wilaya Rungwe Mkoa wa Mbeya Ndugu Noel Mahyenga na Afisaelimu wa Wilaya ya Rungwe Ndugu I.A.A Kameka kwa kunikubalia kwenda kusoma Shahada hii ya Umahiri wa Kiswahili.

Sita, katika shukrani zangu za dhati na kwa namna ya pekee, ninamshukru sana mke wangu, Severa J.K Mushi kwa kunitia moyo, mbali ya kwamba alikuwa amelazwa hospitalini. Watoto wangu Josephat Colman, Leodgar Colman, Glorier Colman, Silvanus Colman na Gudllar Mathew, waliweza kuishi kwa kushirikiana peke yao kwa kipindi chote nilichokuwa masomoni, hali mama yao akiwa amelazwa hospitalini Dar es Salaam.

Mwisho ninawashukuru sana walimu wangu wa Darasa la Awali na Kwanza katika Shule ya Msingi Kindi Juu, Wilaya ya Moshi Vijijini Mkoa wa Kilimanjaro, Mzee Leoni Mallya na Mama Monica Augusti kwa kunionesha njia hadi hapa nilipofikia. Kwa kumalizia shukrani niawashukuru wale wote wengine ambao walisaidia kufanikisha utafiti huu, wakiwemo watafitiwa wote ambao majina yao yameambatanishwa kwenye kiambata.

# IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa*. Nyimbo za ngoma ya *Mbasssa* zilikuwa zinaimbwa katika muktadha wa unyago. Kwa sasa nyimbo hizi haziimbwi katika muktadha wa unyago kutokana na mabadiliko ya kimaendeleo, yakiwemo masuala ya utandawazi, mabadiliko ya sayansi na teknolojia, kupanuka kwa kiwango cha elimu, kubadilika kwa mfumo wa siasa, masuala ya kibiashara na mwingiliano katika tamaduni, kumeathiri nyimbo za ngoma ya *Mbassa*. Nyimbo hizi bado zipo na zinaimbwa katika miktadha ya sherehe za harusi, sherehe za kidini na kwenye kampeni za kisiasa.

Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni ya Kihemenitiki. Nadharia hii inatizama maana ya fasihi, namna fasihi inavyohusiana na kusudi la mwandishi, na kama inakuwa rahisi kupata uelewaji wa ndani wa kazi ya fasihi kutegemeana na mazingira na historia ya hadhira inayohusika. Nadharia hii imesaidia kubaini na kuchambua mada ya utafiti ambayo inahusiana na athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa.*

Utafiti huu ulitumia mbinu mbalimbali zikiwemo mbinu ya udadisi, mbinu ya kusogezeana, mbinu ya uchaguzi holela, mbinu ya ufafanuzi wa matini pia ilitumika mbinu ya mchakato wa ukusanyaji data na udhibiti wake.

Matokeo ya utafiti yalizingatia suala la kimuktadha katika kuchambua maudhui ya ngoma ya *Mbassa*, kujua namna maudhui hayo yanayosawiri katika jamii ya sasa. Pia matokeo ya utafiti yalitizama namna nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zinazoimbwa wakati huu kama zinaendana au zinasawiri mabadiliko ya kimaendeleo katika jamii.

**YALIYOMO**

ITHIBATI ..... i
IKIRARI NA HAKIMILIKI ..... ii
SHUKRANI ..... iii
IKISIRI ..... v
YALIYOMO ..... vi

SURA YA KWANZA ..... 1
1.1 Utangulizi ..... 1
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ..... 1
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti ..... 2
1.4 Malengo ya Utafiti ..... 4
1.4.1 Lengo la Jumla la Utafiti ..... 4
1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti ..... 4
1.6 Eneo la Utafiti ..... 4
1.7 Umuhimu wa Utafiti ..... 6
1.8 Mipaka ya Utafiti ..... 6
1.9 Hitimisho ..... 6

SURA YA PILI ..... 8
MAPITIO YA MAANDIKO ..... 8
2.1 Utangulizi ..... 8
2.2 Machapisho yanayohusiana na Fasihi Simulizi ..... 9
2.3 Ufafanuzi kuhusiana na Maudhui ..... 12
2.4 Ufafanuzi kuhusiana na Nyimbo ..... 13
2.5 Ufafanuzi Kuhusiana na Jamii ya Wachagga ..... 26
2.5.1 Historia na Maisha ya Jaamii ya Wachagga ..... 26
2.5.2 Utamaduni wa Jamii ya Wachagga ..... 28
2.5.3 Mila na Desturi za Jamii ya Wachagga ..... 28
2.5.4 Mafunzo ya Jando na Unyago ..... 30
2.5.5 Dini katika Jamii ya Wachagga ..... 32
2.5.6 Uchumi wa Jamii ya Wachagga ..... 33
2.6 Nadharia iliyotumika kwenye Utafiti ..... 33
2.7 Mwanya wa Utafiti ..... 35

2.8 Hitimisho ........................................................................................................ 36

SURA YA TATU .................................................................................................... 37
MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI ...................................................................... 37
3.1 Utangulizi ......................................................................................................... 37
3.2 Mpango wa Jumla wa Utafiti ........................................................................... 37
3.3 Zana za Kukusanyia Data ................................................................................ 38
3.4 Njia/Mbinu za kukusanyia data ....................................................................... 38
3.4.1 Mahojiano ...................................................................................................... 40
3.4.2 Mbinu za Utafiti ............................................................................................. 40
3.4.3 Mbinu ya kusogezeana .................................................................................. 41
3.4.4 Mbinu ya Uchaguzi Holela ............................................................................ 42
3.4.5 Mbinu ya Ufafanuzi Matini ........................................................................... 42
3.5 Mchakato wa Ukusanyaji Data na Udhibiti wake ........................................... 42
3.6 Sampuli ya Watafitiwa ..................................................................................... 43
3.7 Mipaka ya Utafiti ............................................................................................. 44
3.8 Changamoto katika ukusanyaji wa data ........................................................... 44
3.9 Hitimisho ......................................................................................................... 45

SURA YA NNE ..................................................................................................... 46
UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI ........ 46
4.1 Utangulizi ......................................................................................................... 46
4.2 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data zilizokusanywa ..................................... 46
4.2.1 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Lengo la Kwanza ........................................ 47
4.2.2 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Lengo la Pili ................................................ 70
4.3 Matokeo ya Utafiti ........................................................................................... 85
4.3.1 Athari za Kimaendeleo katika Muktadha wa Nyimbo za Ngoma ya Mbassa ya Jamii ya Wachagga ........................................................................................................ 85
4.3.2 Maudhui ya Nyimbo za Ngoma ya Mbassa Yanavyoakisi Mabadiliko Yanayotokea katika Jamii. ........................................................................................................ 85
4.3.3 Nyimbo za Ngoma ya Mbassa Zinavyosawiri Mabadiliko ya Sasa katika Jamii ....... 87
4.4 Hitimisho ......................................................................................................... 89

SURA YA TANO ..... 90
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 90
5.1 Utangulizi ..... 90
5.2 Uchambuzi wa Data Zilizokusanywa ..... 90
5.2.1 Mafunzo yaliyotokana na Nyimbo za Ngoma ya Mbassa ..... 91
5.3 Athari za Kimaendeleo katika Muktadha wa Nyimbo za Ngoma ya Mbassa ..... 91
5.4 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo ..... 92

MAREJELEO ..... 93
KIELELEZO: NA. 1 MTAFITI AKIWA NA MANJU ALIYEHOJIWA ..... 98
KIELELEZO: NA. 2 PICHA ZA MANJU WALIOHOJIWA ..... 99
KIELELEZO: NA. 3 PICHA YA MTAFITIWA AKIJAZA DODOSO ..... 100
KIELELEZO: NA 4 NYUMBA YA JADI ..... 101

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Lengo la utafiti huu ni kuchunguza athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa.* Katika sura hii, mtafiti amejikita katika vipengele vya: usuli wa tatizo, tamko la utafiti, madhumuni ya jumla na mahsusi ya utafiti, maswali ya utafiti, eneo la utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti. Kwa sehemu kubwa katika kushughulikia vipengele hivi, mtafiti amejikita katika utafiti wa maktabani na uwandani katika kubaini athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Utafiti huu umekusudia kuchunguza athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachaga. Lengo kuu la kufanya utafiti huu ni kuonyesha na kuthibitisha kuwa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zinaweza kuathiriwa kutokana na mabadiliko ya kimaendeleo, hususan zinapoimbwa katika miktadha tofauti na muktadha ambao ulikuwapo kwa wakati huo. Muktadha ambao nyimbo hizi zilikuwa zinaimbwa ni kwenye unyago. Lakini kwa sasa zinaimbwa kwenye miktadha mbalimbali ikiwemo ya harusi, dini na siasa. Kubadilika kwa muktadha ambao nyimbo hizi zilikuwa zinaimbwa, kumeathiri uwasilishaji, hadhira, mandhari, fanani na fani inayotendwa. Kwa kuwa utafiti unajihusisha na muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa*, na kwa kuwa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zinahusiana na jamii ya Wachagga, nyimbo zitakazokuwa zinawasilishwa zitakuwa zinatumia lahaja ya Kichagga. Wamitila (2003:152) katika suala la muktadha anasema kwamba muktadha ni dhana ambayo inaelezea mazingira ya kilugha na kijografia ya kazi ya kifasihi. Aidha katika muktadha wa kijografia au wa kilugha

unaweza kuwa finyu au mpana kutegemeana na kazi ya fasihi inayochunguzwa. Kwa kuwa mtafiti anachunguza nyimbo za ngoma ya *Mbassa*, ambazo zitakuwa na mistari mingi ya kilugha, basi muktadha wake utakuwa mpana (yaani wa mbali). Katika nyimbo za ngoma ya *Mbassa*, mtafiti amajihusisha na msamiati uliotumika katika nyimbo hizo kama hali finyu, pia katika hali ya kijgrafia kwa kuangalia wimbo wote kama ulivyoimbwa na msanii. Kuna baadhi ya waandishi ambao wameandika kuhusiana na suala la nyimbo za ngoma wakiwemo Halima Khamis Suleiman (2012), Esther Massele (2012), Hassan Gora Haji (2011), Ahmed Salim Daud (2012) na Elias Songoyi (2005). Kupitia nyimbo hizi za ngoma za jamii zingine ambazo zimechambuliwa na wataalam hao, zimemwezesha mtafiti kuchambua mada ya utafiti inayohusiana na athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa*. Nyimbo hizi za ngoma ya *Mbassa* kidhima zinatofautiana na za makabila mengine, na hata kwenye namna ya uchezaji, uwasilishaji na maana ya maneno yanayotumika katika wimbo katika muktadha husika. Aidha, mtafiti anatarajia kwamba kutokana na mabadiliko ya kimaendeleo katika jamii ya Waachagga ambayo yanachangiwa na biashara, elimu, utandawazi kwa maana ya sayansi na teknolojia na mabadiliko ya kutoka mfumo wa chama kimoja cha siasa na kuingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa, nyimbo za ngoma ya *Mbassa* kimuktadha haziwezi kuendana na mabadiliko ambayo yametokea katika makabila hayo mengine. Kwa sababu hizo ndiyo maana mtafiti amepata ushawishi na hamasa ya kuamua kufanya utafiti kuhusiana na athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga.

## 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Tatizo la utafiti huu ni kuchunguza na kubainisha athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga. Mtafiti amefikia uamuzi huu wa

kufanya utafiti kutokana na kwamba amewapitia wataalam mbalimbali walioshughulikia suala la nyimbo za ngoma, hususan nyimbo za ngoma ya jamii ya Wachagga, kwa hiyo, mtafiti amegundua kwamba eneo hilo la athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga, bado halijashughulikiwa kikamilifu. Kuna baadhi ya waandishi ambao wameshughulikia suala la nyimbo katika jamii ya Wachagga, lakini kwenye maeneo mengine ya nyimbo wakiwemo, D.P Minja (2000), ameandika kuhusu mabadiliko ya nyimbo za arusi kwenye Jamii ya Wachagga. R.E.K Massawe (1995), ameandika kuhusu mwelekeo wa Fasihi ya Ushairi wa Kichagga kwenye nyimbo za dini ya Kikristo na Grace Mmbando (2004) ameandika kuhusu nafasi ya nyimbo za kijadi za arusi katika jamii ya Wachagga. Pamoja na hao, kuna waandishi wengine walioandika kuhusiana na nyimbo za ngoma za jamii zingine wakiwemo Halima Khamis Suleiman (2012), ameandika kuhusu nyimbo za ngoma ya Pungwa, Esther J. Massele (2012) ameandika kuhusu nyimbo za Wanaume na wanawake wa Kisukuma, Hassan Gora Haji (2011) ameandika kuhusu mitindo ya nyimbo za uganga wa pepo na Ahmed Salim Daud (2012) ameandika kuhusiana na nyimbo za ngoma ya daku katika mtizamo wa kifasihi. Kwa kuwa fasihi simulizi hutofautiana kutoka jamii moja na nyingine, hususani kwenye nyanja ya nyimbo, ni wazi kwamba nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zitakuwa tofauti na nyimbo za makabila hayo mengine katika vipengele vya mandhari, wahusika na hata namna ya uchezaji. Pia maudhui katika vipengele vya ujumbe, msimamo na mtazamo wa jamii hutofautiana. Kwa msingi huo tunaona kwamba waandishi na watafiti hawa watakuwa wamegusia maeneo mengine katika jamii hizo, lakini siyo athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga. Hali hii ndiyo inayompa mtafiti ari na msukumo wa kuamua kufanya utafiti katika eneo hili ambalo linaonesha bado kushughulikiwa kikamilifu.

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Katika utafiti huu malengo yake yamegawanyika katika sehemu mbili, sehemu ya kwanza lengo la jumla na sehemu ya pili malengo mahsusi.

#### 1.4.1 Lengo la Jumla la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga.

#### 1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti

a) Kukusanya nyimbo za ngoma ya *Mbassa* kutoka jamii ya Wachagga na kuchambua maudhui yake.

b) Kuchunguza na kubainisha athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga.

### 1.5 Maswali ya Utafiti

a) Je, nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga zina maudhui gani?

b) Je, kuna athari gani za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa*?

### 1.6 Eneo la Utafiti

Utafiti ulifanyika katika Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Moshi Vijijini, hususan Tarafa ya Kibosho. Mkoa wa Kilimanjaro kwa upande wa Kaskazini Mashariki umepakana na nchi ya Kenya, Kusini umepakana na Mkoa wa Tanga, Kaskazini umepakana na Mkoa wa Manyara na Magharibi umepakana na Mkoa wa Arusha. Aidha, maeneo mengine yaliyohusika katika utafiti huu ni Vyuo Vikuu vya Mwenge-Moshi, na Dodoma. Maeneo haya ya utafiti yamekusudiwa kwa sababu, mkoa wa Kilimanjaro ndiko iliko mada

inayofanyiwa utafiti na ndiko anakotoka mtafiti pia mtafiti alitumia Chuo Kikuu cha Mwenge-Moshi katika kusoma maandiko mbalimbali. Mkoa wa Dodoma, eneo hili ndiko kuliko Chuo Kikuu anachosoma mtafiti pia msimamizi wa utafiti anatoka Chuo Kikuu cha Dododma. Mkoa wa Dar es Salaam, eneo hili limewekwa kwa sababu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho mtafiti amekitumia katika kupata maandiko mbalimbali zikiwemo tasnifu za watafiti wengine.

**KIELELEZO: RAMANI YA MKOA KILIMANJARO NA MIPAKA YAKE**




**Ufunguo**: ___.____.___ Mipaka ya mkoa

-- -- -- -- -- -- -- Mipaka ya Wilaya

___________ Mipaka ya Nchi

N

## 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Kukamilika kwa utafiti huu si kwamba kutasaidia jamii ya Wachagga tu, bali utapanua uelewa mkubwa kuhusiana na fasihi simulizi ya Kiswahili. Wasomaji wa tasnifu hii watapata changamoto ya kutaka kuchunguza nyimbo za ngoma za jamii zingine zilizomo Tanzania. Vijana wengi watahamasika kucheza na kuimba nyimbo za asili zinazotokana na jamii zao na kuacha kuiga nyimbo za tamaduni za nje. Pia utafiti huu utasaidia kutaka kuzifahamu nyimbo za ngoma za jamii nyingine za Kitanzania, kwa kuwa jamii hizo zitataka kuhusianisha maudhui ya nyimbo zao na ya hizo za jamii nyingine.

## 1.8 Mipaka ya Utafiti

Utafiti umefanyika katika Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Moshi Vijijini hususan eneo la Tarafa ya Kibosho. Kwa kuwa Utafiti umejikita katika athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga, mtafiti alifanikiwa kuwapata watafitiwa wote waliolengwa kutoka katika eneo la utafiti. Watafitiwa hao ni kundi la wanaume na wanawake kumi kila jinsi, kundi la Manju sita, wanaume watatu na wanawake watatu na kundi la vijana wasichana na wavulana kumi kila jinsi. Aidha makundi haya yameteuliwa ili kuweza kubainisha vyema athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa.* Kwa kuwa fasihi hubadilika kutokana na wakati, ni wazi kwamba athari zitajitokeza katika vipengele vya mandhari, fanani, hadhira, tukio na hata fani inayotendwa. Hivyo makundi yaliyoteuliwa yatasaidia sana kubainisha vipengele hivyo.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii ya kwanza ilikuwa inatoa mwongozo wa utafiti ikiwa na vipengele vya Usuli wa Tatizo, Tamko la Tatizo la Utafiti, Malengo ya Utafiti na Maswali yake, eneo la utafiti,

Umuhimu wa Utafiti na mipaka ya utafiti. Kukamilika kwa sura hii kunamwezesha mtafiti kuingia katika sura ya pili inayohusiana na maandiko ambayo yatapitiwa yakihusianishwa na mada inayotafitiwa ambayo ni athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga. Maandiko haya yatakuwa yanaongozwa na nadharia Kihemenitiki ambayo ndiyo inayotumika katika uchambuzi wa data zinazokusanywa.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii imepitia maandiko mbalimbali yanayohusiana na fasihi simulizi katika utanzu wa nyimbo, hususan nyimbo za jadi. Aidha, vitabu, makala na tasnifu zilizoandikwa na watafiti wengine zimetumiwa. Pia nadharia ya kihemenitiki inayotumika katika uchambuzi wa data zilizokusanywa, itafafanuliwa katika sura hii. Lengo kuu la kufafanua utanzu wa fasihi simulizi, ni kutokana na kwamba mtafiti anashughulikia kipengele cha nyimbo ambacho ni kipera cha ushairi simulizi ndani ya fasihi simulizi. Hivyo maadiko haya yatakuwa yanapanua mawanda ya mtafiti katika kuijua fasihi simulizi kabla ya kuingia katika tatizo la utafiti ambalo ni athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga. Dhima ya kufanya mapitio ya maandiko imewekwa vizuri katika maneno ya Julius Caeser Enon (1998:41) yasemayo:

> The literature review is the systematic identification and analysis of documents containing information related to the study. The literature reviewed should point out how the problem of study is related to the previous research findings. It should demonstrate how the approach of the study is likely to differ from others. It should justify the need for the study, especially, if similar studies have been done before.
>
> Mapitio ya maandiko ni mpangilio maalum unaoainisha na kuchambua nyaraka zenye taarifa zinazohusiana na mada ya utafiti. Mapitio ya maandiko ni lazima yaoneshe namna tatizo la utafiti linavyohusiana na tafiti nyingine zilizowahi fanyika. Pia inalieleza namna tatizo hilo linavyotofautiana na matatizo mengine ya namna hiyo. Ni lazima kubainisha umuhimu wa tatizo iwapo kuna tafiti nyingine zilizowahi kufanyika (Tafsiri yetu)

Mwandishi anaeleza kwamba maandiko ni nyaraka zenye taarifa zinazohusiana na mada ya utafiti, halafu maandiko hayo inabidi yaonyeshe namna tatizo la utafiti linavyohusiana na tafiti nyingine zilizowahi kufanyika, na kueleza namna tatizo hilo lilivyotofautiana na

matatizo mengine. Hivyo, hii ndiyo sababu ya msingi inayomfanya mtafiti apitie maandiko ya fasihi simulizi kwa undani, ili aweze kukamilisha lengo lake la kuzichunguza athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* inayopatikana katika jamii ya Wachagga.

**2.2 Machapisho yanayohusiana na Fasihi Simulizi**

Kwa kuwa utafiti huu uliegemea zaidi katika fasihi simulizi, basi mtafiti amelazimika kulitalii eneo hili ili kuona kama kuna waandishi walioandika kuhusiana na mada iliyotafitiwa.

Sengo (1973:77) anasema kwamba fasihi simulizi hutumika kama mtumishi wa maisha ya watu/wanajamii. Inatumika kama chombo cha pekee cha kujenga umoja katika jamii husika. Pamoja na ufafanuzi wa mtaalam huyo kuhusiana na fasihi simulizi, kwa upande wa mtafiti anaona kuwa fasihi isipoeleweka vema inaweza kuwa ni chombo cha kuibomoa jamii, hasa pale ambapo fasihi inaelekeza lakini wachache wanapuuzia au wanatafsiri kinyume na maana yenyewe. Pamoja na hayo mtafiti anaona kuwa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zimetumika kama chombo cha kujenga umoja katika jamii ya Wachagga. Kwa hiyo, kufuatila maandiko ya mwandishi huyo yatamsaidia mtafiti kuona ni kwa jinsi gani nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zinasaidia kujenga umoja ndani ya jamii ya Wachagga. Aidha mwandishi hawezi kugusa jamii zote za kitanzania. Kwa hiyo mtafiti anatumia nafasi hiyo katika kuelezea athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa,* kupitia jamii ya Wachagga, kuonesha ni kwa namna gani nyimbo hizo zinatumika kama chombo cha pekee cha kujenga umoja katika jamii.

Kirumbi (1977:31) anasema kuwa fasihi simulizi ni masimulizi yanayopokelewa mdomo kwa mdomo, si masimulizi yaliyoandikwa tangu awali. Kwa maana hiyo, mtafiti anathibitisha kwamba fasihi simulizi ilitangulia kabla ya fasihi andishi. Baada ya kupitia maandiko ya mwandishi huyu hasemi masimulizi haya yalikuwa katika muundo gani, wala hajagusia suala la nyimbo kama kipera cha fasihi simulizi. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba nyimbo za Ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga hazijafanyiwa utafiti wa kutosha kuonyesha namna ambavyo zinaathiriwa kimuktadha kutokana na athari za kimaendeleo zilizojitokeza katika jamii hiyo ya Wachagga.

Songoyi (1997:30) anasema, fasihi simulizi wakati wote imekuwa ikitenganishwa na mafundisho ya fasihi kwa kudhani kwamba fasihi yenyewe ilianza kwa maandishi. Anaendelea kusema kwamba hilo ni kosa kubwa kwa sababu kama inavyofahamika, fasihi simulizi ilikuwepo tangu binadamu alivyoumbwa, aidha binadamu alitumia lugha katika kuimba nyimbo za kazi. Nyimbo hizi ziliimbwa kwa maneno. Kumbe kutokana na maelezo ya mwandishi huyu, ni uthibitisho tosha kabisa kwamba fasihi simulizi ni kongwe kuliko fasihi andishi, na hivyo inabidi ipewe kipau mbele, na kuthaminiwa kwa kuwa ndiyo inayoitambulisha jamii fulani. Aidha, kwa maneno mengine, fasihi simulizi itakuwa na mwisho wake pale dunia itakapokwisha na watu wote wakafa, na fasihi nayo itakufa. Kwa kuwa mtaalamu huyu anazungumzia binadamu kutumia lugha katika kuimba nyimbo za kazi, ni dhahri kuwa katika nyimbo za ngoma ya *Mbassa*, zitakuwepo nyimbo za kazi lakini zitakuwa zinazungumzia jamii ya Wachagga ambayo shughuli zake za kazi hazifanani na za jamii ya Wasukuma. Kwa hali hiyo mtafiti amepata mwanya wa kuzungumzia nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zinazohusiana na kazi katika jamii ya Wachagga.

Bakari (2011:51) katika Songoyi (1998) anasema kwamba Okpewho (1992:40) anazungumzia fasihi simulizi kama vile nyimbo, vitendawili na methali, imekuwa ikiangalia mitazamo iliyoko katika tamaduni za jamii, kuangalia mchango na matini katika kujua utamaduni na historia ya wanadamu. Jambo la pili lilikuwa kuangalia uhusiano kati ya utamaduni na matini iliyohusika. Okpewho aliona kuwa fasihi simulizi katika nyanja zote ni sehemu ya mila na utamaduni wa jamii. Anaendelea kusema kuwa masimulizi yanaweza kufanana kwa sababu binadamu kote ulimwenguni huwa na fikra na masimilizi yanayoashiria hatua ya kukua kwa utamaduni baina ya jamii hizo. Aidha kuhusu utendaji simulizi, Okpewho anaeleza kuwa utendaji hutofautiana kati ya vipengele vya kimazingira, umri, uwezo wa mtendaji, asili ya tukio, eneo la tukio pamoja na utumiaji muziki wa kikundi cha ngoma. Bila shaka kufuatana na mada inayotafitiwa ya athari za kimaendeelo katika mukthadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga, mambo aliyoyataja Okpewho yatajidhihirisha kutokana na hizo nyimbo za ngoma ya *Mbassa*. Kwa kuwa nyimbo hizi za ngoma ya *Mbassa* zinatazamwa athari zake kimuktadha kuhusiana na suala la mabadiliko ya kimaendeleo, bila shaka vipengele ambavyo vimetajwa na Okpewho kwamba vinaathiriwa, vivyo hivyo nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zitakuwa zimeathiriwa katika vipengele hivyo kwa sababu ya wakati. Kwa hiyo kuna kila sababu ya utafiti huu kufanyika ili kuweka bayana athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa.*

Mwakanjuki (2011) akimnukuu Mulokozi (2006:24-28) anatoa maana ya fasihi simulizi kuwa ni ile inayotungwa au kubuniwa na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo bila kutumia maandishi. Kwa hiyo fasihi simulizi ni tukio linalofungamana na muktadha (mazingira) fulani ya kijamii, na kutawaliwa na mambo kama vile fanani, hadhira, fani inayotendwa, tukio, mahali na wakati. Anaendelea kusema kuwa fasihi

simulizi hutungwa kichwani kabla ya ama wakati wa kutambwa. Kupita mwandishi huyu, kumemsaidia mtafiti kubaini namna ambavyo kunatokea athari kutokana na vipengele alivyovitaja, jambo ambalo linampa mwanya mtafiti katika kutazama athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga.

Aidha, katika maandiko yaliyopitiwa kuna wataalam wengine mbalimbali walioandika machapisho yanayofanana na kufafanua kuhusiana na suala zima la Fasihi ya jadi au fasihi simulizi. Miongoni mwa wataalam hao ni Finnegan (1970), Topan lo Lyongo (1972), Miruka (1994) aliyenukuliwa na Mulokozi (1996:33-34), Kirumbi (1977), Syimbo na Mazrui (1992), Msokile (1992, 1993), Mazigwa (1991), na Okpewho (1992).

## 2.3 Ufafanuzi kuhusiana na Maudhui

Baada ya kuwapitia wataalamu mbalimbali ambao wameandika kuhusiana na fasihi simulizi, mtafiti amewapitia waandshi wengine ambao wameandika kuhusiana na maudhui. Katika hali ya kawaida, maudhui katika kazi ya fasihi ni jambo ambalo linaongelewa kuhusiana na jamii kwa wakati huo, na uchaguzi wa jambo ambalo linatakiwa kushughulikiwa katika kazi hiyo ya fasihi.

Madumulla (2009:122) kwa kumrejelea Senkoro (1988) anasema, mchambuzi wa maudhui anaweza kuongozwa na maswali ya jumla kama vile:

Je, msanii anatueleza nini?

Je, msanii ameandika kazi yake akimlenga mtu wa tabaka gani?

Je, kuna utukuzaji?

Na kama upo anamtukuza nani na kwa nini?

Je, kuna ubezaji? anambeza nani na kwa nini?

Je, kuna matatizo yanayojitokeza?

Msanii anapendekeza njia ya kusuluhisha matatizo hayo?

Je, ni migogoro ipi ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni inayojitokeza?

Anaendelea kusema kwamba maswali hayo yanasaidia kujadili vipengele vingine vya maudhui kama vile dhamira, ujumbe, falsafa, mtazamo na msimamo. Mtafiti anakubaliana na mtaalamu huyo kwamba maswali hayo ndiyo yanayomwongoza mchambuzi wa maudhui, na katika swali lake la kwanza anasema, Je, msanii anatueleza nini? Swali hili, kwa namna moja au nyingine, linagusa mada ya mtafiti ambayo ni kuchunguza na kubainisha athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa*. Katika lengo la kwanza, mtafiti anachambua maudhui ya nyimbo alizokusanya. Kwa hiyo swali hilo litakuwa msaada kwa mtafiti katika kujibu swali la lengo la kwanza.

Senkoro (2011:1-4) anasema kuwa maudhui ni jambo liongelewalo pamoja na uchaguzi wa jambo la kulishughulikia katika kazi ya fasihi. Anaendelea kusema kwamba maudhui ya kazi za Fasihi hujumuisha mawazo na pengine mafunzo mbalimbali ambayo yamemsukuma mtunzi ama msanii kufikia huo uamuzi wa kutunga au kusana kazi fulani ya sanaa. Kutokana na maelezo ya mtaalam huyu, ndiyo maana mtafiti ameamua kufaya utafiti kuhusiana na athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga na kuona jinsi maudhui yaliyoko katika nyimbo hizo. Pia katika maudhui tutabaini mawazo na mafunzo yatolewayo na nyimbo za ngoma ya *Mbassa.*

## 2.4 Ufafanuzi kuhusiana na Nyimbo

Nyimbo ni dhana kuu inayohusishwa na mada ya utafiti, ambayo inajikita katika ngoma ya *Mbassa*, nyimbo hizo zikitazamwa namna gani zinavyoathiriwa kimuktadha kutokana na shughuli za kimaendeleo zinazofanywa na jamii hiyo ya Wachagga. Mtafiti amepitia

maandiko mbalimbali yanayohusiana na nyimbo na kuona kuwa waandishi wengi wameandika kuhusiana na nyimbo kwenye maeneo mengi lakini hawajaandika kuhusiana na athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa,* hususan jamii ya Wachagga. Nyimbo za *Mbassa* ni zile zilizokuwa zikiimbwa katika muktadha wa unyago kwenye jamii ya Wachagga. Nyimbo hizi zilikuwa zinaimbwa katika muktadha wa unyago, lakini katika matukio tofauti, likiwemo tukio la siku mtoto wa kike anapofanyiwa tohara na siku ya kutolewa mwali aliyefanyiwa tohara. Nyimbo hizi zilipokuwa zinaimbwa, kulikuwa na fanani, hadhira, na mahali maalum kuendana na tukio lenyewe. Kwa mfano, siku ya kutolewa mwali, nyimbo hizi ziliimbiwa aidha nyumbani kwa wazazi wa mtoto wa kike au nyumbani kwa bibi yake mzaa mama wa mtoto wa kike. Kwa kuwa mviga huo wa unyago haupo kwa sasa kutokana na jamii kuelimika kuhusiana na madhara yanayotokana na kukeketa watoto wa kike, nyimbo hizi leo hii, zinaimbwa katika miktadha mbalimbali ikiwemo miktadha ya sherehe za harusi, sherehe za kidini kama vile ubatizo wa watoto, kupata komunio ya kwanza na kipaimara. Pia zinaimbwa katika shughuli za kisiasa zikiwemo kampeni za uchaguzi mkuu wa serikali. Nyimbo hizi zinapoimbwa katika miktadha iliyotajwa hapo juu, zinaimbwa kwa lengo la kuburudisha na kuelimisha jamii pamoja na kusherehesha shughuli ya wakati huo. Yote haya ni kwa sababu dhima yake kama ilivyokuwa wakati huo imebadilika kutokana na kubadilika kwa hadhira inayoshiriki, mahali wimbo unapoimbiwa, fanani, na tukio lenyewe vyote hivi vimebadilika kufuatia mabadiliko ya kimaendeleo. Kwa mfano, nyimbo hizi zinapoimbwa kwenye muktadha wa harusi, dhima yake haiwi ile ile kwa sababu harusi hufanyikia katika kumbi kubwa za starehe, washiriki ni mchanganyiko wa watu mbalimbali kwa maana ya watu kutoka jamii zingine mbali ya Wachagga na kunakuwa na muziki zaidi ya nyimbo za *Mbassa*.

Finnegan (1970:272) anasema, fasihi simulizi ya Kiafrika inachunguza kazi za nyimbo na ushairi katika jamii. Akifafanua kuhusiana na nyimbo zinazozungumzia mambo ya siasa, anasema:

> It has been well said that Oral Poetry takes the place of news papers among non literate peoples. Songs can be used to report and comment affairs, for political pressure, for propaganda, and to reflect and mould public opinion. This political and topical fiction can be an aspect of many of the types of poetry
>
> Inasemekana wazi kwamba Mashairi Simulizi huchukua nafasi ya magazeti kwa watu wasiojua fasihi. Nyimbo zinaweza kutoa taarifa na maoni juu ya serikali, harakati za kisiasa katika kuakisi na kutoa maoni ya jamii. Siasa na matumizi yake unaweza kuwa mtazamo wa wengi wengi katika ushairi. (Tafsiri yetu)

Mtaalam huyu anazungumzia nyimbo kama kitu ambacho kinatumika kutoa taarifa na maoni juu ya masuala ya serikali kupitia propaganda za kisiasa, lakini bado hajaeleza propaganda hizi za kisiasa zinaathirije jamii husika. Hivyo utafiti huu utaweka bayana ni kwa namna gani shughuli za kimaendeleo zinavyochangia kuathiri nyimbo za ngoma ya *Mbassa* katika jamii ya Wachagga. Kwa hiyo mtafiti anaitazama jamii ya Wachagga ilivyokuwa inaishi na harakati zake za kimaendeleo katika maisha, kwa kuzingatia muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa.*

Ndungo (1991:56) anasema kwamba nyimbo za makabila mbalimbali hutolewa kwa njia ya kuendeleza mafundisho ya hekima malezi na busara za wahenga. Hayo huwa ni mafunzo ya maisha mema kwa mtu. Kwa hiyo kila kipindi huwa na maelekezo yake na nyimbo zake kama kuzaliwa kwa mtoto, mvulana kubalehe au msichana kuvunja ungo, kijana kuolewa au nyimbo za sherehe za arusi na mazishi. Mashairi na nyimbo hutolewa kulingana na majira au mazingira na hivyo mashairi hayo na nyimbo hizo huwa ni sehemu

ya utamaduni. Mwandishi huyu amegusia nyimbo zinazotolewa na makabila mbalimbali kwamba zinaendeleza mafundisho ya hekima, malezi na busara za wahenga. Pia ametaja nyimbo za kuzaliwa watoto, nyimbo za kuimbiwa wavulana au wasichana wanapofikia hatua ya kubalehe au kuvunja ungo, nyimbo za sherehe za harusi na mazishi. Katika nyimbo alizozitaja mtaalam huyu, kuna uwezekano mkubwa kabisa wa miktadha hiyo kujitokeza katika nyimbo za ngoma ya *Mbassa*, lakini kwa vyovyote zitatofautiana kutakana na hadhira, mandhari, fanani na tukio lenyewe. Kwa nsingi huo kuna kila sababu ya kufanyika kwa utafiti wa athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ili kuziweka bayana athari hizo za kimaendeleo ambazo zinajitokeza katika jamii ya Wachagga.

Ndulute (1997) ameandika kuhusiana na nafasi ya nyimbo katika fasihi ya Kihehe. Mwandishi amechambua mambo matatu katika nyimbo za Kihehe, kwanza ameangalia fani katika vitendawili na nahau zilizomo kwenye jamii ya Wahehe, pili alitazama nafasi ya nyimbo hizo katika jamii ya Wahehe, zikiwemo nyimbo zilizokuwa na mwelekeo wa kihistoria katika siasa na utamaduni. Kwa mfano, anamwelezea kijana wa Kihehe kwamba anatakiwa kuhakikisha kwamba maisha yanakuwa endelevu kwa kufanya kazi kwa bidii. Tatu aliangalia utendaji katika nyimbo za jamii ya Wahehe kuhusiana na hadhira iliyohusika. Mwandishi huyu ameangalia nafasi ya nyimbo katika fasihi simulizi ya Kihehe katika miaka ya sabini, jambo ambalo fasihi simulizi huwa inabadilika kuendana na muktadha, umri, asili ya tukio, eneo la tukio pamoja na hadhira inayotenda tukio hilo. Kwa kuwa mwandishi anazungumzia kuhusiana na nafasi ya nyimbo katika fasihi ya Kihehe, bila shaka maudhui yanaweza kutofautiana kutokana utofauti wa jamii, hata katika muktadha kutakuwa na tofauti ya fanani, hadhira, tukio, mahali na wakati.

Hivyo mtafiti anataka kuziba mwanya huo kwa kutazama athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga.

Massawe (1995:8-9) ameshughulikia nyimbo za Kichagga zinazohusiana na sherehe za harusi. Anasema kwamba katika kundi la Wamachame ambao wako katika jamii ya Wachagga, wanaume walionekana kuwatawala sana wake zao kiasi kwamba waliweza kuimbiwa nyimbo zilizohusiana na kudharauliwa kwao. Mwandishi huyu kupitia nyimbo hizo za harusi anaelezea ubabe wanaokuwa nao wanaume wa Kichagga, hususan jamii ya Wamachame ambao huwadharau wake zao kwa kuwaita wapumbavu, na wasiojua kitu chochote. Nyimbo hizi zilidhihirisha unyanyasaji na udhalilishaji wa wanawake. Pamoja na kwamba mwandishi amezikusanya nyimbo kutoka jamii ya Wachagga wa Machame, yeye alizitazama nyimbo za harusi. Lakini utafiti huu unahusu jamii ya Wachagga Wakibosho, katika nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ukichunguza athari za kimaendeleo katika nyimbo hizo. Mtafiti anazitazama nyimbo za ngoma kimuktadha kwamba ni kwa namna gani zimeathiriwa na shughuli za kimaendeleo, ikizingatiwa kuwa nyimbo hizi zilikuwa zikiimbwa katika mviga wa unyago. Kwa kawaida, jamii hubadilika kila baada kipindi fulani. Ni kipindi kirefu tangu Massawe alipozishughulikia nyimbo za harusi hadi sasa, hivyo katika jamii ya Wachagga kumekuwako na mabadiliko makubwa ya kimaendeleo kama vile kupanuka kwa kiwango cha elimu, jamii ya wachagga walau kiwango cha elimu cha watoto wao, walio wengi ni kidato cha nne. Aidha kumekuwa na suala la mabadiliko katika sayansi na teknolojia, kama vile Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), biashara huria katika jamii na mwingiliano wa kuoana katika jamii ya Wachagga. Kutokana na mabadiliko hayo, ndiyo maana mtafiti amechukua jukumu la kufanya utafiti huu ili kuweza kuzibainisha athari hizo na namna zilivyoweza

kuathiri nyimbo za ngoma ya *Mbassa* inayopatikana katika jamii ya Wachagga hususani Wakibosho.

Mulokozi (1996:66) akimnukuu Athumani (1992) ameandika nyimbo zinazohusiana na maombolezi. Kwa mfano katika wimbo wake huu:

Wacha kulia washaki, na kilio kisizidi
Hayo mauti ni haki, ni njia isiyo budi
Ya-sana-llah-izaki, shukuru Binti Saidi
Nyamara kulia, ndiyo kilimwengu
Kaa utulie, ushukuru Mungu
Ooo nalia nalia, naona uchungu
Kwa kuondokewa na wazazi wangu
Nimekuja kukuhani, mpenzi wangu nyamaza
Nimekuja kukuhani, muhibu wangu nyamaza
Naona u mswibani, ukilia waniliza
Naona u mswibani, ukilia waniliza
Shukuru mpenzi wangu, cheka na kuzungumza
Nyamaza kulia, ndiyo kilimwengu.

Mwandishi anamwelezea mwimbaji anayemliwaza mfiwa ambaye amefiwa na ndugu yake. Wimbo huu unaonyesha mahusiana yaliyokuwepo kati ya mwimbaji na marehemu. Wakati mwingine mwimbaji anatoa sifa za marehemu, na hata kuonesha hasara ambayo watapata wafiwa na wale waliobaki kwa sababu ya kuondokewa na marehemu. Mfiwa anakumbushwa kwamba ipo siku na yeye atalala kama huyo ndugu yake, hivyo ni lazima kujiandaa kwa sababu kufa ni lazima kwa kila binadamu. Katika nyimbo za mwandishi huyu anazungumzia uwanja wa nyimbo za maombolezi katika muktadha wa mazishi, muktadha huu kwa vyovyote utatofautiana na wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa*, ukizingatia kwamba mandhari, fanani, hadhira na wakati wa kutendeka tendo hilo kutakuwa na utofauti. Kwa hiyo ndiyo maana mtafiti ameamua kufanya utafiti kuhusiana

na athari za kimaendelo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga.

Mulokozi (1996:63-74), anfafanua kwa kina kuhusiana na nyimbo. Mtaalam huyu anaziweka nyimbo katika kumbo mbili ambazo ni Ushairi-Simulizi na Ngomezi. Kuhusu Ushairi-Simulizi anasema kwamba ni tungo za kinudhumu zinazofuata kanuni fulani za urari wa sauti, mapigo ya lugha na mpangilio wa vipashio vya lugha. Anaendelea kusema kwamba lugha ya ushairi katika fasihi simulizi hupambanuliwa na lugha ya kawaida kwa namna inavyopangiliwa na inavyoingiliana na muktadha wa utendaji. Hivyo wimbo ni kila kinachoimbwa, dhana hii ikijumuisha tanzu nyingi zikiwemo tanzu za kinathari kama vile hadithi. Mtaalam huyu anagawa nyimbo katika makundi manne ambayo ni nyimbo zinazohusiana na tumbuizo, nyimbo zinazotukuza, nyimbo za kuchapua na nyimbo za tendi. Anaaendelea kusema kwamba nyimbo hizo zinapoimbwa zinaonekana kama zinaburudisha lakini zinakuwa na athari kubwa katika jamii. Katika nyimbo nyingi alizozitaja mtaalam huyu, ni wazi kwamba zitatoa mwanga wa kusaidia kubainisha athari za kimaendeleo zinazosababishwa na nyimbo za ngoma ya *Mbassa*. Kwa kuwa athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* hazijafafanuliwa na nyimbo za mtaalam huyu, ni wazi kwamba kuna kila sababu ya kufanya utafiti huu kwa msingi wa kuzibainisha athari za kimaendeleo katika nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1998:161) inasema:

> Nyimbo ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodia, mkong'osio, mapigo, mwendo na muwala. Nyimbo huweza kuimbwa pamoja na kucheza muziki wa kipekee. Huweza kuimbwa na mtu mmoja pekee au na wafuasi wake wakiitikia mkarara. Zipo nyimbo za aina

> mbalimbali kwa mfano, tumbuizo, bembea, taulili, nyimbo za ngoma, nyimbo za miviga, nyimbo za michezo, nyimbo za kawaida n.k. nyimbo hizi huchukua majina tofauti kufuatana na jamii.

Katika maelezo ya Taasisi hiyo, inataja aina mbalimbali za nyimbo, zikiwemo nyimbo za ngoma. Ingawaje mwandishi huyo hajataja ni nyimbo za ngoma gani anayoizungumzia, maandishi yake yanamsaidia mtafiti katika kujua kwamba sampuli alizozichagua wakiwemo manju, zinalenga kumsaidia katika utafiti wake. Kwa kuwa jamii nyingi hutofautiana katika mila na desturi, hakuna shaka kwamba nyimbo za ngoma ya *Mbassa*, nazo haziwezi kufanana na nyimbo alizozitaja mwandishi. Pamoja na aina zote zilizotajwa na taasisi hiyo bado suala la msingi ni kwamba mtafiti anazitazama nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zinavyoathiriwa kimuktadha kutokana na shughuli za kimaendeleo. Hii ni dhahiri kuwa jamii ya Wachagga inayohusishwa na tatizo la utafiti kuhusiana na nyimbo zake za ngoma ya *Mbassa*, bado kunahitajika kufanyika utafiti zaidi ili kuweza kubaini ni kwa namna gani maendeleo yalivyochangia kuathiri nyimbo za ngoma ya Mbassa, hususan katika suala la muktadha. Pia maendeleo ambayo yamo ndani ya jamii ya Wachagga, ni kwa namna gani yanashadidia na kusawiri nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zinazoimbwa kipindi hiki.

Nyoni (1998) ameandika kuhusiana na mabadiliko ya sanaa vijijini kwenye muziki wa ngoma ya Lindeku katika jamii ya Wamatengo, Tanzania. Kwa mfano, baadhi ya nyimbo alizozikusanya, ametumia neno hudi iliyokuwa inatembezwa sokoni, akimaanisha karatasi inayowakilisha thamani ya fedha, lakini maana yake katika wimbo huo ilikuwa na maana nyingine ambayo ni sehemu ya siri ya mwanamke. Akiwa anahusianisha wimbo huo na jamii ya Wamatengo kuwa ilikuwa ni kitendo cha aibu kwa mwanamke kufanya mahusiano ya mapenzi, bila kuwa na ndoa halali. Ni dhahiri kwamba nyimbo za ngoma ya Lindeku, dhima yake kimuktadha itatofautiana na nyimbo za ngoma ya *Mbassa*. Ni

dhahiri kuwa athari za kimaendeleo zitakazosababishwa na nyimbo za ngoma ya Lindeku katika jamii ya Wamatengo zitatofautiana na za nyimbo za ngoma ya *Mbassa*. Kutokana na msingi huo, kuna kila sababu ya kufanya utafiti huu wa athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga.

Mmbando (2004:10-18) ameandika kuhusiana na nafasi ya nyimbo za kijamii za harusi katika kabila la Wachagga. Mwandishi huyu amekusanya nyimbo za harusi na kuelezea namna zinavyotoa mafunzo ya ndani kwa kijana anayeoa. Anaeleza kuwa mafunzo hayo yalimwelekeza kijana wa Kichagga namna ya maisha mazuri ya kuishi na mkewe. Katika nyimbo zake amebainisha maudhui yaliyoko katika hizo nyimbo, kwa mfano katika wimbo wake wa:

| **INU NYI INU** | **LEO NI LEO** |
|---|---|
| *Inu nyi inu* | Leo ni leo |
| *Inu nyi inu* | Leo ni leo |
| *Inu nyi inu, ko Mariki kuore sia* | Leo ni leo kwa Mariki kuna matumaini |
| *Koicho tiro, tiro, tiro* | Ukisikia ndi, ndi, ndi |
| *Koicho tiro, tiro, tiro* | Ukisikia ndi, ndi, ndi |
| *Koicho tiro, tiro, tiro,* | Ukisikia ndi, ndi, ndi |
| *ko Mariki kuore msoro* | Kwa Mariki kuna kijana |
| *Kinate kinanguruma,* | jaa inauma |
| *hoya, hoya,* | Haya, haya |
| *Kinate kinanguruma,* | Njaa inauma |
| *hoya, hoya* | Haya, haya |
| *Kinate kinanguruma* | Njaa inauma |

**Chanzo: Mmbando (2004:15-16)**

Mwandishi anasema kwamba wimbo huu unaimbwa siku ya arusi baada ya kufungwa kanisani, upande wa wazazi wa mtoto wa kiume wamnawaimba upande wa wazazi wa mtoto wa kike, kwa kuwapa ujumbe kuwa wana mtoto wa kiume mwenye uwezo na nguvu nyingi. Hasa anaposema:

*Koicho tiro, tiro, tiro* Ukisikia ndi, ndi, ndi
*Koicho tiro, tiro, tiro* Ukisikia ndi, ndi, ndi
*Koicho tiro, tiro, tiro* Ukisikia ndi ndi ndi
*Ko Mariki kuore msoro* kwa Mariki kuna kijana

Hapa mwandishi anazungumzia jamii ya Wachagga kuwa hawategemei kijana aliyeoa ashindwe kupata watoto, hivyo wazazi wa mtoto wa kiume wanawapa ujumbe upande wa wazazi wa mtoto wa kike kwamba mtoto wao ana kishindo cha kutosha, yaani uwezo wa kuzaa watoto na kuwalea. Mwandishi huyu anazungumzia nyimbo za harusi zinazoimbwa katika muktadha wa kanisani. Harusi za kipindi hicho baada ya kufungwa kanisani, sherehe zilikuwa zinafanyikia kijijini ambako kulikuwa hakuna kumbi za starehe, miundombinu ilikuwa duni na kipato cha jamii kilikuwa kidogo. Kutokana na mabadiliko ya kimaendeleo, harusi za siku hizi zinafanyikia mjini zikiwa zinasindikizwa na maandamano makubwa ya magari yakiandamana na bendi za muziki na kuchukuliwa kwa picha za mgando na jongea. Pia kumekuwa na utoaji wa michango mikubwa ya zawadi. Isitoshe, kumekuwa na mwingiliano katika kuoa na kuolewa, Mchagga anaweza kuoa toka kabila jingine, na vivyo hivyo mtoto wa kike anaweza kuolewa na kabila jingine, tofauti na kipindi cha nyuma, jamii ya Wachagga walikuwa wanaoana wao kwa wao. Aidha, kwa kuzingatia mabadiliko hayo ya kimaendeleo, ndiyo maana mtafiti amechukua uamuzi wa kufanya utafiti ili kuona ni kwa namna gani nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zinavyoathiriwa kutokana na shughuli za kimaendeleo.

Songoyi (2005:139-140) alitafiti kuhusu ngoma ya *Wigashe* ya Wasukuma akiwa anachunguza muktadha wa maana, maudhui na muktadha wa utendaji, anasema kuwa *Wigashe* ni ngoma maarufu sana katika kabila la Wasukuma. *Wigashe* inahusu imani za utumiaji wa dawa katika shughuli zozote zinazofanywa na jamii ya Wasukuma inayopatika katika Mkoa wa Shinyanga. Pamoja na mwandishi kuzungumzia maana na maudhui katika muktadha wa utendaji, ni wazi kwamba fasihi simulizi hutofautiana

kutoka jamii moja na nyingine katika vipengele hivyo. Kwa hiyo nyimbo za ngoma ya *Mbassa* fanani wake watatofautiana na fanani wa ngoma ya *Wigashe*, hata mandhari, hadhira tukio pia wakati kutakuwa kuna kutofautiana. Kwa hivyo utafiti wa kuchunguza athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga inabidi ufanyike ikizingatiwa kuwa katika fasihi simulizi kila jamii ina fasihi yake na ambayo huwasilishwa kwa njia mbalimbali ikiwemo hadithi, nudhumu (ushairi) na misemo. Hii ndiyo sababu ya mtafiti kutaka kutafiti mada ya athari za kimaendeleo katika nuktadha wa Nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii yaWachagga.

Mpangala (2006:19) amefanya utafiti kwenye nyimbo za jamii ya Wamanda kuhusiana na zinavyoelimisha jamii. Mtafiti huyu ameshughulikia nyimbo za Mganda na Kioda za jamii ya Wamanda. Katika nyimbo alizokusanya anaeleza namna zilivyokuwa zinatoa mafunzo na maonyo kwa wanaume walioziacha au kuzitelekeza familiya zao na kuoa wanawake wengine. Mtafiti huyu anazungumzia jamii ya Wamanda, na pia anazungumzia nyimbo zinazohusiana na utoaji wa elimu kwa kutumia nyimbo za Mganda na Kioda. Katika mantiki ya utafiti huu wa athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga, mtafiti wa nyimbo za Mganda na Kioda, haonyeshi kama nyimbo hizo zimeathiriwa na shughuli za kimaendeleo na je, nyimbo hizo za Mganda na Kioda zinaendana na mabadiliko yanayotokea katika jamii? Pia kuna uwezekano mkubwa wa kutofautiana katika miktadha inayoimbwa nyimbo hizo. Kwa hiyo kuna kila sababu ya utafiti huu kufanyika ili kuziweka wazi athari za kimaendeleo, na namna zinavyoathiri nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga.

Leonard (2006:34), amefanya utafiti kuhusiana na athari ya utandawazi katika mchango wa kazi kwenye nyimbo za watoto wa Kipare. Moja kati ya nyimbo alizokusaya ni huu hapa:

| **SHINJIA MWANA** | **LALA MTOTO** |
|---|---|
| *Shinjia mwana shinjia mwana* | Lala mtoto lala mtoto |
| *Ndeghe vothe vevecha, Tehena* | Ndege wote wanapita hakuna |
| *Ee mdori, ushinjie mwana* | Wewe mdogo lala mtoto |
| *Kakicha ni ndhaa mghoje* | Kama ni njaa mngoje |
| *Vaveo ambu ni nethi* | Baba kwani ni nesi |
| *Hetie kindu, Kari naye ethina* | Alete kitu wakati yeye hana |
| *Kindu enekwinka mawa, ambu* | Kitu atakupa pombe, kwani |
| *Etongie he mawa,* | Ameenda kwenye pombe |
| *Shinjia Mwana x2* | Lala mtoto x2 |

**Chanzo: Goodness (2006:34)**

Wimbo huu unatoka kwenye jamii ya Wapare ambao unaeleza namna mama anavyombembeleza mwanaye alale. Anamwambia mtoto lala, lala kwa sababu ndege wote wamelala, si ndege wadogo hata wakubwa wote wamelala. Anamwambia mwanaye kwamba kama anasikia njaa amsubiri baba yake arudi kwa sababu yeye hana cha kumpa halafu anaendelea kumwambia mwanaye kwamba kama baba yake hataleta chakula, atakuja kumpa pombe kwa sababu yeye ni mnywaji. Katika maelezo ya huyu mama inaonesha kwamba analalamika kutokana na unywaji wa mume wake. Haitoshi tu, inaonesha kuwa mwanaume hanunui chakula nyumbani. Pamoja na kwamba wimbo huu ni wa kumbembeleza mtoto, bado una ujumbe kuonesha madhara yanayotokana na ulevi, au unywaji wa pombe kupita kiasi, kwamba familiya haiwezi kupata mahitaji muhimu ikiwemo elimu, matibabu, malazi na chakula. Mwandishi anazungumzia namna Nyimbo za Kipare za watoto zinavyoathiri maendeleo. Kwa kuwa jamii moja hutofautiana na jamii nyingine, ni wazi kwamba athari zitakazojitokeza kwa watoto wa jamii ya Kichagga zitatofautiana na zille za jamii ya Kipare, pia nyimbo zinazoimbwa kwenye ngoma ya

*Mbassa*, kimuktadha zitatofautiana kutokana na hadhira, mandhari, fanani, na hata tukio linalotendeka kwa wakati huo. Kwa hiyo, utafiti huu ni muhimu ufanyike ili kuweza kuziba pengo hilo la athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga. Waandishi wengine walioandika kuhusiana na nyimbo za watoto ni Abiduna (2006) na Mdoe (2011). Waandishi hawa nao wameandika nyimbo zinazohusiana na watoto, ambazo nazo haziwezi kuwa na athari zinazofanana na zile zinazojitokeza katika nyimbo za ngoma ya *Mbassa*, hivyo huu ni ushahidi tosha kwamba utafiti kuhusiana na athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* bado haujafanyika.

John (2006:29: ameandika kuhusiana na nyimbo za jando la wavulana wa Kiyao zilikuwa na matokeo gani katika jamii, akifanyia utafiti wake katika kijiji cha Chikundu wilaya ya Masasi. Mtafiti huyu anazungumzia kwamba katika jamii ya Wayao wazee ni chumvi, hivyo kwa sehemu kubwa wanathaminiwa sana. Mara kunapotokea maovu au kutoelewana katika jamii, wazee hushughulikia jambo hilo mara moja. Kipindi cha jando ambacho wanakiita *Dagala* vijana wanafundishwa kuheshimu wakubwa na kuwasaidia katika matatizo. Mtafiti anaenda mbali zaidi kwa kuzungumzia kwamba vijana wadogo ndio wanaofanya uharibifu. Pamoja na kwamba mwandishi huyu amegusia maudhui na athari zinazotokana na nyimbo hizo katika muktadha wa jando kwenye jamii ya Wayao, ni wazi kwamba maudhui ya nyimbo za jando kwenye jamii ya Wayao, yatatofautiana na maudhui nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga ambazo zinaimbwa katika muktadha wa unyago. Kwa hiyo mada hii ya athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ni lazima ifanyiwe utafiti ili kuweza kubaini mabadiliko hayo yalivyoathiri nyimbo za ngoma ya *Mbassa*.

Mwakanjuki (2011) amaendika kuhusiana na athari za mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa nyimbo za Kapote za mwimbaji Mwandwanga, katika jamii ya Wanyakyusa. Mwandishi ameangalia jinsi mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa yanavyoathiriwa na fani, maudhui na dhima ya nyimbo za kapote katika jamii ya Wanyakyusa kwa kipindi cha 2000 hadi 2010. Utaafiti wetu unachunguza athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga. Mbali ya hivyo, watafiti hawamtazami msanii mmoja tu, bali wanawachunguza waimbaji mbalimbali wakiwemo rika la wazee wanaume kwa wanawake na vijana wasichana kwa wavulana, jambo ambalo kwa Mwakanjuki amezitizama nyimbo za Kapote za mwimbaji Mwandwanga. Aidha, kutokana na kutofautiana kwa mada, kabila linalofanyiwa utafiti, idadi ya wasanii na dhana zinazotumiwa katika utafiti ni tofauti, kuna kila sababu ya kufanyika kwa utafiti huu ili kuweza kuthibitisha ni kwa namna gani nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zilivyoathiriwa kutokana na mabadiliko ya kimaendeleo.

## 2.5 Ufafanuzi Kuhusiana na Jamii ya Wachagga

Mtafiti anaifafanua na kuiielezea jamii ya Wachagga katika historia, mfumo wa utawala, utamaduni katika mila na desturi, lugha, mafunzo ya jando na unyago, dini na uchumi katika jamii hiyo. Lengo la mtafiti katika kuielezea jamii hiyo kwa undani ni ili kuiweka bayana jamii ya Wachagga, na kuondoa maswali ambayo yangeliweza kuulizwa wakati mada ya utafiti inaposhughulikiwa katika kuiwasilisha, kuichambua na kutoa matokeo ya utafiti.

### 2.5.1 Historia na Maisha ya Jaamii ya Wachagga

Jamii ya Wachagga ni miongoni mwa jamii mbili zinazoishi katika mkoa wa Kilimanjaro, jamii hizo ni Wachagga na Wapare. Wachagga wanaishi Kusini-Kaskazini chini ya Mlima Kilimanjaro, mlima mrefu kuliko yote barani Afrika, ambao una urefu wa mita 5,895 toka


usawa wa bahari. Mlima Kilimanjaro una uoto wa asili ambao hutofautiana kadri unapoelekea uwanda wa chini. Mkoa wa Kilimanjaro una wilaya sita, nne kati ya hizo zinakaliwa na jamii ya Wachagga. wilaya hizo ni Moshi Vijijini, Moshi Mjini, Rombo na Hai. Wilaya mbili zilizobakia zinakaliwa na jamii ya Wapare, ambazo ni Same na Mwanga.

**KIELELEZO: MLIMA KILIMANJARO**



**Chanzo: Mtafiti (2013)**

**KIELELEZO: RAMANI YA MKOA WA KILIMANJARO NA WILYA ZAKE**




**Ufunguo: ________**Mipaka ya wilaya

**Chanzo:** htt//sw.wikipedia.org/wiki/mkoa wa kilimanjaro

### 2.5.2 Utamaduni wa Jamii ya Wachagga

Jamii ya Wachagga ilikuwa na mfumo wake uliohusiana na lugha, mila na desturi na dini. Kueleweka kwa nyanja hizi kumemsaidia mtafiti katika kuichambua mada ya utafiti amabayo inazungumzia athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga.

### 2.5.3 Mila na Desturi za Jamii ya Wachagga

Jamii ya Wachagga ina mila na desturi ambazo husimamiwa na rika la wazee, waume kwa wake. Baadhi ya mila na desturi hizo zinahusu mavazi, chakula, malazi, miiko, salamu na matambiko. Mavazi waliyokuwa wanatumia kwa kipindi cha kabla ya ujio wa wageni

yalikuwa magome ya miti na ngozi za wanyama. Jamii ya Wachagga ina vyakula vingi sana vya asili, vinavyotokana na mazao wanayolima na kufuga. Baadhi ya vyakula hivyo hupewa majina kutokana na kundi husika. Kwa mfano: Jamii ya Wakibosho wana vyakula kama vile ***Kibulu*** ambacho ni mchanganyiko wa ndizi na maharage, ***Mtori*** mchanganyiko wa ndizi na nyama ambao hupondwapondwa na kutiwa maji au mchuzi uliochemshia nyama. ***Kitalolo*** ni mchanganyiko wa ndizi, mahindi na mboga za majani, hususan mboga za maboga na mahindi yaliyokobolewa hupondwapondwa pamoja na kutiwa maziwa ya mgando, ***Kisusiyo*** chakula hiki ni mchanganyiko wa damu ya mbuzi, kondoo au ng'ombe na mchuzi wa moto wa nyama ambao humiminwa kwenye damu mbichi na kunywewa wakati huo huo ikiwa bado ya moto. Hivyo ni baadhi tu lakini viko vyakula vingi sana. Kuna vyakula vinavyokuwa maalum kwa akina mama waliojifungua watoto, vijana waliofanyiwa tohara, mwali aliyeolewa kwa siku za mwanzo. Mfano wa vyakula hivyo ni kama vile **mtori, kisusiyo, usawo** na ***muso***. ***Muso*** kwa jina lingine ni uji wa ulezi ambao umekobolewa na kusagwa mashineni au kwa kutumia jiwe maalum la kusagia, ambao unga wake huchanganywa na maji na kuchemshwa na baadaye ukishaiva hutiwa maziwa ya mgando na mhusika huwekewa katika chombo cha kunywea kijulikanacho kama ***Kitela***, chombo hiki kiko katika mfano wa bakuli lakini huwa na mishikio miwili.

Kuhusiana na nyumba, jamii ya Wachagga walijenga nyumba zilizojulikana kama msonge kutokana na umbo lake. Nyumba hizi zilijengewa miti na kuezekwa kwa majani makavu ya migomba ambayo kwa jina la kilugha hujulikana kama ***madawa***. Huezekwa kuanzia chini hadi juu kwa hayo majani (***madawa***). Nyumba hizi kwa jamii ya Wachagga waliziita ***fulusuti***[1] Nyumba hii kwa ndani ni kubwa sana ambayo ilweza kutosheleza familia ya watu watano hadi sita, ng'ombe zaidi ya wawili na mbuzi zaidi ya wanne. Ndani ya

---

[1] Limetokana na neno la kiingereza full suit

nyumba hii kuliweza kutengwa chumba cha wageni, chumba cha watoto, chumba cha mama, eneo la jiko, eneo la mbuzi eneo la ng'ombe na eneo la kupumzikia.

Katika salaam, jamii ya Wachagga walisisitiza sana kwa watoto wao kuhakikisha wanawasalimia wale wote waliowazidi umri kwa jinsia zote. Hivyo watoto waliwajibika kwa jamii yote, mtoto aliweza kuadhibiwa na mtu yeyote bila kujali kama ni mwanaye au la, ikiwa amepita bila kusalimia. Kwa watoto wa kike anaposalimia kwa kushikana mikono ni lazima akunje goti kidogo.

Kwa upande wa matambiko na miiko, jamii ya Wachagga ina matambiko yake. Baadhi yakiwa matambiko kwa watoto wachanga waliozaliwa, alichijwa mnyama kondoo na mtoto kuvishwa kipande cha ngozi katika mkono wake wa kushoto na wazazi wao walivishwa kipande cha ngozi kidole cha kati mkono wa kushoto. Matambiko kwa vijana waliofanyiwa tohara na matambiko ya mvua. Katika matambiko hayo yaliambatana na nyimbo. Pia kulikuwa na miiko, kwa mfano akina mama wajawazito walikuwa hawaruhusiwi kula mayai na maini, imani yake ni kwamba mtoto atazaliwa hana nywele, wanawake walikuwa hawaruhusiwi kufika eneo wanalochinjia wanaume, ilikuwa ni mwiko kuvuka daraja kwa kupishana. Katika matambiko, kwa mfano vijana waliofanyiwa tohara waliimbiwa nyimbo zilizowapa mafundisho, na wakati huo huo zilikuwa zinaburudisha

### 2.5.4 Mafunzo ya Jando na Unyago

Mafunzo haya ya jando na unyago yalifanyika kwa watoto wa kike na kiume waliobalehe. Namna tendo hili lilivyokuwa linafanyika ni kwamba watoto wa kike na kiume, kila kundi na kwa kila kijana alikuwa na msimamizi wake ambaye alijulikana kwa jina la ***Mwiichi***.

Huyu msimamizi ndiye aliyekuwa anampeleka mtoto huyu wa kike au wa kiume kwa yule ngariba. Kwa upande wa watoto wa kike walipokuwa wanafanyiwa tendo hilo la tohara, kulikuwa na akina mama maalum (ngariba) ambao waliwafanyia tohara. Ngariba alikuwa na uwezo wa kuwafanyia tohara watoto wa kike kuanzia mmoja hadi sita kwa siku. Zoezi hilo la kufanyiwa tohara lilikuwa likifanyika asubuhi sana kuanzia majira ya saa kumi alfajiri na lilipokuwa linaendelea, kulikuwa na nyimbo ambazo zilikuwa zinaimbwa ili kumfanya huyo kijana anayefanyiwa tohara asiwe na wasiwasi pia kwa wale ambao wako jirani na eneo la tohara wasijue kinachoendelea. Kwa watoto wa kiume na wao walikuwa na mwanaume maalum wa kuwatahiri. Mara walipokwisha tahiriwa walirudishwa makwao ambako huko walikuwa wamejengewa vibanda vya nyasi ambavyo vilikuwa mbali kidogo na makazi ya hapo nyumbani. Kwenye vibanda hivyo waliishi na wasimamizi wao ambaao waliwapa mafunzo kwa muda wa kipindi cha mwezi mmoja. Kuhusiana na suala la chakula, vyakula vilipikwa na akina mama na kuvipeleka huko kwenye vibanda hivyo, lakina kabla hawajakaribia hilo eneo walikwa wanaimba wimbo ambao wale wasimamizi hutambua kwamba ni chakula kilikuwa kinaletwa, na wao huwa wanaujibu wimbo huo huku wakiwa wanakifuata chakula hicho. Siku moja kabla ya kurudishwa nyumbani, vijana hao walipelekwa porini wakiwa na silaha mbalimbali kama vile mkuki, panga, manati au upinde na mishale kwa ajili ya kuwinda ndege au mnyama yoyote na kurudi naye kwenye kibanda chake. Siku iliyofuata vijana hao waliachiliwa huru na kuruhusiwa kutembelea rafiki zao.

Kwa vijana wa kike baada ya wao kufanyiwa tendo hilo la tohara walirudishwa nyumbani, lakini wao walitengwa na wana familia wengine kwa kuwaweka maeneo maalum katika nyumba ya asili ambapo mawasiliano yalikuwa wao na wasimamizi wao tu. Nao walikaa kwa muda wa mwezi mmoja, baada ya huo mwezi mmoja, ilitengezwa pombe ya kienyeji

**(**Mbege) na kuchezwa ngoma ya *Mbassa.* Uchezaji wa ngoma hii ya *Mbassa* huanza kuchezwa majira ya saa tisa alasiri, ngoma hii inachezewa aidha, nyumbani kwa wazazi wa mtoto aliyefanyiwa tohara, au nyumbani kwa bibi yake mzaa mama wa mtoto aliyefanyiwa tohara. Wachezaji huwa katika duara huku wakishikana mabegani na mtoto wa kike aliyefanyiwa tohara na msimamizi wake huwa katikati ya huo mduara wakati huo kunakuwa na kiongozi anayeanzisha wimbo, huku wote wakipokea na kuimba kwa pamoja. Mtoto huyo wa kike aliyefanyiwa tohara huwa amevalia vazi aina shimizi, shimizi ni aina ya gauni ambayo imeshonwa kwa kutumia kitambaa cheupe. Shingoni anakuwa amevalia shanga na njuga miguuni kichwa chake kikiwa kimenyolewa upara. Wakati wakiwa wanaimba na huku wameshikana mabegani, huwa wanainama kidogo na kusimama huku wakiendelea kuzunguka katika mduara walioutengeneza. Ngoma hii ilkuwa inachezwa siku ile aliyofanyiwa tohara huyo mtoto wa kike na siku ya mwisho ya kutolewa ndani. Zile siku thelathini alizokaa ndani, alikuwa anapewa mafunzo yaliyohusiana na kumlea mume, watoto, kuheshimu wakubwa na wadogo, miiko mbalimbali, kufanya kazi na namna ya kuishi katika jamii.

### 2.5.5 Dini katika Jamii ya Wachagga

Jamii ya Wachagga ilkuwa na dini zake za asili, wamezitumia dini hizo katika suala la imani ambayo iliwaongoza katika kuabudu, wengine wakiwa wanaabudu chini ya mti, chini ya mgomba na wengine nje ya nyumba zao. Walioabudu chini ya mti walitumia mti unaoitwa ***Isale***, wale walioomba chini ya mgomba, baadhi walitumia aina ya migomba ilinaojulikana kwa jina la ***Ilali*** au ***Inanambo***. Maombi haya yalihusishwa na mungu wao waliyemwita ***Ruwa***. Ruwa kwa maana ya Kichagga ilikuwa inamaanisha Mungu au Jua. Baada ya ujio wa wageni, imani hizo zilipungua kwa kuwa jamii ilianza kufuata dini ya Kikristo au ya Kiislamu.

### 2.5.6 Uchumi wa Jamii ya Wachagga

Jamii ya Wachagga hujishughulisha na shughuli za kilimo na biashara. Katika shughuli za kilimo jamii hufuga wanyama wa ndani, hulima mazao ya biashara ikiwemo kahawa, pia mazao ya chakula kama vile ndizi, mahindi, viazi na maharage. Mashamba humilikiwa na mtu binafsi na kuna mashamba ya pamoja. Aidha mashamba haya kwa kadri ya ukubwa wa familia yaligawanywa vijishemu vidogo vidogo ambavyo vilijulikana kama ***Vihamba*** au kikiwa kimoja ***Kihamba.*** Mashamba yaliyokuwa yakitumika kwa kilimo cha maharage na mahindi yanajulikana kama mashamba ya porini, wakati yale yaliyokuwa jirani na makazi ya nyumbani yalitumika kwa kilimo cha kahawa na ndizi. Wachagga walio wengi hufanya biashara ya maduka ya nguo, maduka ya bidhaa za ujenzi, biashara ya mazao na kila chochote anachoona kwamba kitampatia kipato halali. Kwa mfano katika mji wa Moshi wamiliki walio wengi wa maduka ni Wachagga. Asubuhi huteremka toka mlimani na kwenda kufanya biashara, jioni wote huanza tena safari ya kurudi mlimani ambako ndiko kuliko na makazi yao. Kutokana na biashara, Mchagga anapatikana kila kona ya nchi hii.

## 2.6 Nadharia iliyotumika kwenye Utafiti

Utafiti huu umejikita kwenye nadharia ya Kihemenitiki kwa sababu tatizo la utafiti linahusiana na Fasihi Simulizi. Uheminitiki ni taaluma inayohusiana na uelewaji na kutafsiri matini. Chimbuko la nadharia hii ni katika uchambuzi wa falsafa katika matini za kidini, hususan dini ya Kikristo. Msingi mkubwa wa nadharia ya Uhemenitiki ni imani ya kwamba matendo ya binadamu yanaathiriwa kwa njia mbalimbali na asasi tofauti zilizoko katika mazingira yake. Msingi huo unatupeleka katika dhana ya kuibua umuhimu wa kuelewa njia au mbinu za uelewaji wa maana za matini.

Gadaner (1960:269) anaeleza kwa msisitizo kwamba tafsiri haihusishi wala kutuepusha sisi kuwa kinyume na jamii inayozungumza nje ya makala. Kwa maana ya kwamba jamii zinaweza kutofautiana maana katika makala ya aina moja. Aidha, Senkoro (1987:7) naye amemnukuu Gadaner (1960) anasema: Taaluma ya Uhemenitiki hujihusisha na utafutaji wa maana ya kazi za Fasihi kwa kuuliza maswali muhimu manne:

i) Ni nini maana ya fasihi?

ii) Je, maana hii inahusianaje na kusudi la mawandishi?

iii) Je tunaweza kuzielewa kazi za fasihi na tamaduni na historia tofauti na zetu?

iv) Je, ni rahisi kupata uelewaji wa ndani wa kazi ya fasihi au hutegemea mazingira na historia ya hadhira ihusikayo?

Clines (1982:66) anasema kwamba hemenitiki ni fikra katika sanaa na sayansi ya kutafsiri. Anaendelea kusema kuwa hemenitiki inakubalika kwa sababu inakidhi mbinu za tafsiri na siyo tu matokeo ya tafsiri. Kwa hiyo katika habari tafsiri inapatikana kutokana na matokeo ya hemenitiki. Aidha, anasema kwamba kisayansi ili kupata tafsiri, kamusi inaweza kutumika katika kupata maana ya neno, lakini pamoja na kupata maana ya neno hilo ni lazima kupitia habari yote. Kuhusiana na sanaa anasema kwamba tafsiri inaweza kupatikana kutokana na mtu alivyoguswa na neno hilo, kwa hiyo maana zingine hazikamiliki kutokana na maamuzi yaliyojengwa kwa kipindi kirefu. Madai ya msingi ya nadharia ya Uhemenitiki yanahusisha dhana mbalimbali kama vile duara la kihemenitiki, utukuzaji pamoja na ile ya ufuatiliaji wa kisarufi, kisaikolojia na kimuktadha kama wasemavyo Senkoro (1987) na Wamitila (2002) walivyonukuliwa na Ponera (2010).

Wachterhauser (1991) anasema, ili kulielewa andiko, kunatakiwa ungano baina ya upeo wa ulimwengu tunaoishi na ulimwengu wa andiko, huo ukiwa ni ubunifu unaotoa maana

nyingie mpya. Waandishi wengine wanaozungumzia nadharia ya kihemenitiki ni kama vile Newton (1989), Eagleton (1983) na Tompkins (1980). Kutokana na maelezo ya wataalam wote hapo juu, hakuna shaka kwamba nadharia hii inaweza kukabiliana na tatizo la utafiti ambalo ni kuchunguza athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ambayo iko katika jamii ya Wachagga. Pamoja na kwmba nadharia hii inafafanua zaidi maandiko ambayo kwayo yanahusika katika fasihi andishi, lakini inatakiwa kujua kwamba fasihi simulizi ilikuweko kabla ya fasihi andishi. Kwa hiyo fasihi hiyo nayo ilikuwa na maana yake na maana hiyo ilihusishwa na jamii husika. Kazi za fasihi simulizi ni lazima zitajihusisha na utamaduni wa jamii hiyo na itakuwa inaangalia historia ya jamii hiyo pia. Hivyo katika kuzijua kazi ya fasihi kwa undani hatuna budi kuhusisha jamii inayohusika katika kutafitiwa.

## 2.7 Mwanya wa Utafiti

Utafiti huu umelenga kuziba pengo la athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga, baada ya kusoma maandiko na tasnifu zilizoandikwa na watafiti mbalimbali, mtafiti amegundua kuwa katika jamii ya Wachagga nyimbo za ngoma ya *Mbassa,* hazikuwa zimechambuliwa maudhui yake. Pia hakuna mtafiti ambaye amechunguza athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo hizo za ngoma ya *Mbassa*. Kutokana na sababu hiyo, ilimpa mtafiti ari na msukumo wa kukusanya nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga na kuchambua maudhui yake, likiwa ni lengo la kwanza ndani ya lengo kuu la utafiti. Ili kuziba mwanya huo vizuri, mtafiti ametumia lengo la pili ambalo ni kuchunguza na kubainisha athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga. Malengo hayo mawili yatakapochambuliwa kikamilifu yatakuwa yameziba mwanya wa

utafiti ambao ni athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga.

Iser (1978), anasema kwamba katika kuhakiki kazi ya fasihi, kuna nafasi iliyo wazi kati ya mwandishi na msomaji, hivyo basi kwa mhakiki yeyote anayo nafasi ya kuondoa huo uwazi ili kupata maana iliyotarajiwa. Anandelea kusema kwamba kazi kubwa iko mbele ya msomaji, ambaye ndiye mwenye dhamana kwa kushika kalamu yake na kuweka bayana yale yote aliyoyaona, kuyaweka wazi zaidi badala ya kutegemea tahakiki zilizoandikwa. Aidha, kwa kuzingatia maelezo hayo ya Iser, yeye akiwa anaonyesha namna ya kupata uwazi katika fasihi andishi, mtafiti anaona kuwa katika fasihi simulizi, unaweza kuonekana pale msanii anaposimulia hadithi, methali au anapoimba nyimbo. Katika muktadha huo wa masimulizi hadhira, mtambaji, mandhari vyote vinakuwepo. Muktadha huo unaweza kusaidia kubainisha uwazi uliopo katika fasihi simulizi.

## 2.8 Hitimisho

Sura hii ya pili ilihusika katika kupitia maandiko mbalimbali, na tasnifu zilizokuwa zimeandikwa kuhusiana na masuala ya fasihi simulizi, maandiko yaliyokuwa yamelenga katika ufafanuzi wa dhana za maudhui na nyimbo zikiwemo nyimbo za makabila mbalimbali yanayopatikana nchini Tanzania, historia na maisha ya jamii ya Wachagga. Pia ufafanuzi wa maana ya nyimbo za ngoma ya *Mbassa* umefanyika katika sura hii, ukionesha viashiria vya maendeleo ambavyo vinajitokeza katika jamii ya Wachagga. Mwisho ni mwanya wa utafiti. Mambo hayo yote yamelenga kumsaidia mtafiti katika mada ya utafiti inayohusiana na athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga. Kukamilika kwa sura hii kunasaidia mtafiti kuandika sura ya tatu inayohusika na mbinu na vifaa vya utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii ya tatu inalenga kushughulikia mpango wa jumla wa utafiti, eneo la utafiti, zana za kukusnyia data, mbinu/njia za kukusanyia data, mchakato wa ukusanayaji data na udhibiti wake. Masuala mengine ni sampuli ya watafitiwa, mipaka ya utafiti na chanangamoto zilizojitokeza katika utafiti.

## 3.2 Mpango wa Jumla wa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa uwandani na maktaba. Uwandani mtafiti alitembelea maeneo mbalimbali kwa lengo la kukutana na walengwa waliokusudiwa. Kuhusu maktaba mtafiti alitembelea taasisi mbalimbali za kielimu kwa lengo la kupata maandiko yaliyohusiana na mada yake ya utafiti. Data zilizokusanywa ni zile ambazo zilijikita katika kuchunguza athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga. Aidha, katika kuzipata nyimbo hizo za ngoma ya *Mbassa*, ilibidi kuonana ana kwa ana na makundi yaliyokusudiwa kutafitiwa wakiwemo manju, wazee wanaume kwa wanawake na vijana wake kwa wanaume. Katika harakati za utafiti, mtafiti alitumia mbinu na njia mbalimbali katika kupata habari. Baadhi ya njia na mbinu zilizotumika katika kukusanyia data ni kama vile hojaji, dodoso, ushiriki wa utendaji na majadiliano ya kikundi. Njia hii ya majadiliano ya vikundi imetumiwa na mtafiti kwa sababu ya makundi yaliyolegwa, na ina uhusiano wa karibu na mada ya utafiti. Pia mtafiti ameamua kutumia njia hii kwa sababu inampatia mtafiti taarifa nyingi kwa haraka na fanisi ambazo zimesaidia kuielezea jamii hiyo ilivyo. Mbinu nyingine ambazo zimetumika katika utafiti huu ni kama vile mbinu ya walengwa maalum, mbinu hii imetumiwa na mtafiti kupata sampuli lengwa ya watafitiwa wake kwa mfano manju. Kwa msingi huo mbinu hii

ilisababisha kujitokeza kwa mbinu nyingine inayoitwa mbinu ya kusogezeana, mbinu hiii imetumika kwa sababu kulitokea kipindi ambacho mtafitiwa alimwagizia mtafiti kwenda kwa matafitiwa mwingine na vile vile mtafiti kuongozwa kwa mtafitiwa mwingine, hatimaye mtafiti kujikuta kuingia katika mbinu hiyo. Mbinu ya uchanguzi holela pia ilitumika. Mbinu hii imetumiwa na mtafiti kwa sababu ya makundi aliyoyalenga kwa ajili ya uwasilishaji wa walio wengi. Mbinu nyingine iliyotumika ni ufafanuzi wa matini. Mbinu hii imetumiwa na mtafiti kwa sababu ya kutokuwa na muda wa kutosha katika kupitia matini moja moja.

### 3.3 Zana za Kukusanyia Data

Sehemu hii inaelezea zana ambazo zimetumiwa na mtafiti katika kukusanyia data, kuhusiana na mada ya utafiti. Zana ambazo zimetumika katika kukusanyia data ni pamoja na karatasi za maswali ya dodoso, maswali ya hojaji, kamera, kalamu, daftari la nukuu (note book), na ngamizi. Maswali ya dodoso yalitumiwa na mtafitti kwa ajili ya kutuma kwa watu mbalimbali kama walivyoanishwa kwenye kundi la watafitiwa. Maswali ya hojaji, yametumika kwa madhumuni ya makundi ambayo yalikusudiwa na mtafiti. Aidha, watafitiwa walipatikana kwa kadri ya makundi yaliyokusudiwa, hivyo kuombwa kujibu maswali kama yalivyoanishwa na mtafiti. Kamera iliyotumika ni ya kupiga picha za mgando na jongea. Daftari la nukuu (note book) mtafiti alilitumia kila mahali alipokuwa katika safari zake za utafti na ngamizi iltumika katika kuchapa kazi ya utafiti na kurekodi nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zilizokusanywa.

### 3.4 Njia/Mbinu za kukusanyia data

Njia ambazo mtafiti amezitumika kukusanyia data ni pamoja na hojaji, dodoso, ushiriki wa utendaji na majadiliano ya kikundi. Hojaji na dodoso ni mbinu zilizotumika katika

kundi la manju na vijana wa kike kwa wa kiume katika kuuliza maswali yaliyokuwa yameandaliwa na mtafiti. Kulikuwa na tatizo katika mbinu ya dodoso kwa sababu baadhi ya wahojiwa walikuwa hawajui kusoma, kwa hiyo ilimlazimu mtafiti kuwafikia walengwa na kuwasomea. Katika mbinu ya ushiriki wa utendaji, mtafiti alishiriki kucheza na kuimba nyimbo za ngoma ya *Mbassa* hususan wakati kundi la manju na kundi la wazee waume kwa wake walipokuwa wakiimba na kucheza. Kushiriki kwa mtafiti, kuliwafanya watafitiwa waimbe kwa ari na mori mkubwa, baada ya kuona hata mgeni ameshiriki. Mbinu ya majajiliano ya kikundi ilitumika, hususani kwenye kundi la vijana wasichana kwa wavulana, mtafiti alikaa na watafitiwa akiongozwa na mwongozo C, aliweza kufafanua swali kwa baadhi ya wale ambao walikuwa hawaelewi. Mbinu hii ilikuwa nzuri, lakini mtafiti asipokuwa makini anaweza kujikuta ametoka nje ya maswali. Katika mbinu zote hizi, kumetumika pia nyaraka za kumbukumbu za kimaktaba. Kuhusiana na maswali ya dodoso, mtafiti alidodosa maswali tisa yaliyohusiana na kuijua ngoma ya *Mbassa* kwa undani. Makundi yote yaliyotajwa ambayo ni wanaume na wanawake yalipatikana na walisadia kujaza madodoso waliyopewa na mtafiti. Maswali ya hojaji yaliyopangwa kuulizwa kwa manju, makundi ya vijana wanaume na wasichana, wazee wanaume na wanawake, yalijibiwa na makundi hayo kulingana na watafiti walivyokuwa wamekusudia. Maswali yake yalikuwa kumi kwa manju na kumi kwa kundi la wazee wanaume na wanawake na kundi la vijana wasichana kwa wavulana. Makundi ya watafitiwa yalipatikana kwa watafiti kuwasiliana na uongozi ngazi ya kijiji na kujitambulisha pia kueleza adhima ya utafiti wao, jambo liliIofanya uongozi wa kijiji kuridhika na utafiti huo, hatimaye kuwaelekeza watafiti namna na sehemu ya kuwapata watafitiwa.

### 3.4.1 Mahojiano

Mahojiano ni njia amabayo imetumiwa na mtafiti. Njia hii imetumika kwa mhojaji (mtafiti) kukaa na walengwa ambao walichaguliwa katika kujibu maswali ya utafiti. Hapa itakumbukwa kwamba mtafiti anakuwa na maswali ya hojaji aliyolenga kuyatumia katika kundi la Manju, vijana wasichana kwa wavulana na kundi la wazee wanaume kwa wanawake. Tatizo la njia hii ni kwamba mtafiti ni lazima aifahamu lugha ya watafitiwa Raj (2005) anasema, mahojianao ni njia ya kukusanya data ambayo mhojaji (mtafiti) huwakaribisha wahojiwa kuwauliza maswali na kurikodi majibu wanayoyatoa.

### 3.4.2 Mbinu za Utafiti

Katika utafiti huu kumetumika mbinu mbalimbali zikiwemmo mbinu ya kundi maalum. Mbinu hii imetumiwa na watafiti hasa katika kupata sampuli lengwa. Kwa mfano watafiti wametumia manju kama kundi maalum ambalo limehusika katika kuimba nyimbo za ngoma ya *Mbassa*. Kundi hili lilikuwa ni lazima lipatikane kutokana na umuhimu wake katika suala zima la ukusanyaji wa data. Katika kundi hili lililenga watu wazima, wanawake kwa wanaume kwa sababu nyimbo hizi kwa kipindi cha nyuma zilikuwa zinaimbiwa watoto wa kike ambao walikuwa wanafanyiwa tohara katika muktadha wa unyago. Kothari (2010) anasema mbinu hii inatumika katika kupata kundi dogo kutoka kwenye kundi kubwa lenye makundi madogo madogo, pia ni mbinu ambayo ikitumika inatoa matokeo na taarifa kwa undani zaidi.

Mbinu nyingine ni mbinu ya kusogezeana Kombo na Tromp (2006) wanasema kwamba kuna kipindi mtafitiwa analazimika kumwelekeza mtafiti kwa mtafitiwa mwingine kutokana na yeye kutokuwa na data za kumtosheleza, vivyo hivyo kwa wa tatu na kundelea, hadi kwa yule ambaye mtafiti atakuwa amekidhi data anazozihitaji.

Mbinu ya uchaguzi holela ni miongoni mwa mbinu iliyotumiwa na watafiti. Kothari (2010) anasema kwamba hii ni mbinu ya yamkini kwa ajili ya kupata sampuli ndogo kutoka kwenye sampuli kubwa, ambayo sampuli zote kwenye sampuli kubwa huwa na nafasi sawa ya kuchaguliwa.

Mbinu ya ufafanuzi wa matini nayo imetumika katika kupata data za utafiti. Shufaa (2011:12) akimnukuu Raj (2005:153) anasema, maandiko yanampatia mtafiti taarifa zinazohusiana na mada inayotafitiwa. Anaendelea kusema kuwa inatoa ithibati ya data zilizokusanywa kwa mahojiano na ushuhuda wa data zilizopatikana kwenye maandiko.

### 3.4.3 Mbinu ya kusogezeana

Hii ni mbinu ambayo imetumiwa na mtafiti hasa kwa kipindi ambacho alishindwa kupata data za kutosheleza kwa walengwa wake wakiwemo manju kwa hiyo mtafiti alijikuta akielekezwa kwa manju mwingine kwa ajili ya kupata taarifa ambazo manju wa kwanza hakuweza kumpatia. Manju wa pili naye alimwelekeza kwa mtu mwingine, hatimaye naye huyo hakuwa na data zilizotosheleza kwa mtafiti hivyo alilazimika kwenda kwa mtu mwingine, hadi kwa yule ambaye alimpatia data za kuridhisha. Matumizi ya mbinu hii yalitumika kwa sababu kundi la Manju waliobakia katika kuimba nyimbo za ngoma ya *Mbassa* walikuwa wachache, na vijana waliokuwa wengi walikuwa hawazifahamu nyimbo za ngoma ya *Mbassa*. Sababu nyingine iliyochangia kutopatikana kwa watafitiwa, ni kutokana na shughuli za kibiashara na kilimo. Lakini kuna changamoto ambazo zilijitokeza katika kutumia mbinu hii, zikiwemo kusafiri umbali mrefu kwa miguu kutokana na miundombinu, kuwalipa watafitiwa na kutumia muda mwingi katika kumpata mtafitiwa.

### 3.4.4 Mbinu ya Uchaguzi Holela

Katika kupata kundi la walengwa la vijana na wazee ambao walikuwa wanahitajika katika kujibu maswali ya dodoso na hojadi, ilimlazimu mtafiti kutumia mbinu hii kwa sababu eneo la utafiti lilikuwa kubwa kiasi kwamba isingeliwezeka kuwatumia vijana na wazee wote katika eneo hilo la utafiti katika kuwadodosa na kuwahoji. Katika matumizi ya mbinu hii, mtafiti alijikuta kupata baadhi ya watu wasiojua kusoma na kuandika, hivyo kusababisha kutumia muda mwingi katika kutoa maelezo mengi katika hojaji.

### 3.4.5 Mbinu ya Ufafanuzi Matini

Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti katika kupitia maandiko na ripoti mbalimbali. Mtafiti alilazimika kutumia mbinu hii kwa sababu alibainisha mapema kwamba utafiti wake utahusisha maktaba. Mtafiti alipitia maandiko na ripoti zilizokuwa zimeandikwa na watu binafsi, asasi na mashirika. Mbinu hii ilisaidia sana katika utafiti, lakini kulikuwa na baadhi ya changamoto ikiwa ni pamoja na mtafiti kulazimika kutumia gharama katika kupata data zilizohusiana na ripoti, hususan kwenye mashirika na asasi.

## 3.5 Mchakato wa Ukusanyaji Data na Udhibiti wake

Mchakato wa ukusanyaji data ulianzia kwa kupitia tasnifu na maandiko mbalimbali yaliyohusiana na mada ya utafiti kwa upande wa maktaba. Kwa upande wa uwandani mtafiti alienda kujitambulisha katika ofisi za Maafisa Utamaduni wa mkoa wa Kilimanjaro katika wilaya ya Moshi Vijijini, ambao walisadia sana katika kuelekeza watu ambao waliweza kutoa data kwa mtafiti. Katika mchakato wa ukusanyaji data Kombo na Tromp (ibid 2006) wanaelezea utaratibu ambao unatakiwa kufuatwa:

> In research the term “data collection” refers to gathering specific information aimed at proving or refuting some facts. In data collection the researcher must have a clear understanding of what

> they hope to obtain and how they hope to obtain it. In data collection, the researcher must have a clear vision of the instruments to be used, the respondents and the selected area. Data collection is important in research as it allows for dissemination of accurate information and development of meaningful programmes.

> Katika utafiti istilahi "ukusanyaji data" inarejea kuweka pamoja taarifa maalum kwa lengo kuhakiki ukweli. Katika ukusanyaji wa data mtafiti lazima awe na uelewa wa nini anachotaka kukipata na matumaini ya namna ya kukipata. Katika ukusanyaji wa data, mtafiti ni lazima awe na mtizamo sahihi wa zana atakazotumia, watafitiwa na eneo la utafiti. Ukusanyaji wa data ni muhimu katika utafiti kwa maana unaruhusu kusambaza taarifa sahihi na mipango kamili ya maendeleo. (Tafsiri yetu)

Katika makundi yote yaliyochunguzwa, mtafiti aliwahakikishia utunzaji wa siri kwa taarifa zote ambazo wamezitoa kwa watafiti.

### 3.6 Sampuli ya Watafitiwa

Mtafiti amechagua sampuli kutokana na makundi yalivyokuwa yamepangwa, ambayo ni makundi matatu yaliyogawanyika kwa jinsi tofauti. Kundi la kwanza lililolengwa ni manju walau sita waliozijua nyimbo za ngoma ya *Mbassa*, kundi la pili ni wazee wanaume kwa wanawake kumi kwa kila jinsi wanaozijua nyimbo za ngoma ya *Mbassa* na kundi la tatu ni vijana wa kike na kiume, kumi kwa kila jinsi ambao pia wanazijua nyimbo za ngoma ya *Mbassa.* Jumla ya watafitiwa wote ilkuwa arobaini na sita.

Kothari (1993:58) anaeleza kuhusiana na sampuli anasema:

> A sample refers to the selected respondents from the target population for a study. A sample helps the study to be focused, that is identifying the required respondents with relevant information. It also reduces costs."

> Sampuli inahusika na kundi la watafitiwa lililochaguliwa kutoka katika jamii iliyolengwa kutafitiwa. Sampuli inasaidia utafiti kuwa na dira, kubainisha watafitiwa wanaohitajika na wenye kutoa habari sahihi. Pia inapunguza gharama. (Tafsiri yetu)

### 3.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti ulikusudia kuchunguza athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga. Utafiti huu umefanyika katika mkoa wa Kilimanjaro, wilaya ya Moshi Vijijini, hususan eneo la Tarafa ya Kibosho. Katika utafiti huu mtafiti amekukusanya na kuchambua maudhui ya nyimbo isirini na tatu. Katika nyimbo zilizokusanyawa hizo ishini na tatu ndizo zilizoonekana kukidhi mada ya utafiti. Nyimbo hizi zimekusanywa katika mazingira mbalimbali yakiwemo mazingira ya sehemu jamii inakonywea pombe za kienyeji (mbege), nyumbani kwa watafitiwa, mashambani wakati wakiwa wanavuna na kwenye sherehe mbalimbali za kidini na kisiasa.

### 3.8 Changamoto katika ukusanyaji wa data

Mtafiti alikutana na changamoto mbalimbali katika ukusanyaji wa data ikiwa ni pamoja na kutoyapata makundi ya wazee wanaume kwa wanawake, vijana wengi kutokuwa na kumbukumbu ya nyimbo za jadi za jamii ya Wachagga. Katika kuwapata baadhi ya wazee, kuna wazee ambao walikuwa wanalelewa na watoto wao, wengine wakiwa sehemu za mjini, hivyo mtafiti alilazimika kuwafuta. Pia watafitiwa walidai malipo katika utoaji wa data. Katika changamoto hii, mtafiti alijieleza lengo la utafiti wake ni nini, hususan kwa kundi la vijana na hatimaye walimwelewa. Lakini kwa kundi la wazee hususan manju, mtafiti alilazimika kuingia gharama ili aweze kupata data. Ukusanyaji data ulifanyika kipindi cha mavuna hivyo watafitiwa wengi walikuwa kwenye kazi ya kuvuna mahindi. Katika changamoto hii, mtafiti alilazimika kuwafuata watafitiwa mashambani, jambo ambalo lilisaidia sana kwa sababu nyimbo zingine walikuwa

wanaziimba walipokuwa wanaendelea kuvuna. Changamoto kubwa aliyokumbana nayo mtafiti, ni suala la gharama (fedha) katika kipindi cha ukusanyaji data. Utafiti umetumia gharama kubwa kufuatia maeneo ya utafiti yaliyokuwa yamepangwa na mtafiti. Katika kukabiliana na changamoto hii, mtafiti alilazimika kuingia kwenye mkopo katika taasisi za fedha ili kufanikisha adhima ya utafiti.

### 3.9 Hitimisho

Kukamilika kwa sura hii ya tatu iliyojihusisha na mpango wa jumla wa utafiti, zana za kukusanyia data, njia au mbinu za kukusanyia data, mchakato wa ukusanyaji data na uthibiti wake, sampuli ya watafitiwa, mipaka ya utafiti na changamoto katika ukusanyaji data, inamsaidia mtafiti kuingia katika sura ya nne ambayo inahusika na uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa matokeo ya utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii matokeo ya utafiti huu, uwasilishaji na uchambuzi wake umefanyika kwa baadhi ya nyimbo zilizokusanywa kutoka katika eneo la utafiti. Nyimbo zilizokusanya idadi yake ni ishirini na tatu. Lengo la kwanza la utafiti huu, ambalo ni kukusanya nyimbo za ngoma ya *Mbassa* na kuchambua maudhui yake, limechambuliwa kwa kutumia dodoso A na baadhi ya maswali yaliyoko kwenye mwongozo B na C. Katika lengo la pili la utafiti huu ambalo ni kuchunguza na kubainisha athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa,* lengo hili limechambuliwa kwa kutumia mwongozo wa hojaji B na C, ambayo miongozo hii yote inapatikana katika viambata vya utafiti huu. Uchambuzi na uwasilishaji wa malengo yote haya umetumia maelezo ambayo yameongozwa na nadharia ya kihemenitiki kama ilivyofafanuliwa katika sura ya pili.

## 4.2 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data zilizokusanywa

Uwasilishaji wa data zilizokusanywa umekuwa kwa njia ya maelezo. Nadharia ya kihemenitiki ambayo inataka kujua maana ya fasihi, namna maana hiyo inavyohusiana na kusudi la mtunzi na kama kazi za fasihi za tamaduni na historia tofauti na zetu zinaweza kuelezwa na ikiwa kama ni rahisi kupata uelewaji wa ndani wa kazi ya fasihi, au hutegemea mazingira na hadhira inayohusika. Hivyo basi nadharia hii imejikita katika lengo kuu la utafiti huu ambalo ni athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga. Mazingira ambayo zilipatikana nyimbo hizi, ni mazingira ya vilabu vya kiyenyeji, ambako wazee wengi hupenda kukusanyika majira ya kuanzia saa tisa alasiri. Pia mazingira mengine ni nyumbani kwa watafitiwa ambako

mtafiti alilazimika kuwafuata. Aidha kuna baadhi ya nyimbo nyingine zilikusanywa kwenye mazingira ya sherehe mbalimbali zikiwemo za kidini na za kisiasa.

### 4.2.1 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Lengo la Kwanza

Lengo la kwanza katika utafiti huu ni kukusanya nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga na kuchambua maudhui ya nyimbo hizo. Katika Lengo hili, mtafiti amechambua maudhui katika nyimbo kuni na moja. Uchambuzi huo wa maudhui umezingatia dhamira, ujumbe, itikadi, mtazamo na msimamo. Uchambuzi wa Nyimbo hizi umezingatia muktadha wa wimbo wenyewe, namna unavyoimbwa, hadhira iliyohuska na fanani anayeuimba wimbo huo.

#### 1. WARISINDA (SHEMEJI)

| | |
|---|---|
| *Warisinda kocha Kimatiee* | Shemeji karibu Kimati |
| *Ee kocha Kimatiee* | Ee karibu Kimati |
| *Wari woko lyekora ukouee* | Pombe yangu nilipika jana |
| *Lyekora ukouee* | Nilipika jana |
| *Oh! Kuche kuniya kune Kimatiee Oh*! | Uje kunywa unywe Kimati |
| *Kune Kimatiee* | Unywe Kimati |
| *Kokunda kuleye kune Kimatiee* | Ukipenda ukatae kunywa Kimati |
| *Kuleye Kimatiee* | Ukatae Kimati |
| *Oh! Ng'unung'unu sinda dukaee* | Oh! Kunong'onanong'ona chini ya mti |
| *Sinda dukaee* | Chini ya mti |
| *Oh! Sinda duka kikweshafoee* | Oh! Chini ya mti ulikuwa unatafuta nini |
| *Kikweshafoee* | Ulikuwa unatafuta nini |
| *Oh! Ngiwiya tata nyalambalee* | Oh! Niambie babu alisema |
| *Kobara kikombe kulipe kilasiee* | Ukipasua kikombe ulipe glasi |
| *Kulipe kilasiee* | Ulipe glasi |
| *Ee woshiolelee ee woshiolelee* | Ee woshiolelee ee woshiolelee |
| *Ngadino landewa* | Nikatairiwa kabla |
| *Oh! Kulya ko Nlayi kuleleyoee* | Oh! Kule kwa Mlayi kumekataliwa |
| *Kuleleyoee* | Kumekataliwa |
| *Kwendafo kubariyo kilasiee* | Ukienda uko utapasuliwa glasi |
| *Kubariyo kilasiee* | Utapasuliwa glasi |

**Chanzo: Mzee Joseph Karani Mushi miaka 78, tarehe 25/10/2012, Kijiji cha Mango, Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo ambao ulikuwa unaimbiwa kipindi msichana anapotolewa nje kama mwali. PAYODE (2012:30) wanasema, unyago ni sehemu ya Utamadudi kwa watu wanaoishi Pwani ya Tanzania. Watu hao hutumia utamaduni huo kumfundisha mtoto wa kike aliyevunja ungo, mambo muhimu yanayohusu afya ya uzazi, usafi na majukumu mengine yanayomhusu. Utamaduni huo umesaidia kwa kiasi kikubwa kuweka njia kwa watu wazima ambao kwa pwani wanajulikana kama Wanyakanga. Wanyakanga hawa huwaandaa wasichana kwa maisha ya utu uzima. Mwisho wa mafunzo ya Unyago wasichana ambao huitwa wali, hutolewa nje kwa sherehe maalum ya kuhitimu ijulikanayo kama *Kunema.* Sherhe hizi huambatana na ngoma za watu wa pwani.

Katika jamii ya Wachagga ilikuwa na desturi ya kuwafanyia sherehe watoto wa kike ambao walikuwa wamefanyiwa tohara. Katika sherehe hizo ziliimbwa nyimbo ambazo zilitoa mafunzo mbalimbali. Katika uimbaji wa nyimbo hizo kulitumika lugha iliyokuwa na maneno ya kawaida lakini iliyokuwa ya mafumbo. *Warisinda* ni wimbo ambao unatoa mafundisho ya kumkataza mtoto wa kike kufanya mapenzi kabla ya kuolewa. Maudhui ya wimbo huu yalilenga kumpa maadili mwali huyo kuhusiana na madhara ya kufanya mapenzi kabla ya kuolewa. Katika wimbo huu, Kimati ni kijana ambaye ni mchumba mtarajiwa wa mwali aliyetolewa nje. Kwa mfano, msanii anaposema:

| | |
|---|---|
| *Warisinda kocha Kimatiee* | Shemeji karibu Kimati |
| *Ee kocha Kimatiee* | Ee karibu Kimati |
| *Wari woko lyekora ukouee* | Pombe yangu nilipika jana |
| *Lyekora ukouee* | Nilipika jana |
| *Oh! Kuche kuniya kune Kimatiee* | Oh! Uje kunywa unywe Kimati |
| *Kune Kimatiee* | Unywe Kimati |
| *Kokunda kuleye kune Kimatiee* | Ukipenda ukatae kunywa Kimati |
| *Kuleye Kimatiee* | Ukatae Kimati |

Hapa msanii anaonekana kutumia lugha ya mafumbo, lakini ni katika hali ya kumwelezea msichana (mwali) kwamba amekwishavunja ungo na anaweza kuolewa. Mbali na kwamba mwali huyo anaweza kuolewa, bado msanii anaelezea madhara ambayo angeliweza kuyapata iwapo angelifanya mapenzi kabla ya kuolewa kwa kusema:

| | |
|---|---|
| *Oh! Ngiwiya tata nyalambalee* | Oh! Niambie babu alisema |
| *Kobara kikombe kulipe kilasiee* | Ukipasua kikombe ulipe glasi |
| *Kulipe kilasiee* | Ulipe glasi |

Hapa msanii anaonesha kuwa binti huyo anaweza kupoteza ubikira wake ikiwa atafanya mapenzi kabla ya kuolewa. Katika jamii ya Wachagga, msichana ambaye hakukutwa na ubikira siku ya kuolewa, alionekana ni malaya na alidharaulika katika jamii. Kutokana na mabadiliko ya kimaendeleo katika jamii ya Wachagga, ambayo yamechangiwa na suala la kuingiliana katika tamaduni, kuachana na mila potofu ikiwemo ukeketaji, wimbo huu umeathiriwa kimandhari kwa sababu katika jamii ya Wachagga, vyombo ambavyo vilikuwa vinatumika katika kunywea pombe (mbege) vilijulikana kama kata, lakini katika wimbo huu msanii ametumia neno glasi na hata manju aliyehojiwa alipouimba, alitumia neno chupa maneno ambayo yanaonyesha kubadilika kutokana na muktadha uliopo kwa sasa. Pia, kufuatia hojaji na kwa kuzingatia mahojiana yaliyofanyika kati ya manju na mtafiti, inaonesha wazi kuwa wimbo huu umeathiriwa kimandhari kwa sababu kwa sasa unaimbwa kwenye muktadha wa harusi, wakati wa sherehe za Krismas na kwenye shughuli za kupura maharage. Kufuatia ushahidi huo wa hojaji, hakuna ubishi kwamba wimbo huu unapoimbwa katika mikutdha mingine, bado unasawiri jamii ya Wachagga kutokana na maudhui yaliyomo katika wimbo huo. Dhima ya wimbo huu ilikuwa katazo kwa mtoto wa kike kufanya mapenzi kabla ya kuolewa na madhara ambayo atayapata ikiwa atafanya hivyo. Bado katazo hili liko katika jamii ya Wachagga, na ndiyo maana wimbo huu unashadidia kusawiri katika jamii hiyo. Aidha, kwa mtoto wa kike

kutozingatia maadili haya, madhara ya siku hizi ni mengi, yakiwemo magojwa ya zinaa na UKIMWI pamoja na kupata mimba za utotoni.

### 2. WIRAWIRA (TEPETATEPETA)

| | |
|---|---|
| *Wirawira chokyisa nyawoye x2* | Tepetatepata makalio yaanguke x2 |
| *Baba lyako lingane iyowe* | Baba yangu mkubwa sana |
| *Wirawira chokyisa nyawoye* | Tepetatepeta makalio yaanguke |
| *Mayi lyako lingane iyowe* | Bibi yangu mkubwa sana |
| *Wirawira chokyisa nyawoye* | Tepetatepeta makalio yaanguke |
| *Nsaachalyako lingane iyowe* | Kaka yangu mkubwa sana |
| *Wirawira chokyisa nyawoye x2* | Tepetatepeta makalio yaanguke |
| *Ekato mwichye munae* | Huyo mshenga wa mtoto |
| *Wirawira chokyisa nyawoye* | Tepetatepeta makalio yaanguke |
| *Ekato sawoyae munae* | Huyo babu yake mtoto |
| *Wirawira chokyisa nyawoye* | Tepetatepeta makalio yaanguke |
| *Ekato mamye munae* | Huyo mama mkwe wa mtoto |
| *Wirawira chokyisa nyawoye* | Tepetatepeta makalio yaanguke |
| *Ekato wandasae womunae* | Huyo jirani wa mtoto |
| *Wirawira chokyisa nyawoye* | Tepetatepeta makalio yaanguke |
| *Muna kwendye kukarishye* | Mtoto ukienda ujikaze |
| *Wirawira chokyisa nyawoye x2* | Tepetatepeta makalio yaanguke x2 |

**Chanzo: Mama Maria Morisi miaka 62, tarehe 17/10/2012, Kijiji cha Umbwe, Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo ambao ulimfariji na kumpongeza mtoto wa kike alipokuwa anapelekwa kwa ngariba kwa ajili ya kukeketwa, na siku ile alipotolewa nje, anaambiwa kuwa asiwe na wasiwasi kwa sababu baba, mama, kaka, msimamizi, na hata majirani wote wako kwa ajili yake. Wimbo huu ulikuwa unaimbwa kwenye ngoma ya *Mbassa* siku ya kukeketwa mtoto wa kike na siku ile ya mwisho alipokuwa anatolewa nje katika muktadha wa unyago. Huu ni wimbo uliokuwa unaimbwa kuonyesha majigambo katika familia kwamba walikuwa na uwezo wa kumtunza mtoto aliyefanyiwa tohara kwamba amenawiri, amenenepa na anapendeza. Kwa mfano mwimbaji anaposema,

*Baba lyako lingane iyowe* Baba yangu mkubwa sana
*Mayi lyako lingane iyowe* Bibi yangu mkubwa sana
*Nsacha lyako lingane iyowe* Kaka yangu mkubwa sana

Neno *lingane* (kubwa) linaonesha uwezo na utajiri walionao familia ndiyo maana anatajwa baba, bibi na kaka, kudhihirisha kwamba ni familia yenye uwezo kiuchumi. Kwa hiyo ujumbe huo unasambazwa kupitia waliohudhuria, kama msanii anavyosema:

*Ekato wandasae muna* Huyo jirani wa mtoto
*Ekato mamyi muna* Huyo mama mkwe wa mtoto

Wote hawa wanaotajwa wakiwemo majirani na mama mkwe mtarajiwa wa mtoto wa kike, walifika si tu kushiriki katika sherehe hizo, bali walifika pia kwa ajili ya kutafuta maneno ya kusema mitaani. Wimbo huu ulimfundisha mtoto wa kike kuwa na utii, heshima na ukarimu kwenye familia atakayoolewa. Katika wimbo huu dhamira kuu ni matunzo bora. Halafu ujumbe unaopatikana katika huo wimbo ni utii, ukarimu, umbeya, utajiri na uvumilivu. Jamii ya Wachagga inaamini kuwa matunzo kwa mtoto wa kike aliyefanyiwa tohara ni lazima. Mtazamo na msimamo unaopatikana katika wimbo huu ni kwamba mtoto wa kike wa jamii ya Kichagga ambaye hakufanyiwa tohara, alikuwa haolewi.

Kutokana na mabadiliko yaliyoko katika jamii kuhusiana na nyanja ya kijamii, leo hii kupitia vyombo vya habari kama vile magazeti, redio, televisheni na elimu ya asasi zisizo za kiserikali, kunatolewa elimu dhidi ya madhara ya ukeketaji wa watoto wa kike. Aidha, kufuatia mabadiliko hayo, jamii ya Wachagga imeachana na tabia ya kukeketa watoto wa kike. Jambo ambalo limechangia katika kuathiri nyimbo za ngoma ya *Mbassa*. Nyimbo hizi zimeathiriwa katika vipengele vya mandhari, hadhira na tukio linalotendeka. Wimbo huu umebakia kuimbwa kwenye mikutadha mingine kama vile sherehe za kuzaliwa mtoto. Kwa kuwa tunaelezwa kuwa dhima kubwa ya fasihi ni kuburudisha na kuelimisha, bado wimbo huu unasawiri katika jamii ya Wachagga kuendana na maudhui yake ambayo

dhima kubwa ni kueleza utii, ukarimu, heshima na utajiri, mambo ambayo bado yamo ndani ya jamii ya Wachagga, na yanasisitizwa kwa wanajamii wote.

### 3. Oh! KIWONA (Oh! ANGALIA)

| | |
|---|---|
| *Oh! Kiwona* | Oh! Angaliya |
| *Baba kwelele bo* | Baba ulilala nje |
| *Oh! Kiwona* | Oh! Angalia |
| *Nsacha kwelele bo* | Kaka ulilala nje |
| *Oh! Kiwona* | Oh! Angalia |
| *Mayi kwelele bo* | Mama ulilala nje |
| *Oh! Kiwona* | Oh! Angalia |
| *Mayi kashandare ee kashandare x2* | Mama Ukahangaika |
| *Baba kashandare ee kashandare x2* | Baba ukahangaika |
| *Oh! Mbede na kyenda kishamba* | Oh! Mngoje hata kama yuko mbali |
| *Oh! Kiwona* | Oh! Angalia |
| *Baba kwelele bo* | Baba ulilala nje |
| *Oh! Kiwona* | Oh! Angalia |
| *Mayi kwelele bo* | Mama ulilala nje |
| *Oh! Kiwona* | Oh! Angalia |
| *Nsacha kwelele bo* | Kaka ulilala nje |
| *Oh! Kiwona* | Oh! Angalia |
| *Oh! Mbede na kyenda kishamba* | Oh! Mngoje hata kama yuko mbali |
| *Oh! Kiwona* | Oh! Angalia |

**Chanzo: Mama Maria Morisi miaka 62, tarehe 17/10/2010, Kijiji cha Okaoni Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo unaoelezea hali ya kuwatia matumaini wazazi na wanandugu wa mtoto ambaye alikuwa anafanyiwa tendo la kukeketwa, wanaambiwa kuwa wawe na amani, wasiwe na wasiwasi, wasubiri hata kama amepelekwa mbali atarudi. Huu ni wimbo wa ngoma ya *Mbassa* ambao uliimbwa katika muktadha wa unyago. Wimbo huu ni wa kuliwaza na kufariji katika matatizo, uliimbwa na mshenga wa mtoto wa kike wakati anampeleka kwa bibi anayekeketa (ngariba), alikuwa anawaeleza wazazi wa mtoto wa kike aliyepelekwa kukeketwa kwamba wasiwe na wasiwasi, wasubiri tu atarudi salama. Baadhi ya mabinti waliokuwa wanaenda kukeketwa waliingiwa na hofu iliyowasababisha kuzirai na hata kuzimia kabla ya kufika kwa mkeketaji. Jambo hili liliwapa wasiwasi wazazi wa binti kwa sababu ni hali iliyoashiria kwamba angelishindwa kucheza ngoma,

na kwa maana hiyo, sherehe isingekuwepo. Mafundisho yaliyokuwa yanatolewa na wimbo huu kwa mtoto wa kike ni kumweleza kwamba anatakiwa kujua kuwa amefikia utu uzima ambao utamwingiza kwenye changamoto nyingi za maisha. Changamoto hizo ni pamoja na kuolewa, hivyo akiwa kwenye maisha ya ndoa kuna masuala ya kutoelewana na mwenzi wake, jambo linalosababisha kutengana, kwa hiyo inabidi awe mvumilivu. Kwa jamii ya Wachagga ilikuwa ni kawaida ya wanaume kuwaacha wake zao nyumbani kwao, kwa kipindi chote ambacho walikuwa nje kikazi au kibiashara. Mama anabeba majukumu yote, ya kuleya familia, kutunza mifugo, shughuli za kilimo na hata wakati mwingine kulea wazazi wa mwanaume. Ndiyo maana mwimbaji anasema, *Oh! Mmbede na kyenda kishamba* (Mngoje hata kama yuko mbali) akimwambia mtoto wa kike kwamba mwanaume amesafiri kwenda mbali. Mtoto huyu wa kike anasisitiziwa kwamba itabidi ajijue kuwa baba yake hayupo (*baba kwelele bo*), mama yake hayupo (*mayi kwelele bo*), kaka yake hayupo *(nsacha kwelele bo),* kwa hiyo ilimlazimu kujua kuwa yeye ndiye baba, ndiye mama, ndiye kaka, na yeye ndiye mwanaume. Ujumbe unaopatikana katika wimbo huu ni ujasiri, uvumilivu, mateso na ushirikiano. Jamii ya Wachagga ilikuwa na itikadi kwamba mtoto wa kike atakayelia kipindi cha kukeketwa, maisha ya ndoa yatamshinda.

Leo hii, kuendana na mabadiliko ya kijamii kuhusiana na suala la kuingiliana kwa tamaduni tofauti, mafundisho ya dini na masuala mtambuka, yamechangia kwa kiasi kikubwa kuathiri nyimbi za ngoma ya *Mbassa*, hususan katika utendaji wake, kimandhari, kihadhira na tukio linalotendeka. Wimbo wa *Oh! Kiona* bado unaimbwa katika jamii ya Wachagga kupitia miktadha mingine mbali ya muktadha wa unyago ambao zamani ulikuwa unatumika kuimbwa wimbo huu. Aidha, kutokana na hojaji na manju waliokuwa wametafutwa na mtafiti, walikiri kwamba wimbo huo kwa sasa unaimbwa kwenye

miktadha ya semina na makongamano mbalimbali. Maelezo hayo yanadhihirisha ukweli kutokana na kwamba lugha iliyotumika katika wimbo huu ni ya kawaida, ambayo kila mwanajamii wa Kichagga anaweza kuielewa. Pia maudhui ya wimbo huu yanashadidia hali halisi ya maisha kaika jamii ya Wachagga kwamba dhima ya uvumilivu, ujasiri na ushirikiano bado ni mambo muhimu. Maudhui hayo yakidhihirishwa na ukweli kwamba Mchagga anapoamua kufanya jambo liwe la kibiashara, kilimo au la kielimu, hakati tamaa mpaka aone mafanikio yake.

**4. IYOWE (NDIYO)**

| | |
|---|---|
| *Oh iyowee x2* | Oh ndiyo x2 |
| *Iyowee* | Ndiyo |
| *Oh yowe lee* | Oh ndiyo |
| *Yowee na likako yowee* | Ndiyo hata kama limezeeka ndiyo |
| *Lyandurumae x2* | Ni la zamani hizo x2 |
| *Yowee x2* | Ndiyo x2 |
| *Lya tata na nkeku* | La babu na bibi |
| *Iyowee na likakoo yowee* | Ndiyo hata kama limezeeka |
| *Ekato munae* | Huyo mtoto |
| *Iyowee* | Ndiyo |
| *Nyauka ko kekuyee* | Ametoka kwa bibi |
| *Iyowe na likakoo yowee* | Ndiyo hata kama limezeeka |
| *Ekato babae* | Huyo baba |
| *Iyowee* | Ndiyo |
| *Nyacha na mmbengee* | Anakuja kwa mbele |
| *Iyowe na likakoo yowe* | Ndiyo hata kama limezeeka |

**Chanzo: Manka Mushi miaka 39, tarehe 19/10/2012 Kijiji cha Umbwe, Tarafa ya Kibosho**

Wimbo huu unamwelezea mtoto wa kike ambaye anakabithiwa kwa wazazi wake wakati alipokuwa anatoka kukeketwa. Huu wimbo ni wa ngoma ya *Mbassa,* aliokuwa anaimbiwa mtoto wa kike mara alipokuwa anapokelewa nyumbani na wazazi wake akiwa ametokea kwa bibi anayekeketa (ngariba) katika muktadha wa unyago. Wimbo huu ulikuwa unampongeza binti aliyefanyiwa tohara kwamba alikuwa mvumilivu. Kwa namna

nyingine, wimbo huu pia ulikuwa unasisitiza kufanyika tohara kwa watoto wa kike. Kwa mfano mwimbaji alipokuwa anasema:

| | |
|---|---|
| *Yowe na likako yowe* | Ndiyo hata kama limezeeka ndiyo |
| *Lya tata na nkeku* | La babu na bibi |
| *Lya ndurumae* | Ni la zamani hizo |

Msaani alitumia neno *likako* akimaanisha tendo la tohara, na anaposema *lya tata na nkeku* anamaanisha kuwa tendo hilo lilikuwepo tangu zamani za mababu na mabibi. Kwa hiyo mtoto wa kike alipokuwa anaimbiwa, wimbo ulikuwa unamfundisha kwamba suala la mila hasa ya kukeketa ni la muhimu sana, hivyo tendo hilo la kukeketa likawa linapokezwa kizazi kimoja hadi kingine, kwa sasa tendo la kukeketwa halipo tena, na kama lipo jamii inafanya kwa usiri mkubwa sana.

.

Dhamira kuu katika wimbo huu ni mila na desturi. Ujumbe unaopatikana hapa ni suala la tohara kwamba ni muhimu. Itikadi ni kwamba hilo ni jambo lililokuwepo toka enzi za mababu na mabibi. Mtazamo na msimamo ni kwamba watoto wa kike ni lazima wafanyiwe tohara.

Kutokana na mabadiliko ya kimaendeleo ya kijamii, yanayoendana na masuala mtambuka, matumizi ya vyombo vya habari kama vile redio, magazeti, televisheni na mitandao ya kijamii, yamechangia kuathiri nyimbo za ngoma ya *Mbassa*, hususan katika uwasilishaji wake. Katika wimbo huu, unaathiriwa mandhari yake kutokana na kwamba mandhari yanayotumika kwa sasa hayako kwenye muktadha wa unyago. Hadhira inayoshiriki inabadilika, hata tukio nalo haliwi kama awali kwa sababu ya kubadilika kwa muktadha. Kwa mfano, mtafiti alihudhuria sherehe ya kidini iliyohusiana na kanisa Katoliki ambalo hufanya sherehe zinazojulikana kama sherehe za Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo (JNNK), washiriki waliuimba wimbo huu walipokuwa wanaendele na sherehe

zao huku wakiwa wanacheza na kuimba nyimbo mbalimbali. Fasihi inaeleza kuwa mila na desturi za jamii hubadilika kutokana na wakati pia na jamii yenyewe.

Katika jamii ya Wachagga, suala la kukeketa watoto wa kike halipo tena. Lakini jamii hii ina mila na desturi nyingi, zikiwemo za kuzaliwa mtoto, kumwoza binti na za mazishi. Kwa hiyo wimbo huu ambao maudhui yake ni usisitizaji wa mila na desturi, bado unasawiri katika jamii ya Wachagga kuendana na mila na desturi zilizopo kwa sasa.

### 5. EWE RUWA (EWE MUNGU)

| | |
|---|---|
| **Kiongozi:** *Ewe ruwa ewe ruwa*<br>*marikundee* | Ewe mungu ewe mungu<br>baba mpendwa |
| **Washiriki:** *Iya mama* | Eee mama |
| **Kiongozi:** *Luwaware ndani wedu cha*<br>*nyinyile* | Tumleye baba yetu kama<br>ndizi |
| **Washiriki**: *Iya mama ee yewoye*<br>*oh yewoye oh iyaa mama* | Eee mama ee<br>oh ndiyo oh ee mama |
| **Kiongozi:** *Ewe ruwa, ewe ruwa*<br>*Baba mkundee* | Ewe mungu ewe mungu<br>baba Mpendwa |
| **Washiriki:** *Iya mama* | Eee mama |
| **Kiongozi:** *Luwaware imi-wedu cha nyinyile*<br>*cha nyinyile* | Tumbembeleze mume wetu<br>kama ndizi |
| **Washiriki:** *Iya mama* | Eee mama |
| **Kiongozi:** *Chechekecha maramoja*<br>*Mmanye komanyo lee* | Cheza mara moja<br>nijue umekatwa |
| **Washiriki:** *Iya mama ee iyewoye*<br>*oh iyewoye, oh iya mama* | Eee mama ee ndiyo<br>Oh ndiyo oh eee mama |
| **Kiongozi**: *Ngiwiya mmbawarere*<br>*Mami lyako* cha *nyinyile* | Niambie nimbembeleze<br>Mkwe wangu kama ndizi |
| **Washriki:** *Iya mama ee iyewoye*<br>*Oh yewoye Oh iya mama* | Ee mama ee ndiyo<br>Oh ndiyo oh eee mama |

**Chanzo: Graceana Prosper Masawe miaka 48, tarehe 18/10/2012, kijiji cha mawaleni, Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo uliokuwa unaelezea namna ambavyo mwanamke alikuwa anawapenda wazazi wake, anawapenda wakwe zake, na alikuwa anajua kucheza. Wimbo huu ulikuwa unaimbwa wakati wa sherehe za kumtoa nje mwali aliyefanyiwa tohara katika muktadha wa unyago. Katika sherehe hizo za unyago, mchumba mtarajiwa wa binti aliyekeketwa

huwa anaalikwa. Wimbo huu unaimbwa kwa ajili ya kumkaribisha kijana anayechumbia aweze kutoa zawadi kwa huyo binti aliyekuwa amekeketwa. Zawadi hizo zilikuwa ni kitambaa cha kufutia jasho na kofia ambayo ilikuwa imepambwa na fedha za karatasi **(**noti**)**. Kipindi hicho noti ya shilingi mia ilikuwa ya rangi nyekundu na ilkuwa inajulikana kwa jina la noti ya Mmasai. Wakati binti alipokuwa anakabidhiwa hizo zawadi, kiongozi wa ngoma alikuwa anaimba: *Chechekecha nicha mmanye komanyo* akiwa anamwambia binti kuwa amchezee mchumba wake vizuri ili ajue kwamba amekeketwa. *Chechekecha* – ni mtindo wa binti kucheza kwa kuzunguka huku akiwa ameinama kidogo kwa kutazama ardhini. Kwa sababu kijana alikuwa anatoa fedha ilibidi amwone kama kweli alikuwa anajua kucheza. Dhamira kuu katika wimbo huu ni mahari na mapenzi. Ujumbe ulioko katika wimbo ni pamoja na utajiri, ndoa na heshima katika jamii. Itikadi ya jamii ya Wachagga ni kuona fahari mtoto wao anapotolewa mahari na kuolewa. Msimamo na mtizamo ni kwamba siku ya kuchezwa kwa mtoto wa kike ni lazima mchumba wake afike kwenye hiyo ngoma.

Mabadiliko ya kimaendeleo ya kijamii yanayohusiana na masuala ya uhabarishaji na elimu yameathiri kwa kiasi nyimbo za ngoma ya *Mbassa* katika uwasilishaji wake ikiwa ni pamoja na mandhari ya nyimbo hizo zinapoghaniwa, hadhira inayoshiriki katika kughani nyimbo hizo na tukio lenyewe. Pamoja na athari hizo, hazikuufanya wimbo huo kubadilika kimaudhui, kutokana na kwamba baadhi ya wahojiwa walieleza kuwa wimbo huo unaimbwa  katika miktadha mingine ikiwemo ya sherehe za Krisimas na Mwaka Mpya. Kipindi cha Siku Kuu, katika jamii Wachagga huwa na tabia ya kurudi makwao kwa ajili ya kusheherekea Siku Kuu hizo. Wimbo huu kwa kipindi hicho, maudhui yake yalilenga katika suala la utoaji mahari yaliyoambatana na ndoa. Katika jamii ya Wachagga bado sula la mahari lipo, na hususan mahari ambayo hutolewa kwa wazazi wa

mtoto wa kike. Kipindi hiki cha Siku Kuu za Krismasi na Mwaka Mpya, walio wengi katika jamii ya Wachagga, hutumia nafasi hiyo hiyo katika kuoa na kuolewa. Hii inadhihirisha wazi kwamba wimbo huu, maudhui yake bado yanasawiri katika jamii ya Wachagga.

### 6. MASANTULA (MASANTULA)

| | |
|---|---|
| **Kiongozi:** *Masantulae, Iyanseuri x2* | Masantulae, ndiyo |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Iyeolelee, Iyanseuri x2* | A haa, ndiyo |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Kakyo kyijanae, kyacha na nnko,* | Huyo kijana anakuja mbele |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Iyeolelee, Iyanseuri* | A haa, ndiyo |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Kakyo kijana kyire sutye,* | Huyo kijana amevaa suti |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Iyeolelee, Iyanseuri* | A haa, ndiyo |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Kayo sutye sutye mudoe,* | Hiyo suti suti nzuri |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi** *Iyeolelee, Iyanseuri* | A haa, ndiyo |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Kayo sutye nyalekobae,* | Hiyo suti amekopa |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Iyeolelee, Iyanseuri* | A haa, ndiyo |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Nyarye kyadu kyadu kyichae,* | Amevaa kiatu kiatu kizuri, |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Iyeolelee Iyanseuri* | A haa, ndiye |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Kakyo kyadu nyi ntumbae* | Kiatu chenyewe ni mtumba |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Iyeolelee, Iyanseuri* | A haa, ndiyo |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Kyikakuwesa mboni kyidae,* | Akikuuliza habari gani, |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Iyeolelee, Iyanseuri* | A haa, ndiyo |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Newe muni kwekundyee,* | wewe mwenyewe ulipenda, |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Iyeolelee, Iyanseuri* | A haa, ndiyo |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Kyikakuwesa ndifo kwedwee,* | Akakuambia twende kwetu, |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |
| **Kiongozi:** *Iyeolelee, Iyanseuri* | A haa, ndiyo |
| **Washiriki:** *Iyanseuri* | Ndiyo |

**Kiongozi:** *Newe muni kwekundyee,* wewe mwenyewe ulipenda,
**Washiriki:** *Iyanseuri* Ndiyo
**Kiongozi:** *Iyeolelee, Iyanseuri* A haa, ndiyo
**Washiriki:** *Iyanseuri* Ndiyo
**Kiongozi:** *Nyarye kyadu kyadu kyichae,* Amevaa kiatu kiatu kizuri,
**Washiriki:** *Iyanseuri* Ndiyo
**Kiongozi:** *Iyeolelee, Iyanseuri* A haa, ndiyo
**Washiriki:** *Iyanseuri* Ndiyo
**Kiongozi:** *Elyi kufika( kulyabokoke) x2* Utakapofika (Kwake) x2
**Washiriki:** *Iyanseuri* Ndiyo
**Kiongozi:** *Kakyo Kindamyi kirongonae,* Baba mkwe mlalamikaji
**Washiriki:** *Iyanseuri* Ndiyo
**Kiongozi:** *Iyeolelee Iyanseuri* A haa, ndiyo
**Washiriki:** *Iyanseuri* Ndiyo
**Kiongozi:** *Kakyo Kimamyi kimashushue,* Mama Mkwe msemaji
**Washiriki:** *Iyanseuri* Ndiyo
**Kiongozi:** *Iyeolelee, Iyanseuri x2* A haa, ndiyo x2
**Washiriki:** *Iyanseuri* Ndiyo
**Kiongozi:** *Kakyo kyitara kya massawoe,* Kitanda ni cha majani,
**Washiriki** *Iyanseuri* Ndiyo
**Kiongozi:** *Iyeolelee Iyanseuri* A haa, ndiyo
**Washiriki:** *Iyanseuri* Ndiyo
**Kiongozi:** *Kayona mmba mbari tyakitee* Nyumba ni mbavu za mbwa,
**Washiriki:** *Iyanseuri* Ndiyo
**Kiongozi:** *Iyeolele, Iyanseuri x2* A haa, ndiyo x2
**Washiriki:** *Iyanseuri x2* Ndiyo x2

**Chanzo: Mama Severa Mushi, miaka 49, tarehe 20/10/2012, Kijiji cha Kindi, Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo ambao unamwelezea kijana ambaye alikuwa ameenda kuchumbia, lakini hali yake ilikuwa hohe hahe. Masantula ni baba wa binti aliyekuwa anachumbiwa, anaelezwa kwamba kijana aliyefika kumchumbia binti yake hakuwa na uwezo, lakini yeye binti alimpenda na akaamua kuolewa naye. Wimbo huu wa ngoma ya *Mbassa,* ulikuwa unaimbwa kipindi binti aliyefanyiwa tohara anatolewa nje katika muktadha wa unyago. Katika jamii ya Wachagga, baada ya binti kufanyiwa tohara hatua iliyofuata ni kuolewa. Katika kuolewa kwa binti wa Kichagga alielezwa kwamba ni lazima aolewe na kijana mtanashati, aliyekuwa na uwezo wa kifedha na ambaye alitokea katika familia ya kitajiri. Msanii anasema, *Kakyo kyijanae kyacha na nnkoe* akimaanisha kijana mtanashati ambaye alikuwa amevaa suti akiwa anatembea kwa majigambo. Lakini suti yenyewe alikuwa

amekopa (*kayo sutye nyalekobae*), kiatu kilikuwa cha mtumba (*kakyo kyiadu nyi ntumba)*. Binti alikuwa anaelezwa mengi kuhusiana na baba mkwe kwamba alikuwa mnung'unikaji (*Kakyo kindamyi kirongonae*), mama mkwe alikuwa mmbeya (*kakyo kimamyi kimashushu*), kitanda cha kijana kilikuwa cha majani (*Kakyo kyitara kya masawoe*) na nyumba ya kijana ilkuwa ni ya mbavu za mbwa (*Kayo mmba mbari tya kite*). Lakini pamoja na sifa zote hizo mbaya, mtoto huyo wa kike aliamua kuolewa naye. Dhamira kuu katika huu wimbo ni suala la mapenzi ya dhati. Ujumbe ambao uko katika wimbo huu ni umasikini na udhalilishaji. Mtazamo na msimamo wa jamii ya Wachagga, ulikuwa ni lazima binti yao aolewe na kijana aliyekuwa na uwezo wa kifedha, hususan familia tajiri.

Kufuatia mabadiliko ya kimaendeleo ya kijamii, hususan katika dini, mwingiliano wa tamaduni ndani ya jamii na masuala mtambuka, kimuktadha nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zimeathiriwa katika uwasilishaji wake kuhusiana na vipengele vya mandhari, hadhira, fanani na tukio lenyewe. Mandhari ambayo yanatumika kuimbia nyimbo hizi kwa sasa, ni katika muktadha wa harusi, tofauti kabisa na mandhari ya hapo awali (muktadha wa unyago). Hadhira iliyoimba nyimbo hizi katika muktadha wa unyago, ilikuwa ni ndugu ndani ya jamii ya Wachagga tu. Lakini leo hii nyimbo hizi zinapoimbwa katika miktadha mingine kunakuwa na jamii zingine mbali ya Wachagga. Tukio lililolengwa kuhusiana na nyimbo hizo lilikuwa ni unyago, laakini leo hii halipo. Kwa hiyo nyimbo hizi zinaimbwa katika miktadha mingine mbali ya unyago. Mviga wa unyago ulikuwa unaambatana na ngoma ya *Mbassa*, kwa hiyo inaonesha katika jamii ya Wachagga, hususan Tarafa ya Kibosho, unyago umefutika kwa sababu hakuna mafunzo mengine ambayo yanatolewa mbadala wa unyago.

Kwa kuwa nyimbo hizi zilikuwa na lengo la kuburudisha na kuelimisha jamiii, bado wimbo huu wa *Masantula* unasawiri jamii ya Wachagga kuendana na maudhui yaliyomo ndani ya wimbo huo, ambayo ni kuhusiana na suala la mapenzi ya dhati. Dhamira hii inajidhihirisha wazi ndani ya jamii hiyo kutokana na kwamba ni mara chache sana kwa mabinti wa Kichagga walioolewa kuachana na waume zao. Jambo hili linathibitishwa na wimbo wa *Masantula*, pale msichana anapoonesha kumpenda mwanaume (mchumba) aliyemchagua, pamoja na kuelezwa sifa mbaya za kijana mwenyewe, na za wazazi wa huyo kijana wa kiume.

### 7. EKANGICHECHEKA (CHEZA CHEZA)

| | |
|---|---|
| *Ekangichecheka ngichecheka* | Cheza cheza, tucheze |
| *Baba lyakoe* | Baba yangu |
| *Orakilewoe oyayewoyee,* | Ndugu yangu, haya haya |
| *Ekangichecheka* | Chezacheza |
| *Ngichecheka* | Tucheze |
| *Ekangichecheka ngichecheka* | Cheza cheza tucheze |
| *Kinyali sawoyee,* | Kinyali babu yake |
| *Orakilewoe oyayewoyee,* | Ndugu yangu, haya haya |
| *Ekangichecheka* | Chezacheza |
| *Ngichecheka* | Tucheze |
| *Ekangichecheka ngichecheka,* | Chezacheza tucheze |
| *Mayi woko* | Mama yangu |
| *Orakilewoeoyayewoyee,* | Ndugu yangu, haya haya |
| *Ekangichecheka* | Chezacheza |
| *Ngichecheka* | Tucheze |
| *Ekangichyeka ngichecheka* | Cheza cheza tucheze |
| *Wandaasa wokoe* | Jirani yangu |
| *Orakilewoe oyayewoyee,* | Ndugu yangu haya haya |
| *Ekangichecheka* | Cheza cheza |
| *Ngichecheka* | Tucheze |
| *Ekangichecheka ngicheche* | Cheza cheza tucheze |
| *Nsacha wedue* | Kaka yetu |
| *Orakilewoe oyayewoyee,* | Ndugu yangu haya haya |
| *Ngichecheka* | Tucheze |
| *Ekangichecheka ngichecheka* | Cheza cheza tucheze |
| *Mwichi weduee* | Mshenga wetu |
| *Orakilewoe oyayewoyee,* | Ndugu yangu haya haya |
| *Ekangichecheka ekangichecheka* | Cheza cheza tucheze |
| *Mushi wedue* | Mushi wetu |
| *Orakilewoe oyayewoyee,* | Ndugu yangu haya haya |
| *Ekangichecheka* | Cheza cheza |
| *Ngichecheka* | Tucheze |
| *Ekangichecheka ngichecheka* | Cheza cheza tucheze |

| | |
|---|---|
| *Wana wedue* | watoto wetu |
| *Orakilewoe oyayewoyee,* | Ndugu yangu haya haya |
| *Ekangichecheka ngichecheka* | Cheza cheza tucheze |
| *Ngichecheka* | Tucheze |

**Chanzo: Mama Elizabeth Minja, miaka 68, tarehe 18/10/2012 Kijiji cha Msasani, Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo wa Kichagga, uliokuwa unaimbwa kwa kuwakaribisha wageni walioalikwa kwenye sherehe za kumtoa mwali aliyekeketwa nje. Wimbo huu ni wa ngoma ya *Mbassa* ambao ulikuwa unaimbwa siku ya kutolewa nje mwali aliyekeketwa katika muktadha wa unyago. Katika jamii ya Wachagga, siku ya kutolewa nje mtoto wa kike aliyekeketwa, kulikuwa na watu muhimu ambao hawakutakiwa kukosekana katika hafla hiyo. Watu hao ni baba, mama, kaka, babu na majirani wote walialikwa hata kama hawakuwa na chochote cha kumzawadia mtoto aliyekeketwa. Kwa hiyo mtoto wa kike alifundishwa kwamba amefikia umri wa utu uzima, hivyo anaruhusiwa kuchangamana na hao watu. Pia wimbo huu ulimfundisha kuwa na heshima na ukarimu wa kuwapokea wageni pindi atakapoolewa.

Kufuatia mabadiliko ya kimaendeleo ya kijamii ya kuacha na kukataa ukeketaji, na ambapo yanachangiwa na elimu ya jamii kupita vyombo vya habari kama vile magazeti, redio, televisheni na mitandao ya kijamii, imesadia jamii ya Wachagga kuachana na tendo la ukeketaji wa watoto wa kike kama mila potofu, imefanya nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ambazo zilikuwa zinaghaniwa katika unyago kuathirika katika uwasilishaji wake kwenye vipengele vya hadhira, mandhari na tukio linalotendeka.

Mandhari ambayo wimbo huu unaimbiwa (muktadha wa sasa) ni tofauti na ulivyokuwa unaimbwa katika muktadha wa unyago. Athari hizi za mabadiliko, zinaenda sambamba na

hadhira pamoja na tukio lenyewe. Pamoja na athari hizo bado wimbo huu umeonekana kusawiri katika jamii, hususani jamii ya Wachagga kutokana na maudhui yake. Wimbo huu ulimsisitiza mtoto wa kike kuwa na heshima na ukarimu katika jamii. Leo hii, katika jamii ya Wachagga, msisitizo huo umepitiliza kutokana na kwamba wimbo unawasisitizia watoto, wazazi, wazee na majirani kuwa na heshima na ukarimu. Ukweli huu unajidhihirisha katika mstari wa pili, wa saba, wa kumi na mbili, wa kumi na saba, wa ishirini na mbili na wa thelathini na nne katika wimbo huu. Hivyo ni dhahiri kuwa maudhui ya wimbo bado yanasawiri uhalisi wa maisha katika jamii ya Wachagga.

### 8. SAURI (SAURI)

| | |
|---|---|
| *Sauri Saurie* | Sauri Sauri |
| *Sauri nsacha-ko* | Sauri kaka yangu |
| *Elikulembedino* | Mbona ulikwisha tahiriwa |
| *Kololya nsa kiwawa* | Ukaona kinavyouma |
| *Oh! Ngashae ngash a ngakuta* | Oh! nikaungua nikaungua nikakimbia |
| *Sauri Sauri* | Sauri Sauri |
| *Sauri nsacha-ko* | Sauri kaka yangu |
| *Eli kulembedino* | Mbona ulikwisha tahiriwa |
| *Kololya nsa kiwawa* | Ukaona kinavyouma |
| *Oh! Ngashae ngasha ngakuta* | Oh! nikaungua nikaungua nikakimbia |

**Chanzo: Mama Severa Mushi, miaka 49, tarehe 20/10/2013 Kijiji cha Kindi, Tarafa ya Kibosho**

Wimbo wa Sauri ni wa ngoma ya *Mbassa*, ambao unaimbwa na jamii ya Wachagga, hususan kipindi cha mwali (mtoto aliyekeketwa) anapotolewa nje. Kwa kawaida, jamii ya Wachagga ilikuwa na desturi ya kumweka ndani mtoto wa kike aliyefanyiwa tohara kwa kipindi cha mwezi mmoja hadi miwili bila kutoka nje. Akiwa ndani hulishwa vyakula vya

kienyeji kama vile *mmso* (uji wa ulezi), *mtori* (chakula mchanganyiko wa nyama na ndizi) na *usawo* (chakula mchanganyiko wa damu na maziwa). Siku ya mwali kutolewa nje, hufanyika sherehe kubwa inayoambatana na unywaji wa pombe ya kienyeji (mbege). Katika sherehe hiyo, hualikwa wanaume kwa wanawake na kuimbwa nyimbo mbalimbali za ngoma ya *Mbassa.* Wimbo wa Sauri ni moja ya nyimbo ambazo zinaimbwa. Kwa mfano, msanii anaposema:

| | |
|---|---|
| *Sauri Sauri* | Sauri Sauri |
| *Sauri nsacha-ko* | Sauri Kaka Yangu |
| *Elikulembedino* | Mbona ulikwisha tahiriwa |
| *Kololya nsa kiwawa* | Ukaona kinavyouma |

Sauri ni mtu mmoja anayewasilisha jamii ya wanaume. Hivyo wanaume wanapewa ujumbe kwamba wasishangae tendo la tohara kwa sababu nao pia walikwisha tahiriwa. Neno *kiwawa* (kinauma) katika wimbo huo linawakilisha sehemu ya mwili inayotolewa wakati wa kufanyika kwa tendo la tohara. Kwa wanawake inamaanisha kinembe, na kwa wanaume inamaanisha govi. Uondoaji wa sehemu hii ya mwili ilikuwa inafanyika bila ganzi. Wimbo huu ulikuwa unamweleza mtoto wa kike kuwa mvumilivu kipindi chote cha maisha yake, kufuatia chngamoto mbalimbali za maisha, ndiyo maana msanii anasema, *Oh! ngashae ngasha ngakuta* (Oh! nikaungua nikaungua nikakimbia). Kwa hiyo mtoto wa kike anaelezwa kwamba asiyakimbie matatizo.

Dhamira kuu ya wimbo huu ni uvumilivu. Ujumbe wa wimbo huu kwa jamii ni kwamba hakuna kitu au jambo litakalopatikana kwa njia rahisi au ya mkato, bali upatikanaji wake ni kwa njia ya maumivu, mateso na madhara. Jamii ya Wachagga waliamini kuwa njia pekee ya kufundisha uvumilivu ni kufanya tohara kwa watoto wao. Mtazamo na msimamo unaopatikana katika wimbo huu ni mtoto wa kike kushindwa kukabiliana na changamoto za maisha iwapo hatafanyiwa tohara.

Aidha kutokana na mabadiliko yaliyoko katika jamii, kupitia semina zinazotolewa na asasi zisizo za kiserikali, vyombo vya habari kama vile redio, magazeti, televisheni na mitandao ya kijamii, sasa hivi tohara kwa watoto wa kike katika jamii ya Kichagga haifanyiki tena. Kutokana na kutokuimbwa nyimbo hizi katika muktadha wa unyago, nyimbo hizi zimeathiriwa katika vipengele vya mandhari, hadhira, fanani pamoja na tukio linalotendeka. Kwa sasa wimbo huu unaimbwa katika muktadha wa harusi, dhima kubwa ikiwa ni kusisitiza uvumilivu katika maisha ya ndoa. Jambo hili linajidhihirisha kwenye jamii ya Wachagga, hususan ndoa zilizofanyika kwa kufuata mila na desturi, zilikuwa kufarakana kwake ni mara chache sana. Hivyo inaonesha ni kwa namna gani wimbo huu unavyosawiri maisha ya sasa katika jamii ya Wachagga.

### 9. NNKA NNARUMU (MKE WA NARUMU)

| | |
|---|---|
| **Kiongozi:** *Nka Nnarumu nyentondo* | Mke wa Narunu mjinga |
| **Wasiriki:** *Aaa oo yaye* | Aaa woyee |
| **Kiongozi:** *Kakumba muna kaura nkate* | Aliuza mtoto kanunua mkate |
| **Wasiriki:** *Aaa oo yaye* | Aaa woyee |
| **Kiongozi:** *Oo ngamba nka Nnarumu nyentondo* | Oh! nasema mke wa Narumu mjinga |
| **Washiriki:** *Aaa oo yaye* | Aaa woyee |
| **Kiongozi:** *Kakumba muna kaura nkate* | Aliuza mtoto kanunua mkate |
| **Wasiriki:** *Aaa oo yaye* | Aaa woyee |

**Chanzo: Manka Mushi, miaka 39, tarehe 19/10/2012, Kijiji cha Umbwe, Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo wa ngoma ya *Mbassa* ambao unamwelezea mwanamke fulani aliyekuwa anatoka sehemu inayoitwa Narumu. Jamii iliyokuwa inaishi sehemu hiyo ilikuwa nyuma kimaendeleo, hususan katika suala la elimu.

Massawe (1995:9) anasema:

| KIMACHAME | KISWAHILI |
|---|---|
| **Nsongoru:** *Nkaa Kinasha nyiishamiri,* | **Kiongozi:** Mke wa Kinasha ni mpumbavu |
| **Veembi:** *Nkaa Kinasha nyiisamiri,* | **Kiitikio:** Mke wa Kinasha ni mpumbavuu |
| **Nsongoru:** *Nkaa Kinasha nyushi kindo-fo* | **Kiongozi:** Mke wa Kinasha hajui kitu |
| **Veembi:** *Nkaa Kinasha nyisamiri x4* | **Kiitikio:** Mke wa Kinasha ni mpumbavu x4 |

**Chanzo: Massawe (1995)**

Mwandishi anamwelezea mwanamke ambaye mume wake alikua anaitwa Kinasha, akieleza namna mwanamke huyo alivyokuwa mpumbavu na kuonekana kutokuwa na mchango katika jamii. Wimbo huu ulikuwa unaimbwa kwenye sherehe za unyago.

Katika jamii ya Wachagga, hususan jamii ya Wanarumu, kukosekana kwa elimu, kuliwaingiza kwenye masuala ya ushirikina. Wimbo wa *Nnka Nnarumu* (Mke wa Narumu), ulikuwa unaimbwa siku ya kutolewa nje mwali (mtoto aliyefanyiwa tohara), akielezwa kwamba atakapokuwa na familia akumbuke kuwapatia elimu watoto wake. Elimu ndiyo njia pekee ya kuwakomboa katika umasikini. Kwa mfano, msanii anasema:

| | |
|---|---|
| **Kiongozi**: *Nnka Nnarumu nyentondo* | Mke wa Narumu mjinga |
| **Washiriki**: *Aaa oo yaye* | Aaa woyee |
| **Kiongozi:** *Kakumba muna kaura nkate* | Aliuza mtoto kanunua mkate |

Fundisho la kwanza linalotokana na maneno hayo ya msanii, mtoto wa kike anaaswa kuwa mwangalifu katika usichana wake. Akiwa mjinga atauza mtoto na kununua mkate. Neno *muna* (mtoto) limetumika kama lugha ya mficho likiwa na maana ya sehemu yake ya uke, na *nkate* (mkate) limetumika kuwakilisha mimba. Kwa hiyo mtoto wa kike anafundishwa kwamba akiwa mjinga akafanya mapenzi kabla ya kuolewa, atapata mimba na hatapata mtu wa kumwoa tena, katika jamii ya Wachagga, mtoto wa kike aliyepata mimba kabla ya ndoa, alikuwa haolewi tena. Fundisho la pili ni kwamba mtoto wa kike

atakapobahatika kuwa na familia yake, anatakiwa kuhakikisha kwamba watoto wanaandikishwa shule. Katika maana hii ya pili, neno *muna* (mtoto) limetumika kama elimu na nkate (mkate) limetumika kama kitu cha muda mfupi, ingawaje ni kitamu. Kwa hiyo mtoto wa kike anaelezwa kwamba asipompatia mtoto wake eleimu, akapenda starehe na anasa, baadaye atajutia. Dhamira kuu ya wimbo huu ni kuondoa ujunga. Jamii ya Wachagga ilithamini sana suala la kupeleka mtoto shule. Hadi sasa dhamira hii inasawiri kwa sababu kipaumbele kwa watoto wa jamii ya Wachagga ni elimu, na walau kiwango cha chini  ni elimu ya sekondari. Kwa kipindi hiki wimbo huu unapoimbwa, mathalani kwenye muktadha wa siasa, bado maudhui yake yanashadidia na kusawiri ndani ya jamii kwa sababu, walau kila kata katika Tarafa ya Kibosho kumejengwa sekondari. Kwa msingi huo, jamii imepata mwamko mkubwa katika kuelimisha watoto wa kike, jambo ambalo hapo awali mtoto wa kike alikuwa hatiliwi maanani katika suala la elimu, badala yake mtoto wa kiume ndiye aliyepewa nafasi kubwa ya kusoma. Kwa hiyo, dhima kubwa ya wimbo huu ni kueleza hasara, anasa na kudanganywa, mambo ambayo yanachangia kurudisha nyuma maendeleo ya jamii. kwa hiyo msisitizo ni kumpeleka mtoto shule ili kuleta maendeleo.

### 9. MMBERE (NDUGU)

| | |
|---|---|
| **Kiongozi:** *Ee mberee* | Eee ndugu |
| **Washiriki:** *Nsangati* | mbali |
| **Kiongozi:** *Babafo nyindu lengane* | Baba yako mtu mkubwa |
| **Washiriki:** *Nsangati* | Mbali |
| **Kiongozi***: Ee mmberee* | Eee ndugu |
| **Washiriki:** *Nsangati* | Mbali |
| **Kiongozi:** *Nsacha nyindu lengane, mberea sindee* | Kaka yako mtu mkubwa |
| **Washiriki:** *Nsangaati* | Mbali |
| **Kiongozi:** *Mmbera sindee* | Mbali chini |

| | |
|---|---|
| **Washiriki:** *Nsangati* | Mbali |
| **Kiongozi:** *Ee ee* | Ee ee |
| **Washiriki:** *Nsangati* | Mbali |
| **Kiongozi:** *Mmbera sinde* | Ndugu chini |
| **Washiriki:** *Nsangati* | Mbali |

**Chanzo: Benedicta Z. Jacob, miaka 97, tarehe 17/10/2012, Kijiji cha Kindi, Tarafa ya Kibosho.**

Wimbo huu ni wa ngoma ya *Mbassa* ambao uliimbwa kwenye muktadha wa unyago katika jamii ya Wachagga. Wimbo huu unaelezea jamii fulani iliyokuwa na maisha bora, kwa sasa inalalamika jinsi ambavyo maisha yamekuwa na changamoto nyingi zikiwemo za uzazi wa mpango, ambazo wanashindwa kukabiliana nazo. Kwa mfano, msanii anaposema:

| | |
|---|---|
| **Kiongozi**: *Ee mbere* | Ee ndugu |
| **Washiriki:** *Nsagati* | Mbali |
| **Kiongozi**: *Babafo nyindu lengane* | Baba yako mtu mkubwa |
| **Washiriki**: *Nsangati* | Mbali |
| **Kiongozi:** *Nscha nyindu lengane, mberea sinde* | Kaka yako mtu mkubwa |

Kwa maneno hayo hapo juu, msanii anamwelezea mtoto wa kike kwamba awe mwnagalifu katika masuala ya uzazi. Asiweke mategemeo kwa ndugu zake, kujigamba kwamba watamtunzia watoto. *Babafo nyindu lengane* (Baba yako mtu mkubwa), *Nsacha nyindu lengane mberea sinde (*Kaka mtu mkubwa ndugu chini). Maneno hayo yote yanamwasa mtoto wa kike kutotegemea ndugu. Wimbo huu unapoimbwa katika muktadha wa dini na siasa bado unasawiri maisha ya jamii. kwa upande wa siasa unawaasa wanasiasa kutengeneza sera zao wenyewe, na kwa upande wa dini, kila waamini wanaaswa kusimama katika imani waliyo nayo wasidhani kuna dini ambayo itawafikisha kwenye ufalme wa mbinguni. Maudhui makubwa ya wimbo huu ni

kujitegemea. Ujumbe ni mazingira magumu, utegemezi na kulalamika. Mtazamo na msimamo ni kuhakikisha kwamba kila mtu anakuwa na mawazo yake mwenyewe ya kujitegemea kiuchumi, kisiasa na kiimani.

**10. MMBANGA (PANGA)**

| | |
|---|---|
| **Kiongozi:** *O-banga longimanya mmbanga* | Oh! panga limenikata |
| **Wasshiriki:** *Ewo mmbanga* | Wewe panga |
| **Kiongozi:** *O-mbanga longimanya matawi mbanga* | Oh! panga la kukata matawi. |
| **Washiriki:** *Ewo mmbanga* | Wewe panga |
| **Kiongozi:** *Matawi nya karoti mmbanga* | Matawi ya karoti panga |
| **Wshiriki:** *Ewo mmbanga* | Wewe panga |
| **Kiongozi***: O mbanga eee* | Oh! panga ee |
| **Washiriki:** *Ewo mmbanga* | Wewe panga |

**Chanzo: Coletha H. Tarimo, miaka 44, tarehe 18/10/2012, Kijiji cha Mango, Tarafa ya Kibosho**

Wimbo huu ni wa ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga, wanaoishi Tarafa ya Kibosho. Wimbo huu ulikuwa unaimbwa siku ya kufanyiwa tohara mtoto wa kike katika muktadha wa unyago. Ilikuwa ni desturi kwa jamii ya Wachagga, hususan Wakibosho kuimba nyimbo chache siku ya kufanyiwa tohara mtoto wa kike. Katika kuimbwa kwa wimbo huu, kulikuwa na tafsiri mbili. Tafsiri ya kwanza, mmbanga (panga) ilimaanisha uume wa mwanaume. Tafsiri ya pili, mmbanga (panga) ilimaanisha chombo kilichokuwa kinatumika katika kufanya tendo la tohara. Kwa mfano, msanii anaposema, *o-mmbanga longimanya matawi mmbanga* (Oh! panga limekata matawi) na *matawi nya karoti mmbanga* (matawi ni ya karoti), tafsiri yake ni kwamba mtoto wa kike amebikiriwa na mwanaume. Lakini pamoja na tafsiri hizo, wimbo huu maudhui yake ni maumivu ya tohara au wakati wa kufanya tendo la ndoa kwa mtoto wa kike kwa mara ya kwanza.

Ujumbe ni kwamba hakuna jambo lolote linaloweza kutendeka kiurahisi bila maumivu. Mtazamo na msimamo ni kuhakikisha kwamba kila mtu afanye kazi kwa bidii na hakuna kukata tama ya maisha. Wimbo huu inapoimbwa katika muktadha wa kidini, hususan kwenye harusi, maudhui yake yanasawiri jamii ya sasa, lakini unakuwa umeathiriwa katika utendaji wake ukizingatia vipengele vya mandhari, fanani, hadhira na tukio linalotendeka.

### 4.2.2 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Lengo la Pili

Lengo la pili ni kuchunguza na kubaini athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa*. Lengo linawasilishwa na baadhi ya nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ambazo zilikusanywa na mtafiti kutoka katika eneo la utafiti. Eneo la utafiti lilikuwa mkoa wa Kilimanjaro, wilaya ya Moshi Vijijini, Tarafa ya Kibosho. Sababu za kufanya utafiti katika eneo hili ni kwamba mada ya utafiti ililenga nyimbo za ngoma ya *Mbassa* na ambazo zinapatikana katika jamii hiyo ya Wachagga wa Kibosho. Uchambuzi wake unahusisha dhana ya kimuktadha na dhana ya kimaudhui katika nyimbo zifuatazo:

1. **UKIWA REREYE (SHIDA NYINGI)**

| | |
|---|---|
| *Ukiwa rereyee* | Shida nyingi |
| *Ukiwa lofo na lokoe* | Shida ni kwako na kwangu |
| *Ukiwa rereyee* | Shida nyingi |
| *Ndewiya kuda baba munae* | Nitamwambia nini baba yako |
| *Ukiwa rereyee* | Shida nyingi |
| *Ndewiya kuda mayi munae* | Nitamwambia nini mama yako |
| *Ukiwa rereyee* | Shida nyingi |
| *Ndewiya kuda wasachae* | Nitawaambia nini kaka |
| *Ndewiya kuda wandasae* | Nitamwambia nini jirani |
| *Ukiwa rereyee* | Shida nyingi |
| *Ukiwa lofo na lokoe* | Shida ni kwako na kwangu |
| *Ukiwa rereyee* | Shida nyingi |

**Chanzo: Elizabeth Minja miaka miaka 68, tarehe 27/8/2012 Kijiji cha Msasani, Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo wa ngoma ya *Mbassa* ambao ulikuwa unaimbwa katika muktadha wa unyago. Wimbo huu unaelezea masikitiko, huzuni na taabu zilizoko kwenye jamii. Aidha, msanii anaeleza kuwa wimbo huo ulikuwa unaimbwa kuonesha masaibu yaliyoikumba jamii ikiwa ni pamoja na magonjwa ya surua, kifaduro na ndui, ambayo yalisababisha vifo vingi vya watoto wadogo walikuwa tegemeo la jamii kwa siku za baadaye.

Wimbo huu unapoimbwa kwenye jamii ya sasa kupitia miktadha mingine, unasawiri na kuendana na jamii iliyopo sasa kwa sababu katika kipindi hiki kuna majanga ambayo yanafanana na ya wakati huo. Majanga hayo ni pamoja na magonjwa ya UKIMWI na Malaria, ambayo yameonekana kusababisha vifo vingi katika jamii. Lugha iliyotumika katika wimbo huu ni ya Kichagga, ambayo kwa jamii ya Kichagga, hususan jamii ya Wakibosho siyo ngumu kwao. Kwa hiyo, wimbo huu unapoimbwa unashadidia hali halisi ya maisha katika jamii hiyo, na hata unavuka nje ya mipaka ya jamii ya Wachagga kwa sababu magonjwa hayo siyo kwamba yako katika jamii ya Wachagga tu. Kwa mfano, msanii anaposema *ukiwa rereyee* (shida nyingi), *ukiwa lofo na lokoe* (shida ni kwako na kwangu), anaonesha ni kwa namna shida zilizomo ndani ya jamii zinazohusiana na masuala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kipindi hiki ni kipindi ambacho taifa linaingia gaharama kubwa katika kutafuta dawa za kurefusha maisha kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI. Nguvu kazi ambayo ni vijana inapungua kutokana na UKIMWI unaosababisha vifo vingi kwa vijana.

## 2. MMBI ALEBALYA BIRO (NANI ALIYEMGUSA BIRO)

| | |
|---|---|
| **Kiongozi:** *Oh! Mmbi alebalya Biro* | Oh! Nani aliyemgusa Biro |
| *nyama tikawa kali* | nyama zikapanada bei |
| **Washiriki:** *Eee ewoyayee majira* | Ee haya ndiyo majira |
| **Kiongozi:** *Oh! Mmbode baba-lyako* | Oh! Ninaye baba yangu |
| *nki nsara fo sario* | sina wasiwasi |
| **Washiriki:** *Eee ewoyaye majira* | Ee haya ndiyo majira |
| **Kiongozi:** *Oh! Mmbode nsacha wokoo* | Oh! Ninaye kaka yangu |
| *Nki nsara fo sario* | sina wasiwasi |
| **Washiriki:** *Eee ewoyayee majira* | Eee haya ndiyo majira |
| **Kiongozi:** *Oh! Mmbode mayi woko* | Oh! Ninaye mama yangu |
| *nki nsara fo sario* | sina wasiwasi |
| **Washiriki:** *Eee ewoywayee majira* | Eee haya ndiyo majira |
| **Kiongozi:** *Oh! Mmbode sawoako* | Oh! Ninaye babu yangu |
| *nki nsara fo sari* | sina wasiwasi |
| **Washiriki:** *Eee ewoyayee majira* | Eee haya ndiyo majira |
| **Kiongozi:** *Oh! Ngapindo majirae* | Oh! Ninacheza |
| *nka na mmi wakunde* | mme na mke wafurahi |
| **Washiriki:** *Eee ewoyayee majira* | Eee haya ndiyo majira |
| **Kiongozi:** *Ewe baba Mushie* | Wewe baba Mushi |
| *Kafo na wanaa* | ahsante sana |
| **Washiriki:** *Eee ewoyayee majira* | Eee haya ndiyo majira. |

**Chanzo: Maria Ngadoru miaka 65, tarehe 27/8/2012 Kijiji cha Kindi, Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo wa Kichagga ambao ulikuwa unaimbwa katika muktadha wa unyago, ukiwa unaelezea hali ya uchumi katika jamii ya Wachagga. Msanii anaelezea suala la kupanda bei ya nyama. Nyama ni kitoweo ambacho kilipendwa sana na jamii ya

Wachagga. Msanii alikuwa anaelezea hali ya maisha ilivyokuwa, hususan kipindi cha wahujumu uchumi. Katika miaka ya themanini, vitu kama sukari, sabuni na mafuta, viliadimika vikawa havipatikani kwa urahisi, labda kwa njia ya ulanguzi. Ndiyo maana kipindi hicho kukatokea usemi wa "kupitia mlango wa nyuma". Wimbo huu unapoimbwa katika muktadha wa sasa, unasawiri hali halisi ya maisha katika jamii kutokana na kwamba ni kipindi ambacho kimeghubikwa na masuala ya ufisadi, rushwa na ubadhilifu. Mambo haya yamesababisha jamii kuwa na hali ngumu ya maisha. Kwa mfano, hivi sasa ili kupata haki ya msingi inayohusiana na matibabu na huduma nyingine za kijamii kama vile maji na umeme, inalazimu kutoa rushwa ili uweze kuhudumiwa. Kwa kuwa wimbo huu umetumia lugha rahisi inayoeleweka na jamii ya Wachagga, ni wazi kwamba mambo ambayo yalizungumzwa na msanii kupitia wimbo huu kwa kipindi hicho, leo hii mambo hayo yanasawiri katika jamii lakini kwa mtindo mwingine.

### 3. SIRYA MMBA (FUNGA NYUMBA)

| | |
|---|---|
| **Kiongozi:** *Sirya mmba-yo woyaye* | Funga nyumba yako |
| **Washiriki:** *Sirya mmbaa-yo woyaye* | Funga nyumba yako |
| **Kiongozi:** *Ngadangilacha* | Nisipokuja |
| *Kinange kyalya* | soko limekula |
| **Washiriki:** *Sirya mmba-yo woyaye* | Funga nyumba yako |
| **Kiongozi:** *Sirya mmba-yo* | Funga nyumba |
| *Na muni-we kumbi* | Kwa mpini wa jembe |
| **Washiriki:** *Sirya mmba-yo woyaye* | Funga nyumba yako |
| **Kingozi:** *Sirya mmba-yo na muni-wo kyara* | Funga nyumba |
| *Na muni-we kyara* | Kwa mpini wa shoka |
| **Washiriki:** *Sirya mmba-yo woyaye* | Funga nyumba yako |
| **Kiongozi:** *Sirya mmba-yo woyaye* | Funga nyumba yako |
| **Washiriki:** *Sirya mmba-yo woyaye* | Funga nyumba yako |
| **Kiongozi:** *Ngadangilacha* | Nisipokuja |
| *Kideko kyalya* | Kideko kimenila |

| | |
|---|---|
| **Washiriki:** *Sirya mmba-yo woyaye* | Funga nyumba yako |
| **Kiongozi:** *Ngininga kitenge* | Nipe kitenge |
| *Ngikushike nakyo* | nijifunike |
| **Washiriki**: *Sirya mmba-yo woyaye* | Funga nyumba yako |
| **Kiongozi:** *Ngadangilacha* | Nisipokuja |
| *Pati ngilele* | nimelala kwenye pati |
| **Washiriki:** *Sirya mmba-yo woyaye* | Funga nyumba yako |
| **Kiongozi:** *Siya mmba-yo woyaye* | Funga nyumba yako |
| **Washiriki:** Sirya mmba-yo woyaye | Funga nyumba yako |

**Chanzo: Maria Ngadoru miaka65, tarehe 20/8/2012, Kijiji cha Kindi, Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo wa Kichagga ambao ulikuwa unamwelezea mtoto wa kike aliyekuwa na tabia ya kumtoroka mama yake na kwenda kwenye starehe za usiku (disko).

Bakari (2012) anasema, baadhi ya watoto ambao hawajalelewa na wazazi wao, huwa na tabia ya kutoka toka usiku na kwenda katika kumbi za starehe au kuangalia video.

Katika jamii ya Wachagga, ilikuwa ni marufuku kwa mtoto wa kike kuwa nje ya mazingira ya nyumbani, hususan nyakati za usiku. Wimbo wa *Sirya mmba* (Funga mlango) ni wa ngoma ya Mbassa ambao ulikuwa unaimbwa kwenye muktadha wa unyago.

Wimbo huu unapoimbwa katika miktadha ya sasa ikiwemo harusi, sherehe za kidini Krismas na Mwaka Mpya, unaeleza hali halisi ya maisha ya vijana wa sasa. Kufuatia suala la vijana wengi kutoka kijijini kwenda mjini, pamoja na kupata nafasi ya kujiendeleza kielimu, imewaingiza vijana hao kujihusisha na matumizi ya mitandao ya kijamii, wakiwa wanaitumia kwa sehemu kubwa katika kutazama picha zinazohusiana na mapenzi, hususan picha za ngono. Siku hizi kijana kuondoka nyumbani bila kuaga wazazi

wake imekuwa ni jambo la kawaida, kiasi kwamba anaweza hata kumjibu mzazi kuwa aachane na kufuatilia maisha yake. Kwa hiyo wimbo unasawiri jamii ya kizazi hiki kwa kueleza hali halisi kuhusiana na mmomonyoko wa maadili katika jamii.

### 4. NKA KIRITA (MKE WA KIRITA)

| | |
|---|---|
| **Kiongozi:** *Nka Kirita nyalamba lewayoe* | Mke wa Kirita alisema kwamba |
| **Washiriki:** *Ha haa!* | A haa! |
| **Kiongozi:** *Nyalamba lukabe matutae* | Alisema tutengeneze matuta |
| **Washiriki:** *Ha haa!* | A haa! |
| **Kiongozi:** *Matuta Mali-ya serikali* | Matuta ni mali ya serikali |
| **Washiriki:** *Ha haa!* | A haa! |
| **Kiongozi:** *Olele, olele, olelee* | Oh! Oh! Oh! |
| **Washiriki:** *Ha haa!* | A haa! |
| **Kiongozi**: *Nka Kirita nyalamba lewayoe* | Mke wa Kirita alisema kwamba |
| **Washiriki:** *Ha haa!* | A haa! |
| **Kiongozi:** *Olele, olele, olelee* | Oh! Oh! Oh! |
| **Washiriki:** *Ha haa!* | A haa! |

**Chanzo : Anna Okama miaka 72, tarehe 22/8/2012, Kijiji cha Kindi, Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo Kichagga ambao ulikuwa unaimbwa katika muktadha wa unyago. Katika wimbo huu, *Nka kirita* ni mwanamke ambaye alikuwa anahimiza wenzake kufanya shughuli za shambani. Kipindi hicho, katika jamii ya Wachagga, kulitokea ugonjwa wa zao la kahawa, zao lililokuwa linategemewa kibiashara. Kutokea kwa ugonjwa huo, kulisababisha kuanguka bei ya zao hilo. Hivyo, jamii ikawa inahimizwa kulima mazao mengine mbadala ili kuweza kumudu hali ya maisha katika jamii.

Kwa sasa wimbo huu unapoimbwa kwenye miktadha mingine, unasawiri hali halisi ya maisha ya jamii. Aidha, hii ni kutokana na hali iliyopo kwa sasa ya uhimizaji wa serikali kuhusiana na suala la Kilimo Kwanza, ambapo kilimo ndicho kitakachomkomboa Mtanzania wa kijijini kuwa na maisha bora.

### 5. KIMBIKIMBI (MSUKOSUKO)

**Kiongozi:** *Oh! Kimbikimbie* Oh! Msukosuko
**Washiriki:** *Oh! Kimbi na kimbaya* Oh! Msukosuko mkubwa
**Kiongozi:** *Oh! Kimbikimbie* Oh! Msukosuko
**Washiriki:** *Oh! Kimbi na kimbaya* Oh! Msukosuko mkubwa
**Kiongozi:** *Ngadema soko lee* Nikilima maharage
**Washiriki:** *Oh! Kimbi na kimbaya* Oh! Msukosuko mkubwa
**Washiriki:** *Oh! Kimbi na kimbaya* Oh! Msukosuko mkubwa
**Kiongozi:** *Soko tikadeka lee* Maharage yakipotea
**Washiriki:** *Oh! Kimbi na kimbaya* Oh! Msukosuko mkubwa
**Kiongozi:** *Memba akadeka lee* Mahindi yakipotea
**Washiriki***: Oh! Kimbi na kimbaya* Oh! Msukosuko mkubwa
**Kiongozi:** *Oh! Kimbikimbie* Oh! Msukosuko
**Washiriki***: Oh! Kimbi na Kimbaya* Oh! Msukosuko mkubwa

**Chanzo: Lawrencia Mushi miaka 69, tarehe 25/10/2012 Kijiji cha Kindi, Tarafa ya Kibosho**

Wimbo huu wa Kichagga ulikuwa unaimbwa katika muktadha wa unyago. Wimbo huu uliimbwa kwenye miaka ya sabini, ukiwa unaelezea maisha ya jamii katika kipindi hicho. Kipindi hicho kulikuwa na njaa kubwa iliyosababishwa na ukame. Kwa hiyo katika wimbo huu, msanii anaelezea namna msukosuko ulivyokuwa ndani ya jamii. Anasema, alilima maharage, mahindi vyote vilipotea. Katika kipindi hicho, jamii ya Wachagga walikuwa wanakula mlo mmoja kwa siku. Aidha, mlo huo ulitokana na chakula cha msaada walichokuwa wanapewa na serikali, ambacho kilikuwa ni vibaba vya unga.

Wimbo huu kwa sasa unapoimbwa katika miktadha mingine, kijamii unasawiri maisha halisi kutokana na kwamba hali ya maisha katika jamii, kiuchumi kuhusiana na pato la jamii iko juu sana. Kijamii gharama za misha zimepanda, hususan katika elimu, maji, umeme na matibabu. Kipato cha walio wengi katika jamii ya Wachagga ni cha chini, kiasi kwamba kumudu maisha ya kusomesha watoto, kuwa na huduma za maji, umeme na kupata matibabu imekuwa ni suala la msukosuko katika jamii ya Wachagga.

## 6. MAMBO SISA (MAMBO SASA)

| | |
|---|---|
| **Kiongoz**i *Aya mambo sisa,* | Haya mambo sasa |
| **Washiriki:** *Aya mambo sisa* | Haya mambo sasa |
| **Kiongozi:** *Nka mndasa nyare mborue,* | Jirani ni mwongo |
| **Washiriki:** *Aya mambo sisa* | Haya mambo sasa |
| **Kiongozi:** *Nyalamba muna nyaledichae* | Alisema mtoto alikimbia |
| **Washiriki:** *Aya mambo sisa* | Haya mambo sasa |
| **Kiongozi:** *Nyalamba muna nyaletolae,* | Alisema mtoto aliruka |
| **Washiriki:** *Aya mambo sisa* | Haya mambo sasa |
| **Kiongozi:** *Nka muona kabyo mundoroe,* | Mama pigiwa vigelegele |
| **Washiriki:** *Aya mambo sisa* | Haya mambo sasa |
| **Kiongozi:** *Warisinda wedu kabyo ndoroe* | Shemeji yetu pigiwa vigelegele |
| **Washiriki:** *Aya mambo sisa* | Haya mambo sasa |
| **Kiongozi:** *Mbo warisinda wedue* | Ndiye shemeji wetu |
| **Washiriki:** *Aya mambo sisa* | Haya mambo sasa |
| **Kiongozi:** *Nta ngilekariya ngambya notie* | Ningevumilia nipokee noti |
| **Washiriki:** *Aya mambo sisa* | Haya mambo sasa |

**Chanzo: Mama Mkashilingi miaka 70, tarehe 20/10/2012 kijiji cha Kindi Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo wa Kichagga wa ngoma ya *Mbassa*, ambao uliimbwa katika muktadha wa unyago. Wimbo huu ulitumia lugha ya kawaida ya jamii ya Wachagga. Wimbo huu ulikuwa unaelezea tabia za watu waliokuwa wawongo na wambeya katika jamii ya Wachagga. Umbeya na uwongo ni mambo ambayo yalifarakanisha na kusababisha mgogoro ndani ya jamii. Kufuatia hojaji, msanii wa wimbo huu alieleza kwamba ulikuwa unaimbwa kwa sababu watu waliokuwa wambeya na wawongo, walifanya ndoa za watu kusambaratika, pia walisababisha watu kujiingiza katika imani za kishirikina, hata vifo viliweza kutokea.

Wimbo huu unapoimbwa katika miktadha ya sasa, unasawiri jamii kutokana na mfumo wa maisha yaliyopo sasa. Ni ukweli usiopingika kwamba kutokana na mfumo wa siasa uliopo katika jamii, mfumo ambao ni wa vyama vingi vya siasa, inapofika kipindi cha kampeni, wanasiasa huwahadaa wanajamii kwa kuahidi mambo mengi ya kuwatekelezea, lakini mwisho wa siku, hata nusu ya ahadi zao zinakuwa hazijatekelezwa. Zaidi ya hapo,

kupitia vyombo vya habari vinasikika vikitangaza matukio ya vifo vinavyosababishwa na wivu wa mapenzi, kuonyesha kwamba habari za mahusiano ya wawili hao zimepatikana kutokana na umbeya au uwongo. Hali hii inathibitisha ukweli kwamba umbeya na uwongo bado umo ndani ya jamii, jambo ambalo linafanya wimbo wa *Mambo Sisa* uweze kushadidia ukweli huo.

### 7. NDORO (TUMBILI)

| | |
|---|---|
| **Kiongozi**: *ngenda mashie,* | Nilienda mbali |
| **Washiriki:** *nga-acha* | Nikarudi |
| **Kiongozi:** *Ngalemyo kwi* | Nilishindiwa wapi |
| **Washiriki:** *Nsangeni Wo-Narumu* | Kwenye mchanga wa Narumu |
| **Kiongozi:** *Ndoro ngiche* | Ndoro nije |
| **Washiriki:** *Iya mmbala* | Haya magadi |
| **Kiongozi:** *Ndoro ngiche* | Ndoro nije |
| **Washiriki:** *Iya mmbala*. | Haya magadi |

**Chanzo: Editha Edward miaka 48, tarehe 20/8/2012, kijiji cha Manushi, Tarafa ya Kibosho**

Wimbo huu wa ngoma ya *Mbassa* ulikuwa wa uchechemuzi, ukiwaelezea akina mama waliokuwa wameenda kutafuta magadi. Magadi ni aina fulani ya kilainishio cha kupikia vyakula aina ya maharage, mahindi na mboga za majani. Magadi yalifuatwa mbali sana, mwendo wa masaa mengi. Kwa hiyo wimbo huu ulikuwa unaimbwa kwa lengo la kutiana moyo wa kuwa wavumilivu katika safari. Msanii alipohojiwa, alieleza kwamba kipindi hicho kilikuwa pia kipindi ambacho akina mama walikuwa wanabeba ndizi kichwani na kwenda kuuza mjini. Kutoka kijijini hadi mjini ulikuwa umbali zaidi ya kilometa kumi. Kwa hiyo wimbo huu ukiimbwa katika miktadha ya sasa, unavuka mipaka ya jamii ya Wachagga, na kugusa jamii zingine za Watanzania kwa sababu kuna jamii ambazo zinapata adha ya kufuata maji mbali, hususan mikoa ya Shinyanga, Singida, Tabora na Dodoma.

### 8. KALISTA (KALISTA)

| | |
|---|---|
| **Kiongozi:** *Oh! Kalista mbee,* | Oh! Kalista dada |
| **Washiriki:** *Karenguo mawale* | Amevunjiwa mianzi |
| **Kiongozi:** *Nyalenda ko Mwafrikae,* | Alienda kwa baa |
| **Washiriki:** *Karenguo mawale* | Amevunjiwa mianzi |
| **Kiongozi:** *Mwafrika ko Rafelie,* | Baa ni kwa Rafaeli |
| **Washiriki:** *Karenguo mawale* | Amevunjiwa mianzi |
| **Kiongozi**: *Rafeli kibosho umbwee,* | Rafaeli yuko Kibosho Umbwe |
| **Washiriki:** *Karenguo mawale* | Amevunjiwa mianzi |
| **Kiongozi:** *Kishida kyadumbukae,* | Nguo ya ndani imekatika |
| **Washiriki:** *Karenguo mawale* | Amevunjiwa mianzi |
| **Kiongozi:** *Sidiriya yadumbukae,* | Brazia imekatika |
| **Washiriki:** *Karenguo mawale* | Amevunjiwa mianzi |
| **Kiongozi:** *Kabalya Yesu, Yesue!* | Alisema Yesu Yesu! |
| **Washiriki:** *Kareguo mawale* | Amevunjiwa mianzi |
| **Kiongozi:** *Oh! Kalista mbee,* | Oh! Kalista dada |
| **Washiriki:** *Karenguo mawale* | Amevunjiwa mianzi |
| **Kiongozi:** *Ngindewiya kuda babae,* | Nitamwambia nini baba |
| **Washiriki:** *Karenguo mawale* | Amevunjiwa mianzi |
| **Kiongozi:** *Ngindewiya kuda nsachae,* | Nitamwambia nini kaka yake |
| **Washiriki***: Karenguo mawale* | Amevunjiwa mianzi |
| **Kiongozi**: *Oh! Kalista mbee,* | Oh! Kalista dada |
| **Washiriki:** *Karenguo mawale.* | Amevunjiwa mianzi |

**Chanzo: Lauresia Mushi miaka 69, tarehe 25/10/2012 Kijiji cha Kindi. Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo ambao unaelezea wasichana wawili waliokuwa marafiki, ila mmoja alikuwa mjanja kuliko mwenzake. Kwa hiyo alikuwa anatumia ujanja wake kumdanganya mwenzake kwenda baa kunywa pombe na kufanya umalaya. Wakiwa huko walivamiwa na vijana wa kiume, yule mjanja alifanikiwa kutoroka na kukimbia. Nyoni (1991) anamweleze mwanamke ambaye alikuwa anatembea sokoni kutafuta wanaume, hali iliyosababisha jamii nzima kumchukia. Katika wimbo wake anasema:

| KIMATENGO | KISWAHILI |
|---|---|
| *Mbona jutotwi cheki* | Mwanamke amechukua hundi |
| *Je bakomani bandu* | Amabayo wanaume wanaigombania |
| *Mbomba yutotwi cheki* | Mwanamke amechukua hundi |
| *Je bakomani bandu pasoko* | Ambayo wanaume wanaigombania sokoni |
| *Jwakahika Patembo* | Wakati ameenda Litembo |
| *Jokomane nesi Patembo* | Manesi wanamfokea |
| *Limbumba lipumbavu* | Mwanamke mpumbavu |
| *Lekomane bandu pasoko* | Amesababisha wanaume kugombana sokoni |
| *Kizuri kinajiuza* | Kitu kizuri kinajiuza chenyewe |
| *Kibaya kinajitembeza* | Kitu kibaya kinajitembeza chenyewe |

**Chanzo : Nyoni (1991)**

Wimbo wa *Kalista* (Kalista) ni wa Kichagga wa ngoma ya *Mbassa* uliokuwa unaimbwa katika muktadha wa unyago. Mtoto wa kike alionywa kuepukana na matendo mabaya ya kufanya mapenzi katika umri mdogo, na kabla ya kuolewa. Wimbo huu unapoimbwa katika miktadha ya sasa, unasawiri jamii kutokana na hali ya mabadiliko ilivyo hivi sasa. Kwa kupitia mitandao ya kijamii kama vile “twiter”, “facebook”, “google” pamoja na simu za mkononi, vijana wengi, hususan wanaokuwa shuleni na vyuoni, wanaitumia mitandao hii katika kutumiana ujumbe ambao sehemu kubwa ya ujumbe hizo ni za kudanganyana na kutafutiana marafiki. Kwa hali hiyo inaonesha ni kwa namna gani wimbo huu unashadidia hali halisi kuendana na mabadiliko yaliyoko katika jamii.

### 9. MAYI (MAMA)

| | |
|---|---|
| **Kiongoz:** *Mayi Mae,* | Mama, |
| **Washiriki:** *Oh! Mmbora* | Oh! Mwanangu |
| **Kiongozi:** *Ngininga wari na kibata* | Nipe pombe kwa kikata |
| **Washiriki:** *Ngidaye ndami ndani woko* | Nimpelekee baba |
| **Kiongozi:** *Mayi mae* | Mama, |
| **Washiriki:** *Oh! Mmbora* | Oh! Mwanangu |
| **Kiongozi:** N*gininga malela na kinduwi* | Nipe maziwa kenye kibuyu |
| **Washiriki:** *Ngidaye Moli Moli woko* | Nimpelekee mwanao |
| **Kiongozi:** *Moli wokwi* | Mtoto yupi |

**Chanzo: Maria Moris miaka 62, tarehe 17/10/2012 kutoka Kijiji cha Mango Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo wa Kichagga wa ngoma ya *Mbassa* ambao ulikuwa unaimbwa katika muktadha wa unyago. Wimbo huu ulikuwa unamwelezea mwanamke mmoja ambaye alikuwa na tabia ya kuomba pombe na maziwa kila alipokuwa anahudhuria sherehe za unyago. Kutokana na hojaji, msanii wa wimbo huu alieleza kuwa wimbo huu ulikuwa unaimbwa kwa ajili ya kuelezea tabia za watu wanaomba omba kila kunapokucha.

Wimbo hu kwa sasa unapoimbwa katika muktadha kwa mfano, kwenye muktadha wa kisiasa, unaelezea hali halisi ya jamii ilivyo kwa sasa. Wimbo huu umeweza hata kuvuka mipaka ya jamii ya Wachagga, na kuelezea kwa ujumla hali halisi ya jamii ya Watanzania. Kwa mfano, nchini Tanzania, kupitia muhimili wa Bunge, jamii inaelezwa kuwa deni la taifa, limekua kwa asilimia fulani na nchi imepata misaada mbalimbali kupitia nchi matajiri. Pia wimbo uaonesha hali halisi ya jamii kutokana na kwamba kuna watu wengi katika miji ya Tanzania, ambao hukaa pembezoni mwa barabara na kuomba msaada kwa wapita njia. Kutokana na hali hii, inaonesha jinsi ambavyo Watanzania hatujawa na uwezo wa kujitegemea sisi wenyewe. Hivyo, wimbo huu bado unasawiri maisha halisi ya jamii, na siyo ya Wachagga tu, bali ya Watanzania wote.

**10. KIMIKU (KIZEE)**

| | |
|---|---|
| *Kimiku kya ntudu* | Kizee cha mlimani |
| *Kilasamba,* | Hakiwogi |
| *Kiute ku-konu,* | Kipate wapi wakati |
| *Wesana ngui* | Wa kuokotaa kuni |
| *Ngyolo tikadeka,* | Ngyolo zilipotea |
| *Kimanyie- kwi* | Hakujua |
| *Nkanweli nyeweyo nyeweyo* | Nkanwele alikuwepo alikuwepo |

**Chanzo: Berna Munishi, miaka 59, tarehe 17/10/2012, kijiji cha kindi, Tarafa ya kibosho**

Huu nii wimbo wa Kichagga wa ngoma ya *Mbassa*, ambao ulikuwa unaimbwa katika muktadha wa unyago. Wimbo huu ulikuwa unaelezea maisha ya mzee fulani aliyekuwa mchafu, alikuwa haogi na alijenga nyumba yake mlimani. Msanii alipohojiwa kwa nini wimbo huo ulikuwa unaimbwa katika jamii ya Wachagga kwa wakati huo, maelezo ni kwamba kwa wakati huo katika jamii ya Wachagga kulitokea magonjwa ya kipindupindu ambayo yalisababishwa na uchafu, ndiyo maana wimbo huu ukawa unaimbwa.

Wimbo huu, unapoimbwa katika miktadha ya sasa, unashadidia na kusawiri maisha ya jamii, hususan jamii zinazoishi mazingira ya mjini. Kwa mfano, jiji la Dar es Salaam, limekuwa na uchafu sana, na watu wamejenga nyumba sehemu za mabondeni. Kwa sababu hiyo, hata Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania wa awamu nne, Mheshimiwa Daktari Gharib Bilal, ameamua kwa makusudi kuanzisha kampeni maalum za kufanya usafi katika jiji la Dar es Salaam. Kutokana na hilo, inaonekana ni kwa jinsi gani wimbo huu, bado unasawiri maisha halisi ya jamii ya Watanzania.

### 11. NDEKE NSEMENU (NDEGE MSOMENO)

| | |
|---|---|
| *Ayo ndeke nsemenu* | Hiyo ndege Msomeno |
| *Mayi kakuduma kulaleye* | Mama akikutuma usikatae |
| *Ayo ndeke nsemenu* | Hiyo ndege Msomeno |
| *Ndami kakuduma kuladede* | Baba mkwe akituma usikatae |
| *Ayo ndeke nsemenu* | Hiyo ndege Msomeno |
| *Ko wandu kwenda utere* | Kwa watu nenda polepole |
| *Ayo ndeke nsemenu* | Hiyo ndege Msomeno |
| *Kuladedye mami wichoe* | Usimseme mama mkwe vibaya |
| *Ayo ndeke nsemenu* | Ayo ndege Msomeno |
| *Kokoya walelelee* | Ukikuta wamelala |
| *Ayo ndeke nsemenu* | Hiyo ndege Msomeno |
| *Washota ndwe na sindee* | Wakielekeza vichwa kusini |
| A*yo ndeke nsemenu* | Hiyo ndege Msomeno |
| *Newe kuwelala kudo kudo* | Na wewe lala hivyo hivyo |
| *Ayo ndeke nsemenu* | Hiyo Ndege Msomeno |
| *Kokoya wawode mborue* | Kama ni wawongo |
| *Ayo ndeke nsemenu* | Hiyo ndege Msomeno |
| *Ewe wika muda kanee* | Wewe weka maji mdomoni |

| | |
|---|---|
| *Ayo ndeke nsemenu* | Hiyo ndege Msomeno |
| *Ko wandu kwenda utere utere* | Kwa watu nenda polepole |
| *Ayo ndeke nsemenu* | Hiyo ndege Msomeno |
| *Utere, utere* | Pole pole |
| *Ayo ndeke nsemenu* | Hiyo ndege Msomeno |

**Chanzo: Mama Elizabeth Minja miaka 68, tarehe 15/10/2012 kijijini cha Msasani Kindi, Tarafa ya Kibosho**

Huu ni wimbo wa ngoma ya *Mbassa* wa kabila la Kichagga, ambao ulikuwa unaimbwa katika muktadha wa unyago. Wimbo huu ulikuwa unamwelezea mtoto wa kike ambaye alikuwa amekaribia kuolewa, akiambiwa kuwa akiolewa, atakuwa ameyaanza maisha mapya, katika familia tofauti na aliyokuwa anaishi nayo. Hivyo, ilimbidi awe ni mtu wa kutunza siri na asiwe mropokaji kwa maana ya kuongelea kila jambo analoliona. Msanii alipohojiwa ni kwa nini wimbo huo uliimbwa kipindi hicho, maelezo ni kwamba kilikuwa ni kipindi ambacho katika jamii, kulitokea migogoro na mifarakano katika maisha ya ndoa. Lakini alioendelea kusema kuwa kwa kipindi hiki ni kama migogoro ya ndoa imezidi ikilinganishwa na kipindi cha mafunzo ya unyago.

Wimbo huu unapoimbwa kwa sasa, unasawiri hali halisi ya jamii kutokana na mambo mengi yanayotokea ndani ya jamii. Kwa mfano, kipindi hiki ambacho ni cha mfumo wa vyama vingi vya siasa, kumekuwa na uvujaji wa siri za serikali kupitia wanasiasa, jambo ambalo limesababisha migogoro na migongano mingi ndani ya jamii. Baadhi ya vingozi wa kisiasa wa siku hizi, wamekuwa ni watu ambao wanatoa maneno ya kuropoka, kukashfiana na kudhalilishana. Hali hii imejidhihirisha kwa wanasiasa wa Bunge la awamu ya nne, ambao wamekuwa wakitoleana maneno ya kashfa. Kwa uthibitisho huu, ni ukweli usiopingika kwamba wimbo huu unapoimbwa kwa sasa unasawiri hali halisi ya maisha ya Watanzania.

## 12. SENGOMBE (SENGO)

| | |
|---|---|
| *Oh! Sengo nyindu Mangie x2* | Oh! Sengo mtu Mangi x2 |
| *Iyamba Sengoombee x2* | Ndiye Sengo |
| *Sengo mbidi ngichae* | Sengo ni fimbo nzuri |
| *Iyamba Sengoombee* | Ndiye Sengo |
| *Ekato Mangi Mushi wayi* | Huyo Mangi ndiye kaka |
| *Iyamba Sengoombee* | Ndiye Sengo |
| *Ekato Mangi nyi nndu anagane* | Huyo Mangi ni mtu mkubwa |
| *Iyamba Sengombee* | Ndiye Sengo |
| *Ekato Mangi nacha na mbenge wayie* | Huyo Mangi ndiye anakuja mbele |
| *Oh! Sengo nyindu Mangie x2* | Oh! Sengo mtu Mangi x2 |
| *Iyamba Sengombee x2* | Ndiye Sengo x2 |

**Chanzo: Mama Elizabeth Minja miaka 68, Tarehe 15.10.2012, Kijiji cha Kindi Msasani, Tarafa ya Kibosho**

Wimbo huu ambao ulikuwa unaimbwa katika muktadha wa unyago, ulikuwa unamsifia kiongozi na mtawala wa jamii ya Wachagga ambaye kwa kipindi hicho alijulikana kwa jina la Mangi. Katika mahojiano na msanii, alieleza kwamba ilikuwa ni desturi ya Wachagga kumheshimu mtawala wao, na kumwimbia nyimbo za kumsifu, hususan alipokuwa anafanya mikutano na wanajamii. Katika wimbo huu umetumia maneno ya Kichagga, lakini yanaeleweka kiurahisi katika jamii hiyo.

Kwa sasa, wimbo huu unapoimbwa katika muktadha, madhalan wa kisiasa, bado unasawiri jamii husika. Kwa msingi huo jamii ya Watanzania, utamaduni wa kuenzi viongozi wa kiserikali au wa kisiasa, unaendelea kudumishwa. Haya huwa yanatokea wakati kiongozi huyo wa kiserikali au wa kisiasa anapotembelea wananchi kwa lengo la uhamasishaji wa shughuli za kisiasa au za kiuchumi. Kwa hiyo ni dhahiri kuwa wimbo huu wa *Sengombe*, unapoimbwa kwa sasa unasawiri maisha yaliyoko katika jamii.

### 4.3 Matokeo ya Utafiti

Uchambuzi wa matokeo ya utafiti huu, umezingatia zaidi suala la kimuktadha, katika kuchambua maudhui ya nyimbo za ngoma ya *Mbassa*, na kujua namna maudhui hayo yanavyosawiri katika jamii ya sasa, kuendana na mabadiliko yaliyoko ndani ya jamii. Aidha, utafiti huu pia ulitaka kujua iwapo nyimbo za ngoma ya *Mbassa* zilizokuwa zinaimbwa wakati huo (muktadha wa unyago), kama bado zinasawiri mabadiliko ya kimaendeleo yaliyotokea katika jamii.

#### 4.3.1 Athari za Kimaendeleo katika Muktadha wa Nyimbo za Ngoma ya *Mbassa* ya Jamii ya Wachagga

Maswali ya hojaji na dodoso, yalisaidia kwanza, kujua maudhui ya nyimbo za ngoma ya *Mbassa* yalivyokuwa katika muktadha wa unyago, na namna nyimbo hizo zilivyoathiriwa kutokana na mabadiliko yaliyotokea katika jamii, pia maudhui ya nyimbo hizo yanavyosawiri kuendana na mabadiliko yanayotokea katika jamii kwa sasa. Pili, utafiti huu ulitaka kujua nyimbo za Ngoma ya *Mbassa*, ambazo zilikuwa zinaimbwa kipindi cha nyuma (katika muktadha wa unyago), zinapoimbwa kwa sasa, kama bado zinashadidia mabadiliko yaliyoko ndani ya jamii.

#### 4.3.2 Maudhui ya Nyimbo za Ngoma ya *Mbassa* Yanavyoakisi Mabadiliko Yanayotokea katika Jamii.

Katika uchambuzi wa nyimbo kumi na moja uliofanywa na mtafiti, umeonesha na kubainisha nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga zilizokuwa zinaimbwa katika muktadha wa unyago, kwa sasa maudhui hayo yanaswiri jamii ya sasa, na nyimbo hizo zimeatiriwa katika vipengele vya mandhari, hadhira, fanani na tukio linalotendeka. Kwa mfano, katika wimbo namba moja (WARISINDA), wimbo ambao uliimbwa katika

muktadha wa unyago, maudhui yake yalikuwa kumkataza mtoto wa kike kufanya mapenzi kabla ya kuolewa, jambo ambalo imeonekana kuwa maudhui hayo bado yanasawiri katika jamii. Pia imeonekana kwamba muktadha unapobadilika, wimbo huu unaathiriwa katika vipengele vya mandhari, hadhira na tukio linalotendeka. Aidha, unapoimbwa kwa sasa, kuna matumizi ya maneno kama vile glasi, kikombe na chupa kama vifaa vya kunywea pombe (mbege), kwa wakati ule havikuwepo, badala yake walitumia kata na chungu. Maneno haya yanaonyesha namna wimbo huo ulivyoathiriwa kutokana na mabadiliko ya kimaendeleo. Kwa hiyo, kutokana na maelezo hayo, inaonesha ni kwa namna gani maudhui ya nyimbo za ngoma ya *Mbassa* katika muktadha wa unyago, yanavyosawiri muktadha wa sasa kuendana na mabadiliko yanayotokea katika jamii.

Wimbo namba tatu (*OH! KIWONA)* ni wimbo ambao unatoa ujumbe wa uvumilivu, ujasiri, mateso na ushirikiano. Katika muktadha wa unyago, wimbo ulikuwa unaelezea masaibu yaliyoikumba familia ya mtoto aliyefanyiwa tohara. Wimbo huu unapoimbwa kwa sasa, unaonyesha kusawiri katika jamii kufuatia mabadiliko yaliyopo, hususan kipindi hiki ambacho kimeghubikwa na maradhi ya ugonjwa wa UKIMWI. Katika kipindi hiki, familia nyingi zinataabika sana katika kulea waathirika wa UKIMWI, hivyo kunahitajika ujasiri, uvumilivu na ushirikiano katika kulea waathirika hao. Aidha, wimbo huu umeonekana kuathiriwa na mbadiliko hayo katika vipengele vya mandhari, hadhira, fanani na tukio linalotendeka. Kuhusiana na mandhari, wimbo huu ulikuwa unaimbwa katika mazingira maalum ambayo, aidha ilikuwa nyumbani kwa wazazi wa mtoto kike, au nyumbani kwa wazazi wa bibi mzaa mama wa mtoto wa kike. Hadhira ilikuwa ni rika la wazee. Fanani alikuwa Manju maalum aliyeandaliwa na tukio lililotendeka lilikuwa ni tohara. Kwa sasa wimbo huu haufuati utaratibu huo tena. Kuhusu mandhari, unaweza kuimbiwa katika mazingira yoyote, hadhira inakuwa ni mchanganyiko watoto kwa wazee,

fanani anaweza kujitokeza mtu yoyete alimradi anaufahamu wimbo huo na tukio linaweza kuwa kwenye muktadha wa maombolezo au muktadha mwingine. Kwa hiyo kupitia wimbo huu, ni uthibitisho kuwa nyimbo za ngoma ya *Mbassa*, maudhui yake yaliendana na mabadiliko yanayotokea katika jamii, na vivyo hivyo zinaathiriwa kutokana na kubadilika kwa muktadha.

Wimbo namba nne (IYOWE), huu ni wimbo ambao maudhui yake wakati wa muktadha wa unyago, yalikuwa yanasisitiza udumishaji wa mila na desturi katika jamii ya Wachagga. Kwa kuwa suala la mila na desturi halilengi mviga wa unyago tu, bado dhamira hii inasawiri katika jamii hiyo kupitia nyanja zingine za mila na desturi kama vile kuzaliwa kwa mtoto, mazishi na kumwoza mtoto wa kike. Kwa hiyo wimbo huu utakapokuwa unaimbwa katika miktadha hiyo, utakuwa unasawiri maisha ya jamii. Lakini wimbo huu utakuwa umeathiriwa katika nyanja za mandhari, hadhira, fanani na tukio linalotendeka. Katika mandhari, awali imeelezwa kwamba nyimbo za Ngoma ya *Mbassa* zilivyokuwa zinaimbwa katika muktadha wa unyago, zilikuwa zinaimbiwa katika eneo maalum. Lakini zinapoimbwa katika miktadha ya sasa, zinaweza kuimbiwa katika eneo lolote. Hadhira kipindi hicho cha unyago, ilishirikisha zaidi wazee, lakini kwa sasa inashirikisha watu mbalimbali wakiwemo wazee na watoto. Fanani anaweza akawa mtu yeyote, hali mradi anaufahamu huo wimbo. Pia, tukio haliwi tena unyago. Kwa hiyo, wimbo huo ukiimbwa kwa sasa unasawiri mabadiliko yaliyoko katika jamii kutokana na maudhui yake.

### 4.3.3 Nyimbo za Ngoma ya Mbassa Zinavyosawiri Mabadiliko ya Sasa katika Jamii

Katika nyimbo kumi na mbili zilizochambuliwa, zimeonesha kwamba zinapoimbwa katika muktadha wa sasa zinashadidia na kusawiri mabadiliko yaliyoko ndani ya jamii.

Kwa mfano, katika wimbo namba moja (UKIWA REREYE), uliimbwa kipindi ambacho jamii ilikuwa katika masikitiko, huzuni na taabu nyingi kutokana na vifo vya watoto vilivyosababishwa na magonjwa ya surua, kifaduro na ndui. Aidha, wimbo huu umeonekana kuendana na kusawiri hali ya sasa kwa sababu jamii katika kipindi hiki, iko kwenye masikitiko, huzuni na taabu ambazo zinatokana na majanga ya UKIMWI, Malaria na vijana wengi kutumia madawa kulevya, jambo linalosababisha kupoteza nguvu kazi katika jamii na matokeo yake ni kushuka pato la jamii. Kwa hiyo wimbo huu unapoimbwa kwa sasa, unaeleza hali halisi ya maisha ya jamii.

Wimbo namba mbili (MMBI ALEBALYA BIRO), ulikuwa unaeleze mabadiliko ya kiuchumi yaliyotokea katika jamii, likiwemo suala la kupanda kwa bei ya vitu kama vile sabuni, sukari nyama na mafuta. Mambo haya yote yalitokea kipindi cha wahujumu uchumi. Wimbo huu kwa sasa unasawiri katika jamii kutokana na kwamba kipindi hiki kimetawaliwa na masuala ya ufisadi, rushwa na wizi, jambo ambalo linaifanya jamii kuishi katika mazingira magumu ya kushindwa kumudu huduma za kijamii kama vile shule, matibabu, umeme na maji. Kwa hiyo, wimbo huu unathibitisha ukweli kwamba nyimbo za ngoma ya *Mbassa* bado zinaendana na mabadiliko yanayotokea katika jamii, ila kinachobadilika ni muktadha wa nyimbo hizo kama ilivyokwisha elezwa hapo awali.

Wimbo namba tatu (SIRYA MMBA), ulikuwa unaelezea mmomonyoko wa maadili ya watoto wa kike katika jamii ya Wachagga. Wimbo huu uliimbwa kwenye miaka ya themanini kipindi ambacho watoto wa kike walianza kujiingiza katika tabia za kwenda kwenye sherehe za usiku (madisko), ambako huko kulifanyika vitendo viovu na vibaya vilivyokuwa vinaiingiza jamii katika madhara ya mmomonyoko wa maadili. Kwa baadhi ya nyimbo hizo zilizotolewa kama mifano, zinathibitisha wazi kwamba nyimbo za ngoma

ya *Mbassa*, ambazo ziliimbwa katika muktadha wa unyago, zinapoimbwa kwa sasa, zinaonekana kuathiriwa kwenye vipengele vya mandhari, hadhira, fanani na tukio linalotendeka. Lakini, bado maudhui ya nyimbo hizo yanashadidia na kusawiri mabadiliko yanayotokea katika jamii.

### 4.4 Hitimisho

Kukamilika kwa sura hii ya nne iliyojihusisha na uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa matokeo ya utafiti, imemsaidia mtafiti kuandika sura ya tano, ambayo inatoa muhtasari wa utafiti kama hitimisho la utafiti.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Utafiti ulijihusisha katika kuchunguza na kubaini athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa.* Sehemu hii inahitimisha utafiti uliofanywa na mtafiti katika kurejea malengo mahsusi ambayo yaliwekwa na mtafiti; yaliyotaka kukusanya nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga na kuchambua maudhui ya nyimbo hizo, kuchunguza ni kwa namna gani nyimbo hizo zilivyoathiriwa na mabadiliko ya kimaendeleo katika jamii. Pia nyimbo hizi ambazo zilikuwa zinaimbwa katika muktadha wa unyago, ni kwa namna gani zilishadidia na kusawiri mabadiliko yanayotokea katika jamii. Uchambuzi wa utafiti huu, ulizingatia nadharia ya Kihemenitiki. Mtafiti amechambua nyimbo za ngoma ya *Mbassa* kufuatana na zilivyoimbwa na wasanii mbalimbali wa jamii ya Wachagga, na kwa mujibu wa malengo yetu ya utafiti.

## 5.2 Uchambuzi wa Data Zilizokusanywa

Lengo mahsusi la kwanza la utafiti huu lilikuwa kukusanya nyimbo za ngoma ya *Mbassa*. Lengo hili lilijibiwa na dodoso A, kwa kufanya uchambuzi wa nyimbo kumi na moja ambazo zilitazamwa namna zilivyoathiriwa na maendeleo na jinsi maudhui yanavyosawiri ndani ya jamii kuendana na mabadiliko. Pia mwongozo B wa hojaji kwa Manju[2] umesaidia kupata majibu ya swali la lengo la kwanza[3]. Nadharia ya Kihemenitiki imesaidia kuchambua nyimbo hizo zilizokusanywa.

[2] Picha zao kwenye kielelezo na. 1, 2 & 3
[3] Majina yako kwenye kielelezo na. 8 jedwali na. 1

### 5.2.1 Mafunzo yaliyotokana na Nyimbo za Ngoma ya *Mbassa*

Nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga lengo kuu lilikuwa kuburudisha na kuelimisha. Nyimbo hizi zilikuwa zinaimbwa katika muktadha wa unyago. Lakini leo hii zinaimbwa katika miktadha mingine, ambapo imedhihirika kuwa maudhui yake bado yanaendana na mabadiliko yanayotokea katika jamii, bali zinaathiriwa katika uwasilishaji wake kutokana na kubadilika kwa muktadha. Aidha, nyimbo zile zile zinapoimbwa katika miktadha ya sasa, zimeonekana kushadidia na kusawiri mabadiliko yaliyoko ndani ya jamii. Miktadha ya sasa inayoimbwa nyimbi hizi, ni pamoja na harusi, dini, matambiko, kilimo, siasa na mingine kwa kadiri ya mabadiliko katika jamii. Katika miktadha ya sasa, ujumbe unaosawiri ni pamoja na kuwaelekeza vijana kupenda kufanya kazi, kufundisha vijana kuwatii wakubwa, kuwafundisha vijana kuishi kwa ushirikiano, zinawafundisha vijana kujiadhari na mazingira hatarishi, zinafundisha namna ya kutatua migogoro katika familia, zinafundisha uvumilivu katika maisha pia zinafundisha ujasiri. Nyimbo hizi pia zinaelezea majanga ambayo yameshamiri katika jamii kama vile ufisadi, rushwa, utumiaji wa madawa ya kulevya na magonjwa kama vile UKIMWI na Malaria.

## 5.3 Athari za Kimaendeleo katika Muktadha wa Nyimbo za Ngoma ya *Mbassa*

Katika kipindi hiki, ndani ya jamii kumekuwa na mabadiliko yaliyoambatana na wimbi la vijana wengi kuondoka kijijini na kwenda mjini kwa lengo la kutafuta maisha yaliyo bora zaidi, kumekuwa na mabadiliko ya mfumo wa siasa kutoka mfumo wa chama kimoja cha siasa na kuingia katika mfumo wa vyama vingi, kumekwa na majanga mbalimbali yaliyosababishwa na ufisadi, rushwa, utumiaji wa madawa ya kulevya na magonjwa kama ya UKIMWI na Malaria. Aidha, nyimbo zilizokuwa zinaimbwa katika muktadha wa unyago, zinapoimbwa katika miktadha ya sasa, zinaonekana kushadidia na kusawiri mabadiliko yaliyoko katika jamii. Hii ni kwa mujibu wa hojaji na dodoso zilizotumika katika utafiti huu.

## 5.4 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Utafiti huu ulihusu athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga. Tafiti zijazo zinaweza kushghulika na Nyimbo za Ngoma ya *Mbassa* katika kipengele cha fani. Hili ni eneo ambalo mtafiti amegundua kwamba halijashughulikiwa.

## MAREJELEO


Abdalla, A.B (2012), "Athari za Mabadiliko Katika Nyimbo za Taarab: Lugha na Uwasilishaji", Haijachapwa, *Shahada ya Uzamili Katika Fasihi ya Kiswahili,* Chuo Kikuu cha Dodoma.

Abiduna, A (2006), "Structure of Children Songs in Shambala Tribe", *A Degree Dissertation*, University of Dar es Salaam.

BAKIZA, (2010). *Kamusi ya Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford Univesity Press.

Clines, D.J.A. (1982). Biblical Hermenitics in Theory and Practice, *Christian Brehren Review*. 31, 32 pg 65 – 76.

Daud, A.S (2012), "Nyimbo za Ngoma ya Daku: Mtazamo wa Kifasihi", (Haijaijachapwa), *Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili,* Chuo Kikuu cha Dodoma

Eagleton, T. (1983). *Literary Theory: An Introduction.* Minneapols: University of Minnesota Press.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa.* Nairobi: Oxford University Press.

Gadaner, H.G. (1960). *Truth and Method.* (Trans. 1975). Joel Weinsheimer and Donald G. Marshall. London: Sheed and Ward.

Gama, L (2005), "Changes and Socila Dynamics in Ngoni Songs Of Peramiho (SONGEA)", *A Dissertation B.A Degree,* University of Dar es Salaam.

Gibe, A.G (1978), "Fasihi ya Jamii Baadhi ya Washairi wa Kiswahili 1960 – 1977", *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*, Juz. 48, Na 1, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Dar es Salaam.

Haji, H.G (2011), "Mitindo ya Nyimbo za Uganga wa Pepo" Haijachapwa, *Shahada ya Uzamili ya Sayansi Jamii katika Fasihi ya Kiswahili,* Chuo Kikuu cha Dodoma.

Iser, W. (1978). *The Act of Reading: A Theory of Aesthetic Response.* Baltimore, MD: The Johns University Press.

John, J (2006), "The Social Significance of Yao Boys' Initiation Songs: A case Study of Chikudu Village in Masasi District", *Methodology and Practice in Oral Literature Research B.A Degree,* University of Dar es Salaam.

Kalenge, M.J (2012), "SANGU SONGS: A Changing Traditional", Unpublished M.A Thesis, University of Dar es Salaam.

Kezilahabi, E (1983), "Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi" *TUKI* Makala ya Semina III: 223-238.

Khamis, S.A.M (19830), "Nafasi ya fasihi simulizi katika jamii ya Tanzania." *MULIKA* Na 15. Uk. 32

Kirumbi, P.S. (1975). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Shungwaya Publishers Ltd.

Kirumbi, P.S. (1977). *Misingi ya Fasihi Simulizi.* Nairobi: Shungwaya Publishers Ltd.

Kombo, D.K na Tromp, D.L.A. (2006). *Proposal and Thesis Writing*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Komba, P.D.K. (1990). *Misingi ya Uchumi.* Dar es Salaam: Publishers & Sales Agency.

Lenard, G.(2006), "The Effect of Globalization on Roles and Functions of Pare Children Songs", *A dissertation of B.A Degree,* University of Dar es Salaam.

Lyongo, Taban Lo (1972). *Popular Culture in East Africa*. Nairobi: Longman.

Masele, E.I (2012), "Sukuma Women's and Men's songs: A Comperative Study" Unpublished, M.A *Kiswahili literature,* University of Dododma.

Massawe, R.E.K (1995), "Research Project Report on the Study of the Influence of Christianity on Chagga Oral Poetry", *Christianity on Chagga Oral Poetry: Case Study of Wedding Songs in Machame,* University of Dar es Salaam.

Mazigwa, S.A. (1991) *Fasihi ya Kiswahili*. Peramiho: BPN.

Mazrui, A. (1980). *Mwongozo wa Mui Huwa Mwema*. Nairobi: Heineman Kenya Ltd.

Mazrui, A na Kazungu E.K (1981) 'Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili Muhtasari: MwamkoToleo la Pili,' *Jarida la Chama cha Kiswahili.*

Mbunda, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: Education Publishers and Distribution Ltd.

Mbunda, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: EAEP.

Mdoe, S.R 2012 “Nyimbo za Michezo ya Watoto zinavyobadilika na wakati Kifani na Kiutamaduni katika Wilaya ya Magharibi Unguja”, (Haijachapwa), *Shahada ya Uzamili ya Sayansi Jamii katika Fasihi ya Kiswahili,* Chuo Kikuu cha Dodoma.

Minja, D.P (2000), “Chagga Wedding Songs and the social Change” Unpublished *Dissertation of the Bachelor Degree in Arts*, University of Dar es Salaam.

Minzi, L.D.T (19830, “A Critical Survey of Topical Songs in the Sangu Tribe”, *Unpublished Dissertation,* University of Dar es Salaam.

Mmbando, G (2004), “The Position of Traditional Wedding Songs in Chagga Pedagogy” *A dissertation of The Bachelor of Arts with Edation,* University of Dar es Salaam.

Moh’d, H.B (2012), “Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Taarabu za Zanzibar”, (Haijachapwa). *Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili,* Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mpangala, F (2006), “The Educative Function of Traditional Songs in Manda Societies: Case Study of Mganda and Kioda Songs” *A Dissertation of B.A Degree,* University of Dar es Slaam.

Mwakasaka, C.S (1978), “Oral Literature of Banyakyusa” *M.A. Thesis,* University of Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M (1989), “Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili” *MULIKA* Na 21, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: OUT.

Nassor, A.S (2004), “The Effect of Pemba Traditional Songs on Community Ethics” *A Dissertation Degree of Bachelor of Arts with Education,* University of Dar es Saalaam.

Newton, K.M. (1989). “Hermeneutics and Modern Literary Criticism” *British Journal of Aesthetics* 29. Pg. 117.

Nivahe, D.E (2012), “Athari ya Muktadha Katika Uwasilishaji wa Nyimbo za Sherehe za Jando na Unyago katika Jamii ya Wamakua”, Haijachapwa, *Shahada ya Uzamili ya Fasihi ya Kiswahili,* Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ndulute, C (1977), “The Place of Songs in Hehe Oral Literature” *Unpublished M.A. Thesis,* University of Dar es Salaam.

Ndimyake, M (2011), "Athari za Mabadiliko ya Kijamii na Kiuchumi kwa Nyimbo za Kapote za mwimbaji Mwandwanga katika Jamii ya Wanyakyusa", (Haijachapwa), *Ripoti ya Utafiti,* Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ndungo, C.W. (1991). *Misingi na Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili*.Nairobi: University of Nairobi.

Nyoni, F.P (1994), "A Dissertation of M.A. in Theatre Studies", *Workshop Theatre School of* English, University of Leeds.

Nyoni, F.P (1998), "Conformity and Change: Tanzanian Rural Theatre and Socio-Political Changes", *Doctoral Thesis,* University of Leeds

Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature: Backgrounds, Character and Continuty*. Bloomington and Indianapolis: Indian University Press.

Raj, H. (2005) *Theory and practice in social Research.* Delh India: Third revised edition Surjeet Publications.

Sengo, T.S.Y na Kiango, S.D (1973), *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi* Hisi Zetu 1 TUKI, Dar es Salaam.. Chuo Kikuu cha Dae es Salaam.

Songoyi, E.M. (1997). *Oral Literature 1*. The Open University of Tanzania: Msasani Tirdo Buildings.

Steven, Y (2011), "Athari za Maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Kwa Nyimbo za Watoto waishio Mjini: Mjini Mbeya na Tukuyu", (Haijachapwa), *Ripoti ya Utafiti,* Chuo Kikuu cha Dodoma.

Suleiman, H.K (2012), "Nyimbo za Ngoma ya Pungwa: Dhima na Athari yake katika Jamii ya Wazanzibari", (Haijachapwa), *Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswsahili,* Chuo Kikuu cha Dodoma.

Syimbo, B. na Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: EAEP.

Tompkins, J.P. (1980). *Reader Response Criticism.* Baltimore: Hohns Hopkins University Press.

Wachterhauser, B.R. (1991). *Hermeneutics and Modern Philosophy*. New York: Staty University of New York.


## VIAMBATANISHO A: VIELELEZO VYA PICHA

### KIELELEZO: MTAFITI AKIMSUBIRI MANJU KWA MAHOJIANO



**Chanzo: Picha toka eneo la utafiti kijiji cha Kindi Kati, Tarafa ya Kibosho tarehe 16.01. 2013**

**KIELELEZO: NA. 1 MTAFITI AKIWA NA MANJU ALIYEHOJIWA**



**Chanzo: Picha kutoka eneo la Utafiti Kijiji cha Kindi Kati, Tarafa ya Kibosho tarehe 16.01.2013. Jina la Manju ni Benedicta Zainabu Jacob umri miaka 97**

KIELELEZO: NA. 2 PICHA ZA MANJU WALIOHOJIWA



**Chanzo: Picha kutoka eneo la Utafiti, Kijiji cha Kindi Msasani, Tarafa ya Kibosho, tarehe 14.01.2013. Kutoka kushoto ni Elizabeth A. Minja umri miaka 68 na Martha Massaawe umri miaka 69**

KIELELEZO: NA. 3 PICHA YA MTAFITIWA AKIJAZA DODOSO



**Chanzo: Picha toka eneo la utafiti katika Kijiji cha Kindi, Tarafa ya Kibosho, tarehe 23.07.2013. Jina ni Severa J. Mushi miaka 49**

**KIELELEZO: NA 4 NYUMBA YA JADI**



**Chanzo: Picha hii ni kutoka Tamasha la Siku ya Wachagga lililofanyika Mjini Moshi katika Ukumbi wa Zumba Land tarehe 22/12/2012. Picha hii inaonyesha hali halisi kuhusiana na maelezo yaliyoko kwenye sura ya 2.5.3**

## KIAMBATA B: VIELELEZO VYA DODOSO NA HOJAJI

### KIELELEZO: NA 7

### DODOSO NA HOJAJI

A) DODOSO KWA KUNDI LA WANAUME NA WANAWAKE WA JAMII YA WACHAGGA

**Jina la mtafiti:** Mboya, Kolman Aloyce

**Tarehe ya kufanya udodosi**……………………

**Mahali pa Utafiti**…………………………

Tunafanya utafiti kuhusu athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo za ngoma ya *Mbassa* ya jamii ya Wachagga. Tunalenga kukusanya nyimbo za ngoma ya *Mbassa* na kuchambua maudhui yake pamoja na kuchunguza na kubaini athari za kimaendeleo katika muktadha wa nyimbo hizo za ngoma ya *Mbassa* **Tafadhali tunaomba ushirikiano wako katika kujibu maswali yetu.**

---

**Weka alama ya ( V ) katika mabano [ ] kwa jibu lililo sahihi na toa maelezo mafupi kwa sehemu zilizoachwa wazi (…………………………….)**

1. Katika jamii ya Wachagga kuna ngoma ya jadi unayoijua? NDIYO [ ] HAPANA [ ]

2. Kama jibu ni ndiyo ngoma hiyo inaitwaje? (a) Mdundiko [ ] (b) Mbassa [ ] (c) Ling'oma [ ]

3. Ngoma hii ilichezwa na nani kati ya makundi yafuatayo? (a) Wazee wanawake [ ] (b) wazee [ ] Wanaume [ ] (c) wazee wote wanawake na wanaume [ ] (d) vijana [ ]

4. Unaweza kututajia mafunzo machache yaliyokuwa yanatolewa katika Nyimbo hizo za Ngoma ya *Mbassa*? NDIYO [ ] HAPANA [ ]

5. Kama jibu ni ndiyo, tunaomba utueleze baadhi ya mafunzo yaliyokuwa yanatolewa.

(i)……………………………………………………………………………………

(ii)……………………………………………………………………………………

(iii)…………………………………………………………………………………

(iv)………………………………………………………………………………

**Ahsante kwa ushirikiano wako**

**B) MWONGOZO WA HOJAJI KWA MANJU WA NGOMA YA *MBASSA***

1.Tunaomba utueleze kwa kifupi historia yako, jina lako ni nani, una miaka mingapi, elimu yako.

2. Je, ngoma ya *Mbassa* ulianza kucheza ukiwa na umri wa miaka mingapi?

3. Ni nani aliyekufundisha kucheza na kuimba hizo nyimbo za ngoma ya *Mbassa*?

4. Unadhani nyimbo hizi za ngoma ya *Mbassa* zilikuwa zinaimbwa sana katika kipindi gani cha mwaka?

5. Uaweza kutusadia sababu chache kwa nini ziliimbwa katika kipindi hicho? (Tuzitaje kama tano hivi)

6. Unafikiri zilikuwa zinatoa mafundisho gani kwa jamii?

7. Katika mafundisho ya nyimbo hizo za ngoma ya *Mbassa*, unafikiri zililenga sana kundi lipi la jamii kati ya vijana na wazee?

8. Je, kuna madiliko yoyote yaliyotokea katika jamii na kuonekana kuwa yamechangiwa na nyimbo hizo za ngoma ya *Mbassa*?

9. Unaweza kutuimbia nyimbo chache zinazohusiana na ngoma hii ya *Mbassa*? (Wimbo huu una maana gani na uliimbwa wakati gani?)

10. Toa maoni yako kutokana na hizi nyimbo za ngoma ya *Mbassa*, kuhusiana na hali ilivyo

**Ahsante sana kwa ushirikiano wako**

**C) MWONGOZO WA HOJAJI KWA MAKUNDI YA VIJANA WASICHANA NA WAVULANA, WAZEE WANAUME NA WANAWAKE**

1. Tunaomba mutueleze nyimbo za ngoma ya *Mbassa* mlikuwa mnaziimba kipindi gani cha mwaka

2. Mnafikiri ni kwa nini mlikuwa mnaaziimba kipindi hicho?

3. Mnaweza kutuimbia wimbo wowote mmoja unaohusiana na ngoma ya *Mbassa*? Je wimbo huo una maana gani

4. Wimbo huo ulitoa mafundisho gani kwa Jamii?

5. Je, mafunzo hayo yaliweza kubadilisha jamii na kama ilibadilika ni kwa namna gani?

6. Ni nani aliyekuwa anapima mafunzo hayo kama yametekelezwa?

7. Je wimbo ulioimbwa miaka mitano iliyopita ukiimbwa hivi leo unaweza ukawa hali ile ile ya mwanzo?

8. Kama unabadilika unafikiri ni sababu zipi zilizofanya ubadilike?

9. Mwisho; Je, nyimbo za ngoma ya *Mbassa* mafundisho yake yalilenga kundi lipi katika jamiii? Je, kwa wale ambao hawakufuata mafundisho hayo walichukuliwa hatua zpi na hatua hizo zilichukuliwa na nani?

10. Tunaomba mtoe maoni yenu kuhusiana na nyimbo hizi za ngoma ya *Mbassa* mlivyoona hali ilivyokuwa hapo miaka ya nyuma, na hali ilivyo hivi sasa.

**Ahsante kwa ushirikiano wenu.**

## KIAMBATA C: MAJEDWALI YA MAJINA YA WATAFITIWA

### KIELELEZO NA. 8

### SAMPULI YA WATAFITIWA

Jedwali Na. 1 Kundi la Manju

| JINA | UMRI | KE | ME |
|---|---|---|---|
| Elizabeth A. Minja | 68 | | |
| Mkashilingi Mambosha | 70 | ✓ | |
| Lawrencia Masoka Mushi | 69 | ✓ | |
| Joseph Karani Mushi | 77 | | ✓ |
| Joseph Lengorori | 82 | | ✓ |
| Matei Sangisi | 63 | ✓ | |

Jedwali Na. 2 Kundi la Wazee

| JINA | UMRI | KE | ME |
|---|---|---|---|
| Benedicta Zainabu Jacob | 97 | ✓ | |
| Peter Mauna Soka | 93 | | ✓ |
| Joseph Mngere Mushi | 78 | | ✓ |
| Maria Morisi | 62 | ✓ | |
| Anna Subaiya Okama | 72 | ✓ | |
| Maria John Ngadoru | 65 | | ✓ |
| Issac J. Babu | 56 | | ✓ |
| Constantine Jacob | 53 | | ✓ |
| Beda J. Ngadoru | 58 | | ✓ |
| Margareth Matei Mboro | 53 | ✓ | |
| Martha Massawe | 69 | ✓ | |
| Padri Patrick P. Soka | 58 | | ✓ |
| Arbogast Marina Sangisi | 49 | | ✓ |
| Donath J.P Mboya | 49 | | ✓ |
| Greceana Prosper Massawe | 48 | ✓ | |
| Severa J.K Mushi | 49 | ✓ | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Editha Edward | 48 | ✓ | |
| Mwalimu berna Munishi | 59 | ✓ | |
| Aloyce Abdu Minja | 74 | | ✓ |
| Redemtha P. Mssele | 50 | ✓ | |

Jedwali Na. 3 Kundi la Vijana

| **JINA** | **UMRI** | **KE** | **ME** |
|---|---|---|---|
| Manka J. Mushi | 39 | ✓ | |
| Upendo Kyara | 30 | ✓ | |
| Martine Mafikiri Joseph | 32 | | ✓ |
| Jerome J. Mboro | 35 | | ✓ |
| Agricola Joseph | 32 | ✓ | |
| Coletha H. Tarimo | 44 | ✓ | |
| Aman Kavishe | 35 | | ✓ |
| Betreace Mlayi | 23 | ✓ | |
| Happness Malya | 24 | ✓ | |
| Grace P. Massawe | 23 | ✓ | |
| Eliza Morisi Massawe | 20 | ✓ | |
| Deogratius M. Fikiri | 36 | | ✓ |
| Richard M. Lelo | 30 | | ✓ |
| Theresia Donath | 37 | ✓ | |
| Domitila Albin mushi | 27 | ✓ | |
| Condrad Mathew | 32 | | ✓ |
| Jerome Peter Soka | 42 | | ✓ |
| Jastine Lekundayo Mallya | 43 | | ✓ |
| Lawrence Mushi | 40 | | ✓ |